Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Pili - Tarehe 3 Novemba, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima kabla hatujaanza ningependa kutambulisha Waheshimiwa Wabunge Wanawake kutoka nchi kadhaa za *SADC* ambao wametutembelea katika Bunge letu siku ya leo, tunawakaribisha. *(Makofi)*

Swali namba 15 lilifutwa na muuliza swali Mheshimiwa Jackson M. Makwetta.

Na. 16

**Fedha za Barabara Jimbo la Morogoro Kusini - Mashariki**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza: -

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali langu kuhusu barabara za jimbo la Morogoro Kusini - Mashariki hapo tarehe 27 Julai, 2004 ilitaja kiasi cha fedha kilichoombwa lakini haikutaja kiasi kilichotolewa na vile vile ilitaja barabara za Mvomero yaani Jimbo la Morogoro Kaskazini na za Jimbo la Morogoro -Kusini-Mashariki zilizoulizwa: -

(a) Je, wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini-Mashariki walielewaeje jibu la Serikali, kwamba fedha za barabara za Kidunda, Mkulazi, Usungura, Kiwege, Koo, Kikundi, Kungwe, Lubungo na Msomvizi zilipelekwa kutengeneza barabara kwenye majimbo mengine yaliyotajwa kwenye jibu la msingi la swali langu?

(b) Kama ni kweli, je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inawagawa Wanamorogoro na pengine ni tabia ya mtu tu kufanya *reallocation* zisizo za msingi?

(c) Kama hali hiyo sio kweli, je, ni nani alitoa jibu hilo la kumdanganya Waziri na Serikali inachukua hatua gani sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini-Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba tarehe 27 Julai, 2004 wakati najibu swali Na. 317 la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini-Mashariki, nilitaja barabara za Mvomero katika Jimbo la Morogoro Kusini badala ya zile za Morogoro Kusini-Mashariki bali nilitoa maelezo kuhusu miradi ya barabara iliyokuwa inatekelezwa katika Wilaya ya Morogoro kwa ujumla kwa kuwa barabara hizi zinawaunganisha wananchi wa Wilaya yote ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara zilizoko katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge alizozitaja gharama za matengenezo ziko kama ifuatavyo ili kuweka kumbukumbu sahihi:-

(i) Barabara ya Ubena-Ngerengere, mwaka 2002/2003 zilitumika shilingi 20,000,000/=. Mwaka 2003/2004 hakukuwa na fedha zilizotengwa. Mwaka 2004/2005 zilitengwa shilingi 9,000,000/=.

(ii) Barabara ya Ngerengere-Kidunda mwaka 2002/2003 ni shilingi 30,308,804/= zilitumika kwa matengenezo ya barabara hiyo. Mwaka 2003/2004 shilingi 53,126,400/= na mwaka 2004/2005 zilitumika shilingi 23,458,000/=.

(iii) Barabara ya Mtego wa Simba - Ngerengere mwaka 2002/2003 shilingi 15,600,000/=, mwaka 2003/2004 hapakutengwa fedha na mwaka 2004/2005 zimetengwa shilingi 11,458,000/=.

(iv) Barabara ya Msomvizi-Mikese-Lubungo kwa mwaka 2003/2004 zilitengwa shilingi 9,900,000/= na mwaka 2004/2005 zimetengwa shilingi 4,500,000/=.

(v) Barabara ya Madamu - Kinole kwa mwaka 2003/2004 ni shilingi 366,006,300/= na mwaka 2004/2005 shilingi 4,720,000/=

(vi) Barabara Kinole (Tandai) - Tegetero kwa mwaka 2003/2004 ni shilingi 49,357,715/= na 2004/2005 ni shilingi 2,800,000/=. Kwa hiyo, kwa mwaka 2002/2003 jumla shilingi 66,908,804/=, kwa mwaka 2003/2004 shilingi 478,400,415/=, mwaka 2004/2005 shilingi 55,936,000/= na kwa mwaka 2005/2006 zimetengwa fedha kupitia *TASAF* kwa ajili ya Tegetero- Hewe shilingi 50,000,000/=.

Kwa hiyo, napenda kuwatoa wasiwasi wananchi wa Kidunde, Mkulazi, Usungura, Kiwenge, Koo, Kikundi, Kungwe, Lubungo na Msomvizi na Mbunge wao kuwa fedha za

barabara zinaendelea kufanya kazi katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge kama ilivyopangwa na Serikali na Taasisi husika.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, katika sehemu (a) ya maelezo yangu, kwa taarifa tulizonazo hakuna ujanja wowote uliotumika kuhamisha fedha hizi kwenda katika eneo lingine kinyume cha taratibu na hivyo suala la kuwagawa wananchi halipo.

(c) Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Waziri hakudanganywa katika kutoa jibu Bungeni kwa sababu taarifa zilizotolewa katika jibu la msingi ni sahihi na zimetaja ufadhili wa Serikali na Taasisi mbalimbali Kiwilaya ikiwa ni pamoja na Jimbo la Mororgoro Kusini-Mashariki.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata majibu mazuri haya, sasa ndio majibu mazuri ambayo nilikwambia kwamba maswali sio mkopo na majibu sio malipo. Sasa haya ni majibu ambayo yameeleza vizuri, kwanza alitekeleza ahadi yake nilipomwahidi aje Morogoro Kusini-Mashariki alitembelea wiki iliyopita.

Sasa nina swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa barabara hiyo imetengewa shilingi 9,000,000/= na kuna daraja pale maeneo ya Ubena ambalo juzi tulikuwa na wananchi wa maeneo yale tulikuwa tunajitolea kufukia ile barabara na wananchi wa Ngerengere. Sasa tumepewa shilingi 9,000,000/= na mimi nimeshatoa mifuko 20 ya *cement* kutengeneza daraja kwa nguvu za wananchi na Profesa Phillemon Sarungi, kwa sababu aliniahidi kutengeneza, sasa naomba, je, ataongeza kiasi lile daraja la Ubena litengenezwe? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sidhani kama tutakuwa na uwezo wa kuongezea fedha ili kuweza kukamilisha zoezi hilo kwa sababu mpango ule wa barabara uliowasilishwa ndio uliotuwezesha kutenga kiasi hicho cha fedha na hakika tungekuwa na fedha kutokana na ziada nyingine zozote tusingesita kufanya hivyo. Kwa hiyo, nadhani kwa fedha zilizopo tujitahidi tufanye kitakachowezekana mwakani unaweza tena ukatuomba, tunahakika tutakusaidia tu.

**MHE. SULEMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, napenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kwa kuwa fedha hizi za barabara zinapitia Halmashauri ya Wilaya na kwa kuwa Madiwani pamoja na Halmashauri kwa ujumla ndio inasimamia lakini zipo taasisi nyingine nazo zinatoa fedha kwa barabara hizo ikiwemo *VCHDP, TASAF* na mfuko wa *Road Toll* na barabara ile ile inapata fedha mara tatu au mara nne jambo ambalo tulishalalamika, je, Serikali iko tayari kufuatilia Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini kwa fedha ambazo zimepangwa mara tatu au mara nne kwa barabara moja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida tatizo kama hilo halipaswi kutokea kwa sababu mpango unapopangwa tukipata mfadhili kwa kawaida tunapenda ufadhili ufanye kazi nyingine ili kuendeleza na ku-*spread* shughuli za maendeleo.

Kwa hiyo, ninachoweza kumwomba Mheshimiwa Suleiman Sadiq, pengine ukipata nafasi tungekutana pale ofisini tujaribu kuliona tatizo likoje, halafu tutaona namna ya kuzielekeza Halmashauri husika.

Na. 17

**Uchafuzi wa Mazingira**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza: -

Kwa kuwa hivi sasa idadi ya watu wanaokufa kutokana na uchafuzi wa Mazingira *(Air Pollution)* inaongezeka hapa duniani, je, Serikali itakubaliana nami kwamba upo umuhimu wa Serikali za Mitaa kutunga sheria ndogo za kudhibiti hali hiyo mijini ambako kuna idadi kubwa ya watu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli uchafuzi wa mazingira unaongezeka. Ukweli huu unathibitishwa na taarifa mbalimbali tunazozipata kwa kuona na pia kuzisikia kutoka vyombo mbalimbali ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tunashuhudia kuwepo uchafuzi wa mazingira na hususan maeneo ya mijini ambako kuna makazi ya watu wengi. Sababu mojawapo ya kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira ni ongezeko la wakazi na ongezeko la shughuli mbalimbali zinazofanywa pasipo kuzingatia sheria. Uchafuzi wa mazingira unasababisha madhara mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusababisha vifo kwa wanadamu, wanyama na viumbe hai.

Mheshimiwa Spika, chini ya vifungu namba 80 na 54 kifungu kidogo cha (1)(d) vya sheria Serikali za Mitaa Na. 8 ya mwaka 1982. Mamlaka za miji zina nguvu za kisheria za kutunga sheria ndogo za kudhibiti uchafuzi wa mazingira mijini ambako kuna makazi ya watu wengi na viwanda vingi ambavyo baadhi vinachangia katika uchafuzi wa mazingira. Kwa upande wa vijijini, Mamlaka za Wilaya pia zimepewa madaraka ya kutunga sheria za kudhibiti uchafuzi wa mazingira chini ya vifungu Na. 111 (a) kifungu kidogo cha pili na 148 vya sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 ya mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, napenda basi kuziagiza Halmashauri zote nchini kama bado hazijafanya hivyo kuzingatia wajibu wao huu wa kutunga sheria ndogo zinazohusu uchafuzi wa mazingira katika maeneo yake kuzisimamia na kuwaelimisha wananchi ili wazielewe na kuzifahamu kwa faida yao na Taifa kwa ujumla.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa chanzo kikubwa cha magonjwa ya kuambukiza ni uchafu na kwa kuwa inaaminika zaidi ya asilimia 75 ya magonjwa ya kuambukizwa yanasababishwa na uchafu, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuzipatia Halmashauri za Miji na Wilaya magari ya kuzoa takataka na maji machafu ili magari hayo yaweze kuzoa takataka na maji machafu kuliko hali ilivyo sasa?

Swali la pili, kwa kuwa hivi sasa imezuka tabia ya kuchoma takataka katikati ya miji kabisa na kuchafua hali ya hewa au *pollution air combustion* na kuleta madhara kwa afya ya kibinadamu, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atachukua hatua gani kwa matatizo ambayo yanajitokeza katika miji yetu ya uchomaji wa takataka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kila inapopata uwezo kifedha kutoa magari kwa ajili ya kuzoa takataka katika maeneo ya miji na hasa katika Majiji pamoja na Manispaa. Tatizo tunalolipata ni uwezo mdogo lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge uwezo ukipatikana juhudi zitaelekezwa katika maeneo hayo bila wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kuhusu uchomaji taka ovyo mijini na hivyo kusababisha hali ya kero kwa wananchi na vilevile bughudha ninaloweza kusema ni kwamba moja ya sababu kwa kweli ya kupeleka madaraka kwa wananchi ni kutaka watumie fursa na mamlaka waliyopewa kujaribu kupambana na mambo yote ambayo yako katika maeneo yao. Kwa hiyo, rai yangu kwa Halmashauri zote ni kujaribu kutumia *opportunities* hizi kutunga sheria ndogo ndogo, kutumia wataalam waliopo na viongozi wengine katika ngazi ya chini kuweza kuwabana wale wote ambao wanavunja taratibu au wanachafua mazingira kutokana na kutokuelewa ili kuepusha athari ambazo zinaweza kujitokeza.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nina uliza tu swali kuhusu hii mifuko ya *plastic* ambayo sasa kwanza haiozi na imeenea nchi nzima na imefanya uchafuzi mkubwa sana na haiozi ile mifuko, je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa kupiga marufuku mifuko hiyo na badala yake ije mifuko ya karatasi ambayo inaweza ikaoza na ikachomeka kuliko sasa nchi ilivyochafuka namna hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati tulipowasilisha hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais tulisema hivi kuhusu mifuko ya *plastic* kwamba Serikali sasa hivi tunachukua hatua za kutafuta utaratibu wa kuipiga marufuku mifuko yote ya *plastic* isiyooza lakini kisayansi. Kwa hiyo, tunaendelea na hatua hizo ili tufike mahali Serikali iamue kwa pamoja ni mifuko ipi ya *plastic* tutakayoipiga marufuku.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la Mheshimiwa Waziri anasema Serikali inafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba katika nchi yetu mazingira yanahifadhiwa kwa ajili ya usalama wa Watanzania, ni miaka mingi sasa mimi humu ndani nalalamika sana juu ya athari ambayo nchi inaweza kupata kutokana na kiwanda cha *SPM Mgololo?*

Kwa kuwa kiwanda kile kimebinafsishwa, nadhani mwezi wa pili mwaka 2003 lakini wananchi hatuna hakika nini kinaendelea pale, je, Serikali ipo tayari kuandaa taarifa ya kuwaambia Watanzania juu ya hali inayoendelea pale kimazingira?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kuandaa taarifa kuhusu kinachoendelea katika kiwanda cha Mgororo na kwa kifupi tu kiwanda kile sasa hivi wamekwishanunua vifaa vyote ambavyo vinahitajika kukarabati kwa sababu kilikaa miaka zaidi ya 15 bila kufanya kazi. Wataalam wamekwisha kuja nchini wapatao 17, dawa zimekwishaagizwa na kazi iliyopo sasa hivi ni kuandaa uzalishaji ambao utaanza mara moja na kuwatoa wasiwasi wananchi wa Mufindi. Dawa zile zimekwisha korogwa na hakutatokea mlipuko wa aina yoyote. Taarifa kamili itafuata kwa maandishi. Nashukuru. *(Makofi)*

Na. 18

**Wataalam Wazalendo**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza: -

Kwa kuwa, nchi yetu inahitaji sana wataalam wazalendo ambao wapo nje ya nchi, je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhamasisha wataalam hao kurudi na kuitumikia nchi yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kupitia sera ya Menejimenti na ajira katika Utumishi wa Umma, Serikali imechukua hatua mbali mbali na inaendelea na jitihada za kuhamasisha wataalam wazalendo kuja kutumikia nchi yao. Hatua ambazo Serikali imechukua ni pamoja na ifuatavyo: -

(i) Kuongeza mshahara na marupurupu mengine kwa kiwango kitakachoongeza tija na kuwa kivutio kwa wataalam wenye sifa.

(ii) Nafasi ya ajira katika Utumishi wa Umma zitakuwa za uwazi ushindani hivyo kutoa nafasi za ajira kwa watu wenye sifa waliopo ndani na nje ya nchi. Nafasi hizo utangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari na tovuti.

(iii) Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuweka vitendea kazi bora na vya kisasa katika maeneo ya kazi. Kwa kuwa Serikali inazo taarifa za wazalendo walioko nje kila wanapohitajika mawasiliano hufanyika na kama watapenda kurudi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuweka mazingira ya uchumi kukua, amani na utulivu kijamii na kisiasa ili wataalam wazalendo walioko nje waweze kushawishika na kurudi nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuboresha hali ya uchumi, Serikali inafanya kila jitihada kuridhia mikataba na kuweka taratibu nzuri za ushirikiano na jumuiya mbalimbali kama Afrika ya Mashariki, *SADC* ili kuwezesha Watanzania kufaidika na nafasi za ajira hapa nchini na katika jumuiya hizo zinazotokana na ushirikiano huo.

**MHE.WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri sijui Serikali ina mpango gani kwa wataalam ambao wako nje na ambao wana vifaa vyao na utaalam wao na wangependa kurudi hapa nchini kwa kuwekeza na kuhama na vifaa vyao walivyo navyo huko nje kwa ajili ya manufaa ya Watanzania walioko hapa nchini ili waje hapa wajiajiri lakini kwa kuwekeza zana walizonazo huko nje, Serikali inawasidiaje watu hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali ya uwekezaji ni kuvutia wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi na hasa Watanzania waliko nje itakuwa vyema zaidi wakirudi pamoja na vifaa na utalaam walio nao na nina hakika wengi kama ni wachache lakini wapo wanaorudi lakini narudia tena kusema kwamba hii hali ya utulivu na usalama na jinsi Serikali inavyokuza na kuweka hali ya kiuchumi katika hadhi ya kuvutia

wawekezaji nina hakika Watanzania ni pamoja na wale watakao taka kuja kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tukumbuke kuwa Watanzania kufanya kazi nje inaonyesha uwezo wa Watanzania kuweza kuhimili ushindani kama nchi zingine zinavyoweza kuhimili ushindani wa kupata hizo nafasi za kazi.

Kwa hiyo, wale Watanzania ambao kweli wametumia utaalam wao na uwezo kupata kazi nchi nyingine tunapaswa kuwapongeza na wakati huohuo kuwavutia kurudi nchini kuja kushirikiana na wenzao katika kutoa mchango wao ndani ya nchi yao. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea jibu la Mheshimiwa Waziri wa Nchi Utumishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha tumeanza kufikiria dhana ya namna ya kutumia fursa za Watanzania walioko nje na wanaofanya kazi nje.

Kwanza kama chanzo cha fedha za kigeni kwa sababu wanapoleta fedha ndani ya nchi kutoka nje wanatuletea fedha za kigeni sawasawa na mtu aliyeuza pamba na katika uchumi jambo hili linaitwa *remiterses* kwa hiyo tunadhani kuna fedha nyingi sana za Watanzania walio nje ambao wanazileta ndani na zile tungeweza tukazihesabu kama ni pato la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, inawezekana vilevile Watanzania hao wakahesabiwa kama ni wawekezaji wanapoleta mali zao kutoka nje mpaka ndani ni wawekezaji sawa na ungeenda kuleta mwekezaji wa huko aliko. Kwa hiyo, fursa gani wapewe watu hawa ni suala ambalo Hazina tunalifikiria na tunaomba maoni ya Watanzania juu ya suala hilo ili kwenye Bajeti ijayo tuweze kulileta hapa Bungeni ili muweze kulifikiria

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika utafiti uliofanywa unaonyesha kuwa taasisi za watu binafsi zinatoa maruprupu mazuri kuliko za Serikali, je, kuna mpango gani kuhakikisha kuwa tunawalinda wataalam wetu Serikalini kulinganisha na wataalam wanaofanya kazi katika taasisi za watu binafsi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi sana kuweka hali nzuri kwa watumishi wake, kwanza ukiangalia sasa hivi kima cha chini cha Serikali kiko juu kuliko kima cha chini cha nchi, kwa hiyo, hiyo ni namna mojawapo ya kuweza kuweka mazingira mazuri kwa watumishi wa Serikali.

Lakini pamoja na hivyo kwa mujibu wa sera ya ajira na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Serikali inajitahidi sana kuboresha hasa mishahara ya wataalam na *professional staff* ili tuweze kuwavutia wale ambao wako kwenye ajira binafsi kuja ndani ya Serikali na wale waliopo nje vilevile kupenda kufanya kazi ndani ya Serikali ili

kuweza kuongoza uchumi huu ambao ni huria ambao unahitaji utumishi wa umma ambao ni bora na ambao unaelewa jinsi uchumi unavyokuwa na uweze kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuweza kukua ndani ya nchi na uchumi kuwa bora zaidi na mapato ya Serikali kuwa bora zaidi ili iwe chanzo cha Serikali kuendelea kuboresha hali ya utumishi wa umma.

Na. 19

**Ruzuku kwa Sekta Binafsi**

**MHE. MONICA N. MBEGA** aliuliza: -

Kwa kuwa, jukumu la kusukuma gurudumu la maendeleo haliwezi kutekelezwa na Serikali peke yake, na kwa kuwa Serikali imekuwa ikihimiza watu binafsi, taasisi na mashirika ya dini kuunga mkono juhudi hizo, je, Serikali inasemaje kuhusu kutoa ruzuku kwa sekta binafsi zinaoendesha shughuli za elimu na afya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini, napenda kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Monica Mbega, kuwa jukumu la kusukuma gurudumu la maendeleo haliwezi kutekelezwa na Serikali peke yake bila kushirikisha sekta binafsi. Kwa kipindi cha takriban miongo miwili, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kujenga mazingira ya kuimarisha sekta binafsi ili kuifanya iwe mshiriki mkuu wa Serikali katika kuleta maendeleo nchini kwa utaratibu wa *Public Private Partnership*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Monica Mbega, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Mpango wa Elimu ya Sekondari *(MMES)* ruzuku inatolewa kwa shule za sekondari kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Bajeti ya Waziri kwa Elimu na Utamaduni mwaka huu. Katika kutekeleza mwaka wa kwanza wa mpango huo yaani 2004/2005, Serikali itatoa ruzuku kwa sekta binafsi kama ifuatavyo: -

(i) Shilingi 15,000 kwa wanafunzi kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunza kwa sekondari ambazo haziendeshwi kibiashara na siyo Seminari.

(ii) Shilingi 10,000 kwa mwanafunzi kwa ajili ya gharama za uendeshaji kwa sekondari zisizo za Serikali ambazo sio za kibiashara na sio Seminari.

(iii) Kutoa ruzuku ya maendeleo kwa mwenye shule aliyeidhinishwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa ajili ya ujenzi wa shule za wanafunzi wenye ulemavu kwa viwango sawa ile inayotolewa kwa ajili ya Sekondari za Serikali, zinazojengwa na wananchi.

(iv) Serikali kuanzia mwaka 2004/2005 imekuwa ikitoa ruzuku kwa vyuo binafsi vya elimu ya juu na Sekondari binafsi kupitia Mfuko wa Elimu ya Juu unaosimamiwa na Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu.

Kwa mfano *St. Augustine University* (Bugando) imetengewa shilingi milioni 110.3, *Tumaini University* -Dar es Salaam imetengewa shilingi milioni 241.6, *Hurbert Kairuki University* imetengewa shilingi milioni 141.0, *St. Augustine University* (Nyegezi) imetengewa shilingi milioni 147.988, *Tumaini University* (Iringa) imetengewa shilingi milioni 214.8, Binza Sekondari, Maswa imetengewa shilingi milioni 35, Kibaha Sekondari imetengewa shilingi milioni 130.6, *St. Joseph* Sekondari, Mbozi shilingi milioni 80.0, *St. Joseph Teachers College,* Moshi shilingi milioni143.0 na *Midlands High School* shilingi milioni 83.4.

Aidha, Serikali imeanza kulipa ada ya wanafunzi wanaosomea uganga kwenye vyuo binafsi sambamba na wale wa vyuo vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwaruhusu walimu waliosomeshwa katika vyuo vya Serikali kuendelea kutumiwa na shule za watu binafsi na pia waliosomeshwa kwenye vyuo vya watu binafsi kuajiriwa na Serikali.

Kwa upande wa sekta binafsi ya afya, kuna hospitali za aina mbili. Aina ya kwanza ni zile ambazo zinaendeshwa kibiashara, wakati aina ya pili ni zile ambazo haziendeshwi kibiashara kama vile za madhehebu mbalimbali ya dini. Pamoja na misamaha ya kodi inayotolewa na Serikali kwa ajili ya kuzisaidia hospitali zote nchini, kwa zahanati, vituo vya afya na hospitali za madhehebu, Serikali inatoa misamaha ya kodi na ushuru wa leseni.

Mheshimiwa Spika, kwa hospitali zisizoendeshwa kibiashara, Serikali inatoa ruzuku ya vitanda kwa hospitali teule za madhehebu ya dini. Aidha, Serikali inalipa mishahara ya waganga na watumishi wengine wanaofanya kazi katika hospitali hizo. Hospitali hizi pia zinapata asilimia 100 ya gharama za matumizi ya kawaida kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingependa kusaidia zaidi sekta hizi lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti inashindwa.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na yanaonyesha jinsi ambavyo Serikali inajali wananchi wake. Swali dogo la nyongeza ni kwamba; kwa kuwa katika shule hizi za binafsi kumekuwa na watoto ambao wanafiwa na wazazi wao na kwa

kuwa Serikali tayari imeshatangaza kutoa ruzuku hizo ambazo zitatolewa kwa sekta binafsi lakini pia kwa upande wa Serikali kupunguza ada.

Je, Serikali itakubali kuwatoa watoto waliofiwa na wazazi kutoka shule binafsi ili waingie Sekondari za Serikali ili kufaidi ile ruzuku ambayo Serikali itatoa kuanzia mwakani na hivyo kuwafanya hao watoto wasikose nafasi ya kuendelea na masomo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI (k.n.y WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Monica Mbega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa misaada hii kwa watoto wa familia zisizo na uwezo wa kifedha inayo masharti na sharti mojawapo ni kwamba wale wanaopewa misaada hii lazima wawe wamefaulu mitihani na katika baadhi ya shule za binafsi vile viwango vya kufaulu watoto kwenda sekondari bado sio vya kuridhisha kama vile viwango vinavyotumika kwenda katika shule za Serikali. Lakini jambo hili bado naendelea kufuatilia kuweka utaratibu ambao kuendelea na elimu iwe katika shule ya binafsi au ya Serikali kuzingatia suala la kufaulu na tutakapokuwa tumefika hapo wazo la Mheshimiwa Mbunge tunaweza kulitilia maanani.

**MHE. LEDIANA M. MNG’ONG’O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nashukuru kwa majibu mazuri ambayo yametolewa nina swali. Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kutoa ruzuku katika elimu na ruzuku katika hospitali, je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku kwa vituo vinavyolea watoto yatima kama kituo cha Tosamaganga ambacho kina watoto wengi yatima?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lediana Mng’ong’o. kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa ruzuku katika maeneo mengi sana na naamini hata katika vituo vya kulelea watoto kama alivyotaja Mheshiwa Mbunge vipo vinavyopata ruzuku. Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba Serikali inasisitiza zaidi *public private partnership,* kwa hiyo, pale ambapo Serikali haiwezi kutoa ruzuku basi sekta binafsi inatoa pia ruzuku. Lakini iwapo kituo hiki kina hali mbaya sana basi Mheshimiwa Mbunge anaweza akawasiliana na Wizara kuona kwamba tutafanyaje.

Mheshimiwa Spika, nilijibu katika jibu langu la msingi nilieleza ruzuku ambayo Serikali inatoa. Lakini pamoja na ruzuku hii Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa ajili ya sekta binafsi na mashirika ya dini. Kwa mfano, *Hulbert Kairuki University* wamepewa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 840 na *St. Joseph Secondary School,* Mbozi wamepata shilingi milioni 150 na *Missionary Sisters Pressures Blood* wamepata shilingi milioni 145. Kwa hiyo, taratibu pamoja na jitihada kubwa ambayo Serikali inafanya hata kwenye vituo vya watoto yatima Serikali hatimaye itafika. Naahidi katika mwaka ujao linaweza likafikiriwa.

Na. 20

**Kuwezesha Wavuvi**

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM (k.n.y. MHE. ALHAJ AHAMADI H. MPEME)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inao mkakati wa kuondoa umaskini na kwa kuwa uvuvi ni moja ya kazi inayotegemewa na wananchi wengi waishio kando kando ya Bahari, Mito na Maziwa; na kwa kuwa kutokana na uwezo mdogo walio nao wanachi hao wanashindwa kutumia raslimali hiyo ili kuondoa umaskini.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo ili waondokane na umaskini?

(b) Je, ni vikundi vingapi vya wavuvi wadogo wadogo vimepewa mikopo ya zana za kisasa za uvuvi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za makusudi kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kupambana na umaskini. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kufanya tathmini ya hali halisi ya sekta ya uvuvi kupitia mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya uvuvi *(Fisheries Master Plan Study)* ambao ulikamilika mwezi Mei, 2002 na kutambua maeneo 15 ya kupewa kipaumbele. Kati ya maneoneo hayo 15 eneo moja linahusu kuwajengea uwezo wavuvi wadogo wadogo wakiwemo wa mwambao wa Bahari ya Hindi. Kufuatia kukamilika kwa mpango huo, Serikali inakamilisha taratibu za kuendesha mradi wa *Marine and Coastal Environment Management Program (MACEMP)* ambao chini yake kuna kipengele cha kutoa misaada ya zana za uvuvi kwa wavuvi wadogo wadogo pamoja na kuboresha miundombinu ya maeneo ya uvuvi.

Chini ya mradi huu wa *MACEMP* wavuvi wadogo wadogo wataweza kupata zana za kisasa kwa utaratibu maalum unaoandaliwa hivi sasa. Mradi wa *MACEMP* unatarajiwa kuanza katikati ya mwaka 2005.

Aidha, Serikali itawapatia wavuvi hao elimu ya kuwawezesha kuandaa rasimu ya miradi *(Project Proposals)* kwa ajili ya kuomba mikopo kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya fedha.

(ii) Pia kuwapatia wavuvi wadogo wadogo mafunzo yanayohusu uvuvi endelevu na uhifadhi bora na salama wa mazao ya uvuvi.

(iii) Kuanzisha mifuko ya kuweka na kukopa.

(iv) Ujenzi wa soko la kisasa la Feri, Dar es Salaam na ujenzi unaoendelea wa soko la samaki la Kirumba, Mwanza, ili kuongeza ubora wa mazao ya uvuvi.

(v) Kuanzisha na kusimamia maeneo Tengefu ya Hifadhi ya Bahari za Mafia na *Mnazi Bay* ili kulinda mazalio ya samaki.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumuarifu Mheshimiwa Alhaj Ahamad Hassan Mpeme na wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara ya kuwa jumla ya vikundi 77 vya wavuvi wadogo wadogo vimepewa mikopo na wahisani mbalimbali kwa ajili ya kununulia zana za kisasa za uvuvi.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uvuvi ndio tegemeo kubwa kwa wananchi wanaoishi kando kando mwa Mto Ruvuma na kwa kuwa inaonekana kwa idadi ya samaki kwenye mto huo imepungua sana, hivyo kuwafanya wananchi kuvuka mpaka na kwenda kuvua kwenye mito iliyoko Msumbiji, je, Serikali iko tayari kufanya utafiti na kama itabainika hivyo itachukua hatua gani ili kuwasaidia wananchi hao kiuchumi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII :** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aridi Uledi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali siku zote inafanya utafiti katika maeneo mbalimbali hasa katika maeneo ya Bahari pamoja na Mito na ndio maana kuna chombo hiki cha utafiti cha *Tanzania Fisheries Research Institute* ambayo inafanya utafiti katika maeneo mbalimbali. Lakini hivi sasa pia tuna waelekeza wananchi waweze kupanda samaki hawa ili waweze kuvuna samaki kwa sababu unaweza kuvuna bila ya kutumia Bahari au Mito. Kwa hiyo, hili nasema tunalisisitiza hivi sasa suala zima la *agriculture* lakini utafiti pia utazidi kuendelea katika maeneo mbalimbali ya Mito na Bahari.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na kwa kuzingatia kwamba alishatembelea Visiwa vya Ukerewe najua kwamba ni maeneo haya ambayo yamefanya Tanzania iwe maarufu kwa kupeleka samaki nje ya nchi zaidi ya asilimia 50 ya samaki wanaopelekwa nje wanatoka katika visiwa hivi. Je, katika mpango huo wa mwaka 2005 sikusikia kama kuna Ukerewe imetajwa?

Je, Mheshimiwa Waziri atahakikisha kwamba Ukerewe imetajwa ambayo ina maji asilimia 80, Wilaya ya Ukerewe ni maji na kwamba wavuvi wote, watu wote wa Wilaya ile wanategemea uvuvi?

Je, ataipa kipaumbele Ukerewe katika huo mpango wa mwaka 2005?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kama ifuatavyo:-

Tunatambua umuhimu wa Kisiwa cha Ukerewe na ndio maana kama alivyosema kwamba mimi binafsi nimetembelea lakini baada ya hapo pia maafisa mbalimbali wameweza kutembelea katika maeneo hayo na kama nilivyoeleza kwamba tuna mpango kabambe wa *Fisheries Master Plan* ambao ni wa Taifa zima. Hii programu ambayo nimeitaja hivi sasa ya *MACEMP* ni tofauti ambayo inashughulikia katika maeneo ya Pwani. Lakini nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara inatambau umuhimu wa Ukerewe na wavuvi wa Ukerewe na kwamba tutajitahidi tuwezavyo.

Na. 21

**Usimamiaji wa Misitu ya Asili**

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa usimamiaji wa Misitu ya Asili katika ngazi mbalimbali za Serikali haueleweki vizuri na Taasisi zilizopewa jukumu la kusimamia misitu ya aina hiyo hazifahamiki kwa wananchi na kwa kuwa hivi sasa misitu ya asili katika milima ya Ukaguru ambayo pia ni chanzo kikubwa cha maji katika Wilaya ya Kilosa kwenye Mito ya Kitete, Msowero, Mvumi, Rudewa na Mkondoa imeanza kuvamiwa na wakata miti kwa utaratibu usioeleweka:-

(a) Je, Misitu ya asili katika milima Ukaguru, Wilayani Kilosa inasimamiwa na nani na kwa utaratibu upi?

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani za haraka za kuzuia ukataji ovyo wa miti katika misitu hiyo ili kuokoa vyanzo vya mito inayotegemewa kutoa maji kwa matumizi ya wananchi, hususan wa Tarafa ya Gairo yenye uhaba mkubwa wa maji?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wilaya ya Kilosa ina misitu 16 iliyohifadhiwa yenye hekta 85,154.5 Hekta 1,619.1 kati hizi ni misitu ya hifadhi ya uvunaji na hekta 83,535.4 ni misitu ya hifadhi ya vyanzo vya maji na ardhi dhidi ya mmomonyoko wa udongo. Misitu yote hii ikiwa ni pamoja na iliyopo kwenye milima ya Ukaguru ni misitu ya Hifadhi ya Taifa na inasimamiwa na Serikali Kuu kupitia Mradi wa Misitu ya Hifadhi *(Catchment Forestry Project)* na inashirikiana na Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji. Ushirikishwaji wa Serikali za Vijiji vitatu vya Mamboya, Kiyegeya na Kitange II vilivyo karibu na msitu wa Hifadhi wa Mamboya umeanza na utaendelezwa katika misitu mingine.

(b) Ni kweli ukataji wa miti umefanyika katika eneo la Kijiji cha Masenge kwa ajili ya mashamba. Eneo hili liko nje ya msitu wa hifadhi wa Mamiwa Kaskazini ambao ni moja ya vyanzo vya maji. Aidha, ni kweli kuna matukio machache ya ukataji miti katika misitu ya hifadhi katika safu ya milima ya Ukaguru kwa ajili ya kuni, nguzo na mbao. Ili kuzuia ukataji miti ovyo, Serikali imesimamisha uvunaji wa miti katika misitu ya asili nchi nzima kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2004 hadi tarehe 31 Januari, 2005. Katika kipindi hiki, Serikali itaandaa utaratibu bora wa uvunaji.

Aidha, Serikali itaendeleza doria katika misitu ya hifadhi kwenye milima ya Ukaguru kwa kushirikisha Serikali za Vijiji ili kuzuia ukataji wa miti ili kuokoa vyanzo vya mito inayotegemewa kutoa maji kwa matumizi ya wananchi, hususan wa Tarafa ya Gairo yenye uhaba mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuimarisha doria, Serikali itaendelea na jitihada za kuwaelimisha na kuwahimiza wananchi wapande miti na wahifadhi misitu ya asili ambayo wataimiliki na kuisimamia ili iwapatie mazao na huduma mbali mbali zinazotokana na raslimali hii. Hii itapunguza shinikizo la uvunaji kwenye misitu ya hifadhi ya asili.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa msitu huu wa Mandege unavunwa sana mbao za nguzo kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri. Sasa je, Serikali iko tayari kutoa mrabaha ili tuweze kupanda miti mingine katika msitu huo kwa sababu sasa hivi hawatoi chochote?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christopher Wegga, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza kwamba kwa kweli Serikali inasimamisha uvunaji wa misitu katika maeneo haya yote ya misitu ya asili ili kufanya *inventory* na kujua miti mingapi? Ya aina gani na halafu utaratibu gani wakuwashirikisha wananchi?

Mheshimiwa Spika, nipende kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria ambayo tuliipitisha hapa ya misitu ya mwaka 2002 inatoa nafasi kwa wananchi wenyewe pia kuwa na maeneo ya Hifadhi za Misitu. Kwa hiyo, hapo hapo wananchi wenyewe wanaweza kufaidika mmoja mmoja bila suala zima la mrabaha.

Na. 22

**Sheria ya Uchunguzi wa Maiti**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu mwaka 2002 iliahidi kuangalia upya sheria ya uchunguzi wa maiti zinazotokana na vifo visivyo vya kawaida kama

kujinyonga, kutumbukia visimani na kadhalika ili kuondoa kero ya wananchi kulinda maiti hizo kwa siku tatu hadi nne wakisubiri Polisi na Madaktari kwa ajili ya uchunguzi. Je, Serikali imetafuta ufumbuzi gani kwa hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uchunguzi wa maiti zinazotokana na vifo vya kutatanisha katika maeneo yasiyo na huduma za Polisi husababisha kero kubwa kwa wananchi kulinda maiti hizo kwa siku mbili hadi tatu wakisubiri Polisi na Madaktari kwa ajili ya uchunguzi. Baada ya kuchunguza malalamiko haya Serikali imebaini kuwa kero hiyo haisababishwi na kasoro za sheria ya uchunguzi wa maiti, bali inatokana na upungufu wa vitendea kazi kama usafiri, vyombo vya mawasiliano na pia huduma za polisi na hospitali kuwa mbali na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero hiyo kwa wananchi, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Serikali inaongeza vitendea kazi mbalimbali vya usafiri kama magari, pikipiki na boti na hivyo kuweza kulifikia eneo la tukio haraka yaani siku hiyo hiyo. Mwaka huu wa fedha kwa mfano Wilaya zote nchini zitapata magari yatakayosaidia kuwafikisha haraka wapelelezi kwenye matukio ya uhalifu.

(ii) Kuongeza na kusambaza vyombo vya mawasiliano kama *radio call* ili taarifa ziweze kuwafikia wahusika haraka.

(iii) Kutoa mafunzo na zana za kisasa za uchunguzi wa maiti na hivyo zoezi la kuchunguza maiti liweze kufanyika kwa haraka na kwa muda mfupi na kwa ufanisi mkubwa.

(iv) Kusogeza huduma za polisi na hospitali karibu na wananchi ili huduma hii iweze kutolewa mapema na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa makini kero hii ya Wananchi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi hiyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mauaji yanapotokea vijijini Polisi huarifiwa rasmi na huwajibika kwenda kuchukua maiti hawa/marehemu hao kuwapeleka Hospitali za Wilaya au za Mikoa kwa ajili ya uchunguzi. Lakini baada ya uchunguzi, Polisi hao hawarudishi wale

marehemu au maiti hao kwenye Vijiji walikozichukua na hivyo kusababisha wafiwa kulazimika kuwasafirisha.

Je, Serikali haioni ni busara kwa kuitaka polisi kurudisha maiti hao huko walikochukua kwa kuzingatia uwezo mdogo wa wananchi na kuwapunguzia familia ya marehemu makali ya msiba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida na mara nyingi matukio kama haya yakitokea kwanza sheria inataka Polisi wafike katika eneo hilo na Daktari, ili Daktari aweze akachunguza kubaini chanzo kilichosababisha kifo hicho ili kuwawezesha polisi sasa kuchukua hatua za kisheria na mara nyingi huwa Daktari na Polisi wanakwenda pamoja katika Kijiji kinachohusika upimaji ufanyiwa pale pale na baada ya kumaliza upimaji basi wananchi wafiwa wale huruhusiwa kuzika maiti. Huo ndio utaratibu wa kawaida, sasa inapotokea mara chache sana kwamba uchunguzi huo Daktari hawezi kuufanyia Kijijini anataka maiti ibebwe ipelekwe hospitali.

Sasa hapo ndio suala Mheshimiwa Mbunge linapokuja kwamba baada ya uchunguzi kusema kweli ni jukumu letu sote sio Polisi peke yao ni jukumu vile vile la Madaktari na Polisi na wananchi kwa ujumla kurudisha maiti na suala la kurudisha maiti kwa kweli ni utamaduni uliojengeka hapa nchini na mara nyingi tunajitahidi. Polisi, Hospitali na wananchi kurudisha maiti ili akazikwe kwa heshima Kijiji kwake na utaratibu huo utaendelea hivyo hivyo.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Kibakwe kuna kituo cha polisi na kuna Kituo cha Afya chenye Daktari, je, isingekuwa busara sasa uchunguzi wa maiti ukafanyika kule kule Kibakwe badala ya kupata Polisi na Daktari kutoka Mpwapwa ambao ni usumbufu kwa ajili ya mwendo mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba sheria inataka tukio likitokea Daktari aweze akachunguza halafu baadaye ndio hatua za Polisi zinafuata. Sasa Kibakwe tutatazama kama Mganga aliyeko pale ngazi yake ya udaktari inaruhusu kuchunguza maiti, maana inawezekana pale labda yuko *Clinical Officer* tu au yuko Mganga wa ngazi ya chini na kumbe sheria inamtaka *Medical Officer.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutatazama pale Kibakwe Mganga yule ana ngazi gani? Kama ngazi hiyo inaruhusu kisheria kwa kweli hamna sababu yeyote ya kumchukua Daktari kutoka Mpwapwa.

Hivyo hivyo kwenye kituo cha Polisi si kila Polisi atachunguza maiti, sheria inataja ngazi fulani ya cheo fulani cha uwajibikaji cha Polisi, sasa Mkuu wa Kituo cha Polisi pale Mpwapwa tazama kama cheo chake kinaruhusiwa kisheria kuchunguza basi kusema kweli hakuna sababu yoyote kwa nini huduma zitoke Mpwapwa kama utaalam pale Kibakwe unatosheleza.

Na. 23

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi - Ngorongoro**

**MHE. MATHEW OLE-TIMAN (k.n.y. MHE. PARSEKO V. KONE)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Ngorongoro wamejenga vituo vya Polisi vya Arash, Piyaya na Wasson; na kwa kuwa wameshindwa kukamilisha ujenzi huo kutokana na uwezo mdogo na wingi wa miradi ya maendeleo ya kuchangia:-

(a) Je, Serikali iko tayari kusaidia nguvu za wananchi hao ili waweze kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo?

(b) Baada ya ujenzi huo kukamilika, je, Serikali itapeleka askari polisi kwenye vituo hivyo na kuwapa vitendea kazi kama gari na zan nyingine za ulinzi ili kuimarisha ulinzi kwenye maeneo husika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Ngorongoro kwa hatua waliyofikia katika ujenzi wa vituo vya polisi Arash, Piyaya na Wasson kwa njia ya kujitolea. Huu ni mfano mzuri ambao ungefaa uigwe na wananchi wa sehemu mbalimbali hapa nchini.

Mheshiwa Spika, pamoja na ukweli kuwa Serikali ina utaratibu wa kuchangia ujenzi wa vituo vya Polisi pale ambapo wananchi huonyesha moyo wa kujitolea kama ilivyo kwa wananchi wa Jimbo la Ngorongoro lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti na miradi ya ujenzi wa vituo vya Polisi kuwa vingi nchini kote, wakati mwingine Serikali hushindwa kuchangia haraka ujenzi wa kila kituo. Hivyo Serikali itachangia ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya Arash, Piyaya na Wasson iwapo Bajeti ya mwakani itaruhusu. Kwa sasa namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwahamasisha wananchi wa

Jimbo lake waendelee na ujenzi wa vituo hivyo na Serikali itapeleka askari na vitendea kazi muhimu kwa kadri hali itakavyoruhusu.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile huwa tunasikia kwenye vyombo vya habari, vita kati ya Wamasai na Wasonjo na yanatoka katika maeneo haya ya Wasson, Arash, Piyaya, Serikali haioni ni wakati muhimu sasa kujenga vituo hivyo na kupeleka askari kuliko kungoja Bajeti ya mwaka ujao? Hili suala ni la dharura.

Pili kwa sababu suala hili linahusu vituo vya Polisi vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi, je, Serikali inaweza pia kusaidia kumalizia vituo vya Komolo, Orkesmet katika Wilaya ya Simanjiro?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Parseko Kone, Mbunge wa Simanjiro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba miaka ya hivi karibuni katika Wilaya ya Ngorongoro kumetokea mapigano ya Wamasai na Wasonjo jambo ambalo Serikali ya Mkoa wa Arusha inalisimamia kwa karibu ili kumaliza huo mgogoro na kwa kuzingatia hivyo katika vile vituo vitatu ambavyo wananchi wamejitolea kujenga tayari tumeshasogeza huduma ya Polisi kituo Wasson tayari tumeshapeleka pale Polisi ili wasaidie ile huduma ya Polisi iwe karibu zaidi na hilo eneo. Lakini dawa kubwa si kupeleka Polisi tu lakini ni pamoja na kuwapatanisha zile koo za Wasonjo na Wamasai.

Huduma ya Polisi katika eneo hilo tunashughulikia hivyo, vituo vya Payaya na Arash tunaomba tu waharakishe kujenga nyumba, vimeshakamilika kwa kiwango kikubwa lakini hakuna nyumba wala hakuna nyumba ya kupanga. Maana yake hata ingekuwa ya kupanga tusema basi wapange utakuta nyumba ya kupanga hamna. Kwa hiyo, tunaomba waharakishe ili na sisi tuharakishe kupeleka askari kule.

Kuhusu vituo alivyovitaja vya Simanjiro sasa Mheshimiwa Parseko Kone, yeye anajua mwaka jana tulishirikiana tukajenga kituo kikubwa kabisa cha kisasa kuliko vituo vyote hapa nchini kule kwake na hivi navyo tunamuahidi tutashirikiana, nguvu za wananchi na sisi Wizara katika kukamilisha hivyo vituo alivyovitaja.

Na. 24

**Uwezo wa Watanzania Kujua Kusoma na Kuandika**

**MHE. RHODA L. KAHATANO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati wa uhai wake alikazania sana maendeleo ya Watanzania kwa kusisitiza kwamba watu wote wapewe

uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu na maendeleo ya wananchi kielimu yalionekana kwa sababu kiwango cha watu waliojua kusoma na kuandika kilipanda kwa kiasi cha asilimia 70, na kwa kuwa, siku za hivi karibuni tumesikia kutoka kwenye vyombo vya habari kwamba kuna watu wasiojua kusoma na kuandika huko Songea kiasi cha asilimia 54 na sehemu mbalimbali namba ya wasiojua kusoma na kuandika inaongezeka:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha utaratibu wa kufundisha watu wazima kusoma, kuandika na kuhesabu kwa maendeleo yao na ya nchi nzima?

(b) Je, MEMKWA imefika wapi katika kuwasaidia wananchi kuinua kiwango cha elimu na kwamba ingawa MMEM inafanya kazi nzuri, kwa nini EWW isiandae pamoja na MMEM?

(c) Je, Serikali inaliambia nini Taifa kuhusu kuacha kabisa Elimu ya Watu Wazima?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Rhoda Kahatano, Mbunge wa Viti Maalum, napenda nitoe utangulizi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, baada ya kuikomboa nchi hii kutoka ukoloni aliweka mkazo mkubwa katika kuwapa wananchi uwezo wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Alifanya hivyo kwa njia mbili:-

(i) Kwa kuwapa fursa watoto wote kupata elimu ya msingi kwa kuanzisha Shule ya Msingi katika kila kijiji nchi nzima.

(ii) Kuanzisha mpango kabambe wa Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, uandikishaji wa watoto katika shule za msingi ulifikia kilele cha asilimia 98 ya rika lengwa mwaka 1980 na kujua kusoma na kuandika kilele cha asilimia 90 mwaka 1986. Baada ya hapo kutokana na matatizo ya kiuchumi, mafanikio hayo yakaanza kuporomoka hadi kufikia viwango vya chini vya uandikishaji shuleni asilimia 73.5 mwaka 1990 na kujua kusoma na kuandika asilimia 71 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Rhoda Kahatano, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imeandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu *(Education Sector Development Programme - ESDP)* inayohusu ngazi zote za elimu yaani elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu ya Juu pamoja na Elimu ya Watu Wazima. Hatua ya kwanza kabisa ya utekelezaji wa

programu hiyo ikaamuliwa iwe ya elimu ya msingi kwa watoto wote kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi mwaka 2002 hadi 2006 ambao umefanikiwa kuongeza uandikishaji wa watoto wa rika la elimu ya msingi (miaka 7 hadi 13) kutoka asilimia 55.4 mwaka 1995 hadi 90.1 mwaka 2004 na watoto wote kutoka asilimia 73.5 hadi 106.3 mwaka 2004.

Hatua hii inalenga kuziba kabisa bomba linaloongeza wasiojua kusoma na kuandika ifikapo mwaka 2006. Hatua ya pili ni ya kuwashughulikia watoto wa miaka 11hadi 14 na vijana wa miaka 15 ahdi 18 walioikosa Elimu ya Msingi kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa yaani MEMKWA na Watu Wazima wa miaka 19 na zaidi kupitia Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii kwa kifupi MUKEJA.

Wakati MUKEJA unatoa fursa kwa wananchi kupata ujuzi na uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu na pia kuwaongezea ujuzi na uwezo wa kuendesha kwa ufanisi shughuli zao mbalimbali za kiuchumi, MEMKWA unatoa fursa kwa watoto na vijana walioikosa kuipata elimu ya msingi waipata kwa mfumo usio rasmi ndani ya muda mfupi wa miaka minne.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika sehemu (a) ya jibu, MEMKWA na MUKEJA zinatekelezwa kupitia Bajeti ya MMEM. Mwaka huu 2004/2005 zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 3.4 kutekeleza mipango hiyo. Hii ni mara ya kwanza kutengwa kiasi kikubwa kama hiki kwa ajili ya Elimu ya Watu Wazima ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 55 ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijawahi kuacha kabisa kutekeleza Mipango ya Elimu ya Watu Wazima, bali kulikuwepo na kulegalega kutokana na matatizo ya kibajeti ambayo sasa tumeondokana nayo. Kupitia MEMKWA na MUKEJA siyo tu kutaharakisha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu bali pia kutasaidia kwa kiwango kikubwa juhudi ya kuondoa umaskini kwa kufuta ujinga na kuibua katika jamii mtindo sahihi wa kuendelea kujielimisha maisha yote *(life long education).*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nafurahi sana kwa majibu mazuri ya Waziri katika utaratibu huu wa mpango wa MEMKWA, liko tatizo kubwa sana la walimu, watoto hawa wanaonekana kama yatima kwenye shule hizi. Serikali inatamka nini kwa ajili ya kuhakikisha kwamba walimu wanapatikana kwa ajili ya MEMKWA?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Henry Shekiffu, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mwaka wa kwanza na wa pili wa MMEM lilikuwepo tatizo la walimu kwa sababu utaratibu wa kuwalipa vizuri ulikuwa haujakamilika lakini nina hakika kwa Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye amepitapita katika eneo lake mwaka huu hali hiyo imeanza kubadilika kwa sababu pesa zimekwisha pelekwa huko Wilayani za kuwalipa walimu na tunashauri pale ambapo walimu

hawajaajiriwa wasikose kuwaangalia walimu wetu waliostaafu wanaoishi katika maeneo hayo waajiri waweze kupata malipo na wasaidie kufundisha. *(Makofi)*

Na. 25

**Wanawake Kuoa Wavulana Wadogo**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa waraka uliotolewa na Afisa Elimu Kiongozi kuhusu kosa la kuoa mwanafunzi unaelekea kuwaelemea wanaume kama waoaji na kwa kuwa kitendo cha kuoa kwa sheria za Tanzania ni mwanaume kuoa mwanamke lakini kwa sheria za Kimataifa hata mwanamke anaoa na ndoa yake inatambulika kisheria:-

(a) Je, msimamo wa sheria za nchi hii ni upi iwapo mwanamke wa Kitanzania atapatikana na kosa la kuoa mvulana mdogo wa shule?

(b) Je, tangu waraka huo uanze kutumika, ni wanawake wangapi wametiwa hatiani kwa kosa hilo na kama wapo wamehukumiwa kwa sheria ipi?

(c) Iwapo mwanamke asiye Mtanzania ataoa mvulana mdogo wa shule wa Kitanzania, je, ni sheria gani itatumika kumhukumu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hatua za (i) Kanuni iliyotungwa na Waziri wa Elimu iitwayo *The Education (imposition of Penelties to Persons who marry or Impregnate a School girl) Rules 2003* na (ii) Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2004 ulitokewa na Afisa Elimu Kiongozi, zimezingatia kama alivyosema kwa maneno yake mwenyewe Mheshimiwa Mbunge katika swali lake kuwa na ninamnukuu: “Kitendo cha kuoa kwa sheria za Tanzania ni mwanaume kuoa mwanamke,” mwisho wa kumnukuu.

Kanuni zinazotungwa na Waziri na Nyaraka za Elimu zinatolewa na Afisa Elimu Kiongozi huzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na Sheria nyingine za nchi yetu. Aidha, Wizaya yangu haina taarifa ya sheria yoyote ya Kimataifa inayotambua ndoa ya mwanamke kumuoa mwanaume. Hilo ni jambo tofauati na ndoa ya watu wa jinsia moja ambazo kuna nchi chache zinazozitambua ndoa za aina hiyo na Tanzania siyo miongoni mwa nchi hizo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, tangu Waraka wa Afisa Elimu Kiongozi uanze kutumika tarehe 13 Aprili, 2004, hakuna mwanamke ambaye ameshitakiwa kwa kosa hilo kwa sababu hapa Tanzania tabia hiyo haipo na kosa hilo halipo.

Aidha, Wizara yangu haina taarifa ya tukio lolote kuhusu mwanafunzi mvulana kuolewa na mwanamke.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali halisi katika jamii haijaonyesha haja ya kutunga sheria ya kumlinda mvulana mdogo wa shule kuolewa na mwanamke, haijatungwa kanuni ya kukataza jambo hilo na kutoa adhabu kwa mkosaji, lakini endapo mtoto wa shule mvulana atakuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke yeyote awe Mtanzania au asiye Mtanzania, mwanafunzi huyo atafukuzwa shule kwa kosa la kukiuka maadili mema ya jamii kama vile itakavyokuwa kwa msichana atakayekuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanaume yeyote hata kama hayajawepo matokeo ya mimba. *(Kicheko)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, kadri ulimwengu unavyozidi kuendelea na maendeleo ya teknolojia mbalimbali yanavyoongezeka ina bainika wazi sasa hata watoto wadogo wa kiume wameanza kuwa katika hatari kubwa ya kuhatarishiwa maisha yao kwa wanawake kuwafuata kama vile wanaume wanavyowafuata watoto wa kike.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sasa kuna haja ya Wizara pia kuchukua tahadhari ya kuwa na kanuni na sheria ndogo itakayosaidia kuwalinda watoto hao ambao wengi kwa hali ya kawaida wameonekana sasa wanaanza kuathiriwa sana na tabia mbalimbali za wanawake pia kuwaharibu na kuwababaisha watoto hao wadogo wa kiume? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu Mheshimwa Jenista Mhagama, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu la msingi tunatunga kanuni hizi na sheria hizi kwa kuangalia tabia iliyo katika jamii, kama Mheshimwa Jenista Mhagama, anaona kuna tabia ya aina anayoizungumzia namwomba tuendelee kutaarifiana.

Lakini nisingependa tuanze kuchukua hatua ya kuvuka daraja kabla ya hatujafika darajani, kama kutakuwa na tatizo wakati muafaka tutaweza kutunga kanuni ya kuweza kutoa ulinzi unaohitajika.

Na. 26

**Ugonjwa wa *Hysteria* Shuleni na Vyuoni**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, upo ugonjwa wa kucheka ovyo, kulia, kukimbia, kuanguka na kuzimia ambao huwashika wasichana shuleni na vyuoni unaojulikana kama *hysteria* na

mwaka huu mwanzoni ulijitokeza katika shule za msingi za Kabugoso na Mgusu, Wilayani Geita:-

(a) Je, ugonjwa huo unasababishwa na nini na jina lake halisi kwa Kiswahili ni lipi?

(b) Je, ni matukio mangapi ya ugonjwa huo yameshatokea tangu mwaka 2001 hadi sasa?

(c) Je, tiba ya ugonjwa huo ni nini?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ugonjwa wa *Mass Hysteria* ambo hauna jina la kiswahili ni tatizo ambalo mara nyingi hutokea kwenye makundi ya vijana wanaoishi pamoja, kwa mfano katika mabweni ya shule au kambi. Matukio mengi huwatokea vijana wa kike au watoto wa kike. Hata kama shule ni ya mchanganyiko wa wavulana na wasichana, utakuta idadi ya wasichana wanaoathirika ni asilimia 70 hadi 90. Dalili za *Mass Hysteria* kwa kawaida hutokea ghafla kwa mtu mmoja, kisha huenea haraka kwa wengine na waathirika hurudia hali ya kawaida baada ya muda mfupi wa saa moja hadi siku kadhaa.

Mheshimiwa Spika, waathirika kwa kawaida huwa ni vijana ambao wamezoeana au ni marafiki. Mara nyingi kuna tukio la kitu ambacho kinahusishwa na dalili za *Mass Hysteria* kujitokeza katika kundi husika, mfano harufu fulani, tishio la kuhatarisha maisha, sumu au taarifa za kuwepo kwa ugonjwa wa hatari.

Dalili zinazojitokeza mara nyingi ni kuzimia ghafla, kupoteza fahamu na kutikisika kama mtu aliyeugua degedege au kifafa, kichefuchefu na kutapika ovyo, maumivu ya kichwa, kuchekacheka bila sababu au kupumua kwa nguvu na kasi kubwa. Dalili hizo huweza kujitokeza kwa vipindi ama kuendelea kwa muda mrefu bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, chanzo huhusishwa na hofu itokanayo na imani kwamba kuna ugonjwa fulani wa hatari, uchawi na hewa chafu, sumu na kadhalika. Akishaanza kijana mmoja kubadilika wengine hufuata haraka, aidha, kutokana na kuona mwenzao akibadilika ama kusikia fununu za tukio la hayo mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina takwimu za uhakika ni matukio mangapi ya ugonjwa yaliyojitokeza kwani mara nyingi huwa hayatolewi taarifa na jumuiya husika.

Mheshimiwa Spika, tiba ya ugonjwa huu ni pamoja na kumpumzisha mgonjwa na kumliwaza, kumpa *glucose* au sukari. Aidha, mgonjwa anaweza akapewa dawa za kumtuliza.

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia hali hii isitokee, inashauriwa kuwa ni vema uongozi wa shule hasa za bweni uwe na mawasiliano ya mara kwa mawa na wanafunzi ili kujua mahitaji na matatizo yao.

Na. 27

**Athari za Uvutaji Sigara**

**MHE. AISHA P. MAGINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, uvutaji sigara husababisha ugonjwa wa mapafu, shinikizo la damu, tatizo la kunuka mdomo, tatizo katika njia ya hewa na kadhalika na kuwa kila siku mtu mmoja hufa kila baada ya sekunde 6½ duniani:-

(a) Je, Serikali inakubaliana nami kwamba uvutaji sigara huua zaidi ya ugonjwa wa UKIMWI?

(b) Je, ni jitihada zipi zinachukuliwa na Serikali katika kupambana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aisha Magina, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa uvutaji sigara husababisha magonjwa ya mapafu, shinikizo la damu, kunuka midomo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uvutaji sigara huua watu wengi zaidi duniani kuliko UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo kulingana na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* zinaeleza kuwa uvutaji wa sigara huua takribani watu milioni kumi kila mwaka duniani kote wakati wastani wa watu wanaokufa kutokana na UKIMWI duniani ni zaidi kidogo ya milioni tatu kwa mwaka.

Hata hivyo nchi yetu haina takwimu za uhakika kuhusu suala hili, lakini kwa kuwa kuna ukweli kwamba UKIMWI na matumizi ya tumbaku vinaathiri zaidi nchi maskini ikiwemo Tanzania, hatuna budi kuamini kuwa uwiano huo upo pia hapa nchini kwetu.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia takwimu hizo hapo juu, Tanzania kwa kupitia Bunge lako Tukufu ilitunga Sheria ya Udhibiti wa Matumizi ya Tumbaku na Mazao yake mwaka 2003. Chini ya Sheria hiyo Waziri wa Afya ameunda Kamati ya

kuishauri Serikali kuhusu udhibiti wa matumizi ya tumbaku na bidhaa zake. Kamati hiyo imeundwa na Wajumbe toka sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu imeendelea kuwaelimisha watumiaji tumbaku na wanachi kwa ujumla juu ya madhara yake na kuwalazimisha watengenezaji wa sigara kutoa onyo kuwa sigara huathiri afya zao.

**MHE. AISHA P. MAGINA:** Mheshiwa Spika, ahsante, nina swali moja la nyongeza, je, kuna dawa yoyote mtu anaweza akatumia ili aweze kuachana na uvutaji wa sigara? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aisha Magina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tabia ya kuvuta sigara ni ya utashi wa mtu, kwa hiyo, kwa utashi wake vilevile anapaswa kuacha sigara bila kutumia dawa yoyote.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa sigara tunajua kabisa ni kitu cha hatari na ukienda miji kama Dar es Salaam, Musoma unakuta kuna mabango yanayo-*encourage* watu kuvuta sigara, ni lini Serikali itapiga marufuku mabango hayo?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimwa Dr. James Wanyancha, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli yale mabango wala hayakufanyi uvute sigara, kama wewe hutaki kuvuta sigara pawe na bango pasiwepo na bango hutavuta sigara. *(Makofi)*

Lakini katika kila juu ya *packet* ya sigara inayotengenezwa hapa nchini kuna onyo linakwambia unavuta, hatari, sasa usivute. *(Kicheko)*

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza ya swali nyongeza.

Kwa kuwa wavutaji wa sigara wanapovuta wanaathiri zaidi wale ambao wanakuwa karibu nao tofauti na mtu anayetumia kipodozi kinamuathiri mwenyewe yule mtumiaji na vilevile akinamama wanaathirika zaidi kwa sababu hawawezi kuwaambia baba hebu toka kavutie nje ya nyumba, kwa nini Serikali haisimamii vizuri kama ambavyo imeweza kusimamia sheria ya vipodozi na kupiga marufuku uingizaji, badala yake wanaruhusu watengenezaji wa sigara kuweka onyo tu ambalo halitekelezwi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sheria imepiga marufuku uvutaji sigara katika maeneo ya hadhara na sheria ile inataka kama ni hotelini ama hata kwenye *stadium* kuwepo na maeneo maalum ya wavutaji na maeneo ya wasio vuta, ni kweli kwamba wewe usiyevuta kama mwenzio anavuta karibu yako wewe pia unaathirika unayevuta moshi wa sigara ya mtu mwingine.

Kwa hiyo, sheria ile inaweka sheria kwamba mahali pa wazi, mahali pa watu wengi pawe na maeneo ya kuvuta na maeneo ambayo si ya kuvutia sigara. Sasa ni wajibu wa kila mmoja akiona mahali pana sigara aseme kwa nini unavuta hapa na hoteli zote zimeelekezwa kuwa na sehemu maalum yaani mahali pasipokuwa pa kuvutia sigara na mahali pa sigara.

Lakini kama mtu na mumewe ndani ya nyumba, mimi nadhani mume mpaka anaoa mke amempenda kuliko wanawake wengine wote, sasa kama umempenda utamlinda. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ukimpenda Mmakonde unampenda na ndonya yake. Maswali kwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa,
Mheshimiwa Gwassa Sebabili. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 28

**Kinga ya Kisheria kwa *UNHCR***

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imekuwa ikipokea wakimbizi kutoka kote ulimwenguni hata kabla ya Uhuru kutokana na siasa yake safi na kujali haki za msingi za binadamu za kuishi na kupata hifadhi na katika kutekeleza *charter* mbalimbali za Kimataifa kuhusu masuala ya amani na kwa kuwa watendaji wa Shirika la Kimataifa linalohudumia Wakimbizi wanatumia vibaya kinga ya kisheria waliyonayo kwa kuvunja sheria za nchi hii, mfano mwaka 1998 mtumishi wa *UNHCR* aliposababisha kifo cha Afisa Mtendaji wa Kata Marehemu Mussa B. Mkasa na kufukuzwa kwa walinzi 32 wa Shirika hilo *summarily* bila kuwalipa madai yao na kwa kuwa inasemekana kwamba kinga hiyo ya kisheria kwa *UNHCR* inatambulika Tanzania pekee:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hujuma wanazofanyiwa raia wake kukataliwa haki zao za kimsingi na kisheria?

(b) Je, toka mwaka 1998 Ndugu Mkasa alipouawa, Serikali imechukua hatua gani kumsaidia mjane wa Marehemu hasa katika kutoa huduma za masomo kwa watoto?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuiondolea kinga ya kisheria *UNHCR* ili walinzi 32 waliofukuzwa kinyume cha sheria waipeleke mahakamani?

**SPIKA:** Litajibiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi *(UNHCR)* ni mojawapo ya asasi mbalimbali za Kimataifa zenye kinga katika nchi zote duniani ikiwemo Tanzania. Kinga hii hutolewa na nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa duniani kwa Mashirika yote yalio chini ya Umoja wa Mataifa huo, kulingana na Mkataba wa Kimataifa unaohusu Hadhi na Kinga za Kidiplomasia wa mwaka 1961yaani *Vienna Convention on Diplomatic Relations, 1961* ambao Tanzania imeuridhia.

Kwa mujibu wa mkataba huu, afisa mwenye kinga hii ya Kibalozi anapotokea kuvunja sheria ya nchi, ataweza kushtakiwa tu pale Shirika lake au mwajiri wake atakapokubali kumwondolea kinga hiyo. Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa haina budi kuheshimu kinga hiyo kwa wafanyakazi wote wenye hadhi ya kupata kinga hiyo kama ilivyoainishwa katika sheria ya nchi yetu inayozungumzia hadhi na kinga za kidiplomasia ya mwaka 1986 inayoitwa *Diplomatic and Consular Immunities and Privileges Act, 1986.*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Gwassa Sebabili, kuwa Serikali kwa upande wake imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kinga hizi hazitumiwi vibaya na mara nyingi hata hao wahusika wenyewe wamekuwa wakitimiza wajibu wao ipasavyo isipokuwa katika matukio machache sana. Pale itokeapo mtu kufanya kosa ambalo linalazimu afikishwe mbele ya vyombo vya sheria na akawa anayo kinga hii, basi pande zote husika hukaa chini kwa madhumuni ya kukubaliana jinsi ya kushughulikia suala hilo ikiwa ni pamoja na ombi la kumwondolea mhusika kinga hiyo ya kisheria, ili ashitakiwe. Makubaliano yanaposhindikana basi mhusika anaweza kufukuzwa nchini na kurudishwa kwao ambako anaweza kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za nchini kwake.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia suala hili mambo muhimu tuliyogundua ni kama ifuatavyo:-

Kwanza mfanyakazi wa *UNHCR* anayetuhumiwa kuhusika katika ajali iliyosababisha kifo cha Marehemu Musa Badru Mkasa, ambaye kwa sasa ni mstaafu hakuwa na kinga ya kidiplomasia kumzuia asifikishwe kwenye vyombo vya sheria wakati wa tukio.

Pili, upelelezi wa kesi hii umeshakamilika na mtuhumiwa anatafutwa na polisi ili afikishwe mahakamani hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba juhudi za kumpata mtuhumiwa zitakapokamilika sheria itafuata mkondo wake na haki za familia ya Marehemu zitajulikana.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa kesi ya Marehemu Mkasa, baada ya kufuatilia kutoka ofisi ya *UNHCR,* tuliarifiwa kuwa wale walinzi 32 walikuwa wameajiriwa kama vibarua hivyo, malipo yao yalikuwa ni yale ya masharti ya vibarua. Baada ya *UNHCR* kubadili mfumo wa ulinzi kutokana na utaratibu uliowekwa na Umoja wa Mataifa, *UNHCR* waliamua kutangaza *tender* ya kazi ya ulinzi kwa makampuni ya ulinzi.

Baada ya Kampuni ya *West Security Guards* kushinda *tender* waliamua kutowaajiri wale walinzi 32 wa zamani na badala yake waliwalipa mshahara wa mwezi mmoja kwa kila mmoja wao kama kiinua mgongo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni msaada gani Serikali imetoa kwa mjane tangu mumewe afariki mwaka 1998, hasa katika kutoa huduma ya elimu kwa watoto wa Marehemu, ningependa kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu la kujikimu pamoja na jukumu la kupeleka watoto wa Marehemu shuleni na kuwahudumia si jukumu la Serikali, bali ni jukumu la familia ya Marehemu mwenyewe.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Katika jibu la msingi ni kwamba utaratibu wa kinga ya Kibalozi ni wa Kimataifa na ni wa muda mrefu sana, je, kwa sababu ya mabadiliko yaliyoko katika dunia ya sasa ya utandawazi Mheshimiwa Waziri anakubali kwamba umefika wakati wa kurekebisha utaratibu au sheria hiyo hasa kwa nchi zinazoendelea kwa sababu inaonekana kwamba kuna matumizi mabaya ya sheria hiyo katika nchi kama ya Tanzania?

La pili, ni kweli kwamba jukumu la kupeleka watoto shuleni katika matukio ya aina hii ni haki au ni wajibu wa familia, lakini kwa kuwa Serikali imesema itawasaidia watoto wote wasiokua na uwezo kuweza kujiendeleza kielimu, Serikali inasemaje kuhusu watoto wa Marehemu huyu ambao hawana msaada wowote kwa wakati huu na Shirika hili limewalalia?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Gwassa Sebabili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mkataba wa *Vienna Convention* kuhusu kinga na hadhi za Kidiplomasia ni wa siku nyingi lakini nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania siyo Kisiwa ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, kama tunataka haya yabadilike lazima tufanye kwa majadiliano na kwa ridhaa ya Jumuiya ya Kimataifa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nisisitize kwamba kama tulivyojibu katika jibu la msingi ni kwamba Serikali haina ushahidi wa moja kwa moja kwamba kinga hii inatumika vibaya, nimesema yako matukio machache sana katika nchi yetu ambapo yametokea hivyo lakini siyo ya kutufanya tuseme kwamba utaratibu huo haufai.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili la hawa watoto wa Marehemu, bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hakusema kwanza wanasoma katika ngazi ipi. Kwa sababu kama wapo katika *Primary School,* Elimu ni bure.

Mheshimiwa Spika, lakini kama wako *Secondary School,* naamini kabisa wakifuata utaratibu ambao Serikali imeeleza ikaonekana kabisa kwamba familia hii haina uwezo, naamini kabisa familia hii inaweza ikasaidiwa ili watoto wa Marehemu waendelee kusoma.

Na. 29

**Mgogoro wa Mpaka - Chukwani na Kikosi cha JWTZ Na. 161 Chukwani**

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna mgogoro wa ardhi wa tangu mwaka 1998 kati ya eneo la wananchi wa Shehia ya Chukwani, Wilaya ya Magharibi na eneo la kikosi cha JWTZ Na. 161 Chukwani:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo?

(b) Kama inalifahamu, je, imechukua hatua gani kulitatua?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu wakati wa kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 2004/2005, maeneo mengi ya Jeshi yenye migogoro yanatokana na kuvamiwa na wananchi kwa kudhani hayatumiki. Napenda kuwasisitizia tena wananchi kuwa si vyema na ni jambo la hatari kuvamia, kufanya shughuli na kuishi karibu au ndani ya maeneo ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kutambua tatizo hili, tangu mwaka 2003/2004 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeanza kuchukua hatua za kuyapima maeneo yote ya Jeshi ili kuwa na mipaka inayoeleweka na kupata hatimiliki. Hadi sasa maeneo ya kambi 28 za Jeshi yamepimwa na karibu katika maeneo hayo yote wananchi wameachiwa maeneo ambayo tayari wanafanyia shughuli zao za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inalifahamu tatizo la mpaka wa ardhi baina ya wananchi wa Shehia ya Chukwani na Kikosi cha Jeshi 161 Chukwani.

(b) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imechukua hatua za kumaliza tatizo hilo kwa kuwashirikisha wananchi wa eneo hilo, uongozi wa Jeshi, Kikosi cha Chukwani na Serikali ya Mapinduzi, kupitia Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, Mheshimiwa Dr. Mwinyihaji Makame, ambaye ni Waziri katika Ofisi ya Rais anayeshughulikia Fedha na Uchumi, ili kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, makubaliano yaliyofikiwa ni kuweka mpaka mpya. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kutambua umuhimu wa shughuli za kila siku za wananchi imewaachia wananchi baadhi ya maeneo ili wafanyie shughuli za maendeleo na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kutafuta fedha za kuyapima maeneo mengine ambayo hayajapimwa ya vikosi vingine vikiwemo vile vya Unguja na Pemba.

Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wamesaidia kutatua migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Wanajeshi kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa na Wilaya akiwemo Mheshimiwa Remidius Kissassi.

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi ni Jeshi letu wote, liko kwa ajili ya kuwalinda wananchi na mali zao na pia kutoa msaada wa hali na mali kwa wananchi wakati wa maafa. Jeshi linahitaji msaada wa wananchi na wananchi wanahitaji msaada wa Wanajeshi wao. Ni wajibu wetu wote kuepusha migogoro isiyo ya lazima kwa kuacha kuyavamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za Jeshi.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Remidius Kissassi ameridhika na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea na shughuli nyingine.

Matangazo ya vikao, lakini kabla ya matangazo niseme kwamba Spika amekuwa na utaratibu wa kutambulisha wageni wa Kimataifa tu wanaokuja kuhudhuria Shughuli

za Bunge, kwa maelezo kwamba Watanzania ni haki yao, lakini nimeshauriwa kwamba Wabunge wana haki ya kuleta wageni wao ndani ya Bunge.

Sasa isingekuwa vizuri Spika akawatambulisha wageni wa Mbunge fulani kwamba wapo katika Bunge. Basi naona ni ushauri mzuri kwa sababu ni wageni wa Mbunge. Sasa leo napenda kuwatambulisha wageni wa Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Frederick Sumaye, ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Hanang waliokaa katika *gallery* kulia kwangu na sasa watasimama.

*(Hapa Wageni waliotambulishwa walisimama na kuonekana kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**SPIKA:** Tunawakaribisha Waheshimiwa Madiwani. Sasa matangazo ya vikao.

Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. John Malecela, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wahudhurie kikao cha Kamati hiyo kuanzia saa tano katika ukumbi namba 227 ghorofa ya pili. Ziko Kamati tano zimepangiwa kukutana leo.

Ya pili, ni Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Mambo ya Nchi za Nje wakutane leo saa tisa na nusu alasiri kwa lengo la kukutana na Wabunge wa Bunge la Mpito la Burundi, niliowatambulisha jana. Kwa hiyo, Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje inakutana nao leo.

Ya tatu, ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa George Lubeleje anaomba Wajumbe wakutane kwenye ukumbi namba 133 ghorofa ya kwanza leo saa saba mara baada ya kikao cha Bunge kuahirishwa kwa kipindi cha asubuhi. *Agenda* ni kujadili Muswada wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa. Muswada utakaowasilishwa Bungeni baadaye katika Kikao hiki.

Ya nne, ni Kamati ya Fedha na Uchumi, nadhani walianza jana wanaendelea leo saa tano asubuhi chumba namba 428.

Mwisho ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba Wajumbe wake wakutane saa saba mchana katika ukumbi namba 227 ghorofa ya pili ili wapitie taarifa na maoni ya Kamati kuhusu Muswada utakaowasilishwa Bungeni unaowahusu. Mwisho wa matangazo. Sasa tunaendelea na *Order Paper,* Katibu, endelea.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mwaka 2004
***(The National Economic Empowerment Bill, 2004)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta hoja hii ingawa kwa kweli imechelewa. Baada ya kuwa na sera za ujamaa na kujitegemea, ni vema kukawa na elimu ya kutosha kuhusu maudhui halisi ya *empowerment.* Dhana nzima iendane na ile ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, wakati uliokuwa muafaka wa kuanzisha sera hii, ilikuwa wakati tunaanza kubinafsisha au kuuza mashirika ya umma. Hivi sasa kwa mashirika yaliyobaki ni machache na makubwa sana kiasi kwamba hakuna Mtanzania anayeweza kuyanunua au hata kuyakodi. Bila shaka Watanzania watakuwa wabia tu na hisa zao zikiwa ni weusi au Utanzania wao tu! Hawatakuwa na usemi juu ya viwanda hivyo. Zaidi ni Watanzania wachache tu wenye nafasi Serikalini ndiyo watakuwa wabia. Hili lipo hadi sasa kwani mawakala wa makampuni makubwa Serikalini! Hivi kijana wa miaka 30 amejenga umaarufu kiasi gani na ana uwezo gani kifedha au kitaaluma hata awe *representative* wa kampuni za nje? Muswada usilete njia ya kuhalalisha viongozi Serikalini kupitia kwa watoto wao kujinufaisha!

Kabla ya kupitisha sheria hii ni vema kuangalia vikwazo *(bottlenecks)* zilizoko katika mfumo wa sheria za nchi ili iweze kufanya kazi vizuri. Hii peke yake haitakidhi haja inayokusudiwa.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa *The National Economic Empowerment Act* ni Muswada muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Ni Muswada unaokusudiwa kuwawezesha Watanzania wanyonge waingie katika shughuli za uchumi wa nchi yao kama wachezaji wakuu badala ya kuwa watazamaji.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Tanzania hivi sasa umeshikwa na wageni, Watanzania wazalendo wamekuwa *site lined,* lakini Muswada huu unaona aibu kusema hivyo. Hakuna hata kipengele kimoja kinachowataja Watanzania wazalendo au Watanzania weusi kama ndio walengwa wa Muswada huu na jinsi gani Muswada unakusudia kuwawezesha ili wajikomboe na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu hautoi *mechanism* ya kuwawezesha wazalendo kushika uchumi wao. Muswada huu haumsaidii Mtanzania mweusi maskini na unaona aibu kusema hivyo. *Needs complete rewriting.*

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, ushirika ulikuwa chombo muhimu cha kuwezesha wazalishaji hususan wakulima wa mazao ya kiuchumi. Pamoja na jitihada za kufufua ushirika, je, ni kwa vipi wana ushirika kwa ujumla watawezeshwa kupitia Muswada huu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wasemaji wamemalizika nilivyoarifiwa na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa mtoa hoja Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maelezo ya majumuisho naomba kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naitambua kwa heshima kabisa Kamati iliyohusika na uchambuzi, lakini namtambua zaidi Makamu wa Mwenyekiti Mheshimiwa George Lubeleje, ambaye ndiye alisoma kwa niaba ya Kamati. Pili, naitambua Kambi ya Upinzani, namtambua sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, ambaye alisoma maelezo ya Kambi ya Upinzani.*(Makofi)*

Tatu, namtambua Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Benedicto Mutungurehi, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Leonard Derefa na wa mwisho kwa waliochangia kwa kusema ni Mheshimiwa William Shellukindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa John Mwakipesile na Mheshimiwa Talala Bana Mbise. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijajielekeza moja kwa moja kujibu hoja moja moja, naomba tu nianze kwa masuala ya jumla.

Kwanza, nataka niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba sheria hii iliyoletwa kwetu sisi ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000 ya Chama cha Mapinduzi. Bahati nzuri ametukumbusha Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, jana Kiongozi wa Upinzani iko kwenye mwelekeo, lakini ukifungua Ilani yenyewe ukurasa 7 tumeelekezwa sisi kufanya jambo hili. Leo tunaleta sheria ili kuweka msisitizo na katika kutekeleza sera ya uwezeshaji na kuhalalisha kisheria.

Mheshimiwa Spika, labda niwakumbushe kwamba jambo lenyewe hili la uwezeshaji Serikali ya CCM imekuwa inatekeleza mambo haya wakati wote siyo kwamba sheria hii inakuja ili kuanza kutekeleza masuala ya uwezeshaji, tumefanya mengi sana kwa nia hii hii ya uwezeshaji.

Nataka nitoe kwa mfano, eneo la ubinafsishaji peke yake kati ya Mashirika 308 yaliyobinafsishwa hadi kufikia mwezi Juni, 2004 Mashirika 153 yamebinafsishwa kwa Watanzania pekee kwa upendeleo maalum wote wanatoka Mikoani kwa mfano zile

*RETCOs* ukiwauliza wale wafanyakazi walionunua zile kampuni za usafirishaji masharti tuliyowapa ni ya upendeleo kabisa kwa sababu ni wananchi wa Watanzania Mikoa yote kwa Dar es Salaam ukiuliza ile *KIUTA* tumewapa kwa shilingi milioni 400 tena kwa mishahara yao tu bila hata ya kutoa senti tano.

Kwa hiyo, kuna mambo ambayo tumefanya tukijua kwamba tunawawezesha wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia yapo Mashirika 127 katika hayo 308 ambayo yamebinafsishwa kwa ubia, kuna Watanzani ambao wametafuta *partners* wa nje tumewapa, lakini kiungo kikiwa ni Watanzania ambao ndiyo walengwa. Mashirika katika hayo 308 yaliyobinafsishwa kwa wageni peke yake ni 28 tu.

La pili, kwa mfano Kituo chetu cha *TIC* mpaka sasa kimeandikisha miradi 2,626 hadi mwezi Machi yenye thamani za dola za Kimarekani bilioni 8, kati ya hiyo miradi inayomilikiwa na Watanzania asilimia 100 ni 1,161 kwa masharti ambayo mnayajua kwamba kiwango cha uwekezaji mtaji wa Mtanzania ni theluthi ya kiwango cha mtaji cha uwekezaji kwa mtu wa nje. Kwa hiyo, kuna nafuu hapo, kama Mtanzania peke yake anataka kuwekeza kiwango kinachotambulika na *TIC* cha mtaji ni theluthi moja ya kiwango cha mwekezaji kutoka nje. Sasa hawa Watanzania peke yao ambao wamepewa upendeleo namna hii ni 1,161. Waliowekeza kwa ubia ni 834 na wa nje peke yao ni 631.

Tatu, kuhusu elimu, watu wamezungumza ukweli. Nakumbuka wengi wamesema hapa kwamba uwekezaji wa mwanzo kabisa uanzie kwenye elimu. Sasa nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba tumeshawekeza sana uwezeshaji katika elimu. Kwa mfano, Bunge hili limeridhia utaratibu na Mheshimiwa Rais, mnakumbuka ametangaza tufuta ada zote za shule za msingi, huo ni uwezeshaji. Lakini mwaka 2004 tumepunguza ada za shule za sekondari za Serikali kwa asilimia 50 na mambo mengi sana katika elimu ambayo tumeyafanya kwenye vyuo vya ufundi na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwenye biashara mwaka huu tumeshuhudia Serikali ikiondoa ada za leseni kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuondoa kero na kodi mbalimbali nyingine za kero tumeziondoa huu ni uwezeshaji wa aina yake. Kwenye kilimo na mifugo tumeondoa kodi ya zana za kilimo na pembejeo za mifugo. Mfuko wa Pembejeo tunatoa ruzuku kwa mbolea kwa mwaka wa pili mfululizo. Lakini kwenye ardhi baada ya kujua kwamba watu wanashindwa kujiendeleza katika kujenga makazi ya kudumu kwa sababu gharama ya upimaji wa viwanja na hivi, Serikali imeamua yenyewe kuwekeza ili kuwawezesha wananchi kupata viwanja vilivyopimwa, Dar es Salaam tumepima tayari viwanja zaidi ya 30,000. *(Makofi)*

Halafu tumeanzisha utaratibu wa kuanza kutambua nyumba fulani fulani zile *squatter* za Manzese kwa kutoa Hati Maalum tofauti na utaratibu wa kawaida, leseni badala ya Hati. Leseni hizi zitakuwa zinawawezesha kutambulika kama zilivyo Hati katika vyombo fulani fulani vya fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utoaji wa hatimiliki za kimila vijijini katika maeneo ambayo wananchi wanayamiliki kimila. Lakini pia mnajua Serikali imeanza maandalizi ya Mradi Maalum ambao unasimamia zoezi hilo la utambuzi na kuthaminisha mali mbalimbali za wananchi ili ziweze kuwa na thamani katika vyombo vya fedha. Mnajua jitihada za Mheshimiwa Rais ambazo amezifanya na mgeni maalum ambaye amemleta Bwana Disotto kwa ajili ya kusimamia na kuisaidia Tanzania katika miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la ujenzi tumewezesha sana sasa hivi ujenzi wa barabara nyingi umekamilika katika maeneo ya Vijijini na Mijini kwa kutumia fedha zetu. Hivi vinawezesha wawekezaji Watanzania ambao wako kwenye sekta ya usafirishaji ili kuweza kufanyabiashara zao vizuri, lakini kwa wazalishaji wengine wa bidhaa kuweza kupita kwenye barabara hizo bila vikwazo vyovyote.

Kwa hiyo, nilitaka nianze hapo kwamba sheria hii kwa kweli tunarasmisha tu mambo haya ambayo Serikali ya CCM imekuwa inafanya kisheria ili na sisi Waheshimiwa Wabunge tuwe sehemu ya mafanikio haya. Tunaweza tukasema kwamba haya yote tuliyoyafanya sasa tumeyafanya kwa mujibu wa sheria ambayo tumeitunga hapa Bungeni, lakini mambo haya tumekuwa tukiyafanya kwa kuelekezwa na Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2000.

Jambo lingine la jumla ambalo nilitaka niliseme ni kwamba kwa mujibu wa sheria hii na mifano yote niliyoisema hapa, uwezeshaji tunaozungumza kwa mujibu wa sheria ni fursa zaidi siyo pesa, si suala la pesa wala mikopo mingi wala si kugawa pesa kwa watu ni fursa. Hawa wote tuliowapa ubinafsishaji, uwekezaji na nini ni fursa zaidi kwamba Watanzania wanazo fursa zenye masharti mepesi zaidi kuliko wageni. Kwa hiyo, uwezeshaji huu umekuwa ukifanywa bila uratibu wala misingi ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Baraza linaloundwa ndilo litakalotoa mwongozo, kusimamia, kuelekeza na kuratibu. Uwezeshaji wenyewe utafanywa na Taasisi, Idara na Wizara mbalimbali kupitia Sera za Kisekta na sheria ambazo nyingi ya hizo itabidi Baraza lipendekeze kwa Serikali na hatimaye Serikali ipendekeze kwa Bunge hili ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza habari ya sheria kwa vyovyote vile sheria ni nyingi sana, ili sheria hii iweze kutekeleza majukumu yake vizuri lazima sheria nyingi sana zitaguswa ili ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, maelezo mengine ya jumla nilitaka kusema kwamba kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyopendekeza Baraza litaweka utaratibu kwa mujibu wa sheria hii kuwawezesha Watanzania katika maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, ametueleza hapa na ametoa maoni yake na utaratibu wa namna ya kuwawezesha wananchi wa Tanzania ili tujenga matajiri wa kweli kweli wa Kitanzania na watu ambao watakuwa na uwezo wa kiuchumi wa kiwango cha juu na kati.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge kwamba katika mengi ya mikakati ambayo tulikuwa tunaigusa hapa ni bahati mbaya hizi

sera tulizigawa siku nyingi sana Waheshimiwa Wabunge wamesisahau na bahati mbaya vilevile kwenye *library* yetu tulikuwa hatujaweka tunaomba radhi kwa hilo lakini sasa tumeziweka. Lakini ukisoma kwenye sera hiyo ambayo tuliizindua hapa mwezi Juni, 2004 utaona kwamba mikakati mingi ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaielekeza Baraza lianzie iko imefafanuliwa vizuri sana katika sera hiyo.

Kwa hiyo, Baraza kwa kweli litapata kazi nyepesi sana ya kuanzia kwa sababu maelekezo yote ya namna ya kuanza, hoja zote zimeainishwa kwenye sera na namna ya kutatua sera na namna ya kutekeleza sera yenyewe imeelekeza hapa namna gani Baraza lifanye kama ni marekebisho ya sheria na sera fulani fulani za Serikali.

Kwa mfano, nitasoma eneo moja, tumezungumzia habari ya uchumi na ujengaji wa mazingira ya uwekezaji. Sera imeelekeza mikakati ifuatavyo. Ili kukuza uchumi madhubuti na kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji mikakati ifuatavyo itatekelezwa:-

Moja ya mikakati hiyo ni kuzielekeza sera za kisekta katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi. Sisi tunaamini kila Wizara hapa kupitia sera zake ina uwezo wa kurekebisha sera ikawa na fursa za kuwawezesha wananchi, kila sekta hapa ukienda kwenye Mawasiliano, ukienda kwenye Utalii, ukienda kwenye Kilimo, ukienda kwenye Mifugo kila mahali mpaka fedha kwa kupitia sera za Fedha namna wananchi wanavyoweza kuingia na kukopa mikopo kwa urahisi kwenye vyombo vya fedha. Hizo zinaweza zikarekebishwa kupitia sera za fedha, lakini baadaye kupitia sheria mbalimbali.

Kwa mfano, Mfumo wa Utawala wa Kodi kwenye mikakati katika kuboresha Mfumo wa Utawala wa Kodi utaboreshwa kwa kuchukua hatua za utekelezaji zifuatazo:-

Moja ya hatua hiyo utaratibu wa kuwapa wawekezaji wakubwa unafuu wa kodi utapanuliwa kuwahusisha pia wananchi ili nao wapate unafuu huo kama wawekezaji wa ndani. Lakini pia kuhusu sheria baadhi ya sheria na kanuni na taratibu zilizopo haziendani na dhana ya uchumi wa uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, tamko la sera hii ni kurekebisha sheria, kanuni na taratibu zilizopitwa na wakati ili ziendana na sera ya uwezeshaji. Mikakati itakayotumika kurekebisha sheria ya kanuni na taratibu ili ziandane na sera na uwezeshaji ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kutunga sheria ambayo tumeshafanya, lakini pili, kurekebisha sheria mbalimbali zinazosimamia sera za Serikali.

Mheshimiwa Spika, upande wa leseni tamko la sera juu ya leseni nasema leseni za biashara zitatumika kama njia ya kuratibu shughuli za uchumi na siyo tu kama chanzo cha mapato ya Serikali. Ndiyo maana tumeanza kuchukua hatua ya kufuta ada ya kifedha kwa leseni hizo ili kutekeleza hoja hii ya sera.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine iko mikakati ya kuinua hadhi ya wananchi ili wakopesheke. Wananchi wengi hawakopesheki kwa sababu hawana uzoefu na ujuzi wa

kutosha kutayarisha miradi na kuiendesha hadi iweze kupata faida na kujenga uwezo wa kulipa madeni. Sera hii inataka Baraza liwawezeshe wananchi na kusaidia kuboresha huduma za usanifu wa miradi zinatolewa na Taasisi zake na makampuni ya wananchi ya wataalam waelekezi. Aidha, sera hii inataka Baraza lichangie gharama ambazo wananchi watatakiwa kulipa ili waandikiwe miradi ambayo inaweza kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, viwango vya ujuzi tumezungumzia habari ya ujuzi na elimu, tamko la sera hii kuhusu eneo hilo inasema: "Serikali iangalie upya mfumo wa elimu kwa nia ya kuongeza kina cha mtazamo wa kisayansi ili kukabili mila na desturi potofu zinazodumaza maendeleo na kumjenga mwananchi anayejiamini, mbunifu na mwenye ari ya kuzalisha na kufanya biashara ama shughuli nyingine kwa makini na ustadi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine mfumo wetu wa elimu utatakiwa kuwajengea wananchi misingi ya ujasirimali, mfumo wa mafunzo utahakikisha kwamba ujuzi unaongezeka wakati wote kulingana na mahitaji ya ushindani katika masoko."

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema haya machache ili kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba maeneo mengi ambayo walikuwa wanayachangia jana kwa kweli sera imeshayaainisha na ndiyo maana sasa tunatengeneza sheria ili Baraza liangalie namna ya kutekeleza hoja mbalimbali zilizopo katika sera kwa kupitia mapendekezo ya mikakati ambayo tayari yameishaainishwa katika sera hiyo. Haya ni maelezo machache sana ambayo ni miongoni mwa mikakati na hoja ambazo zilishatayarishwa na Kamati ya Mawaziri na wataalam.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya jumla Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya kulinganisha uwezeshaji wa hapa na Afrika Kusini. Wengi walisema tusione haya kwa sababu wenzetu wa *South Africa* wamesema moja kwa moja kwamba ni *Black Empowerment,* sisi tunazunguka uwezeshaji Watanzania mbona ni jumla mno?

Sasa nilitaka kusema tu kwamba ukweli hata mazingira ya Uhuru ya Afrika Kusini unawawezesha kuwa na ubaguzi wa namna hiyo, kwa sababu hata mazingira yao ya mapambano yalikuwa ya ubaguzi hivyo hivyo kati ya watu weusi na watu weupe. Kwa hiyo, historia yao inawawezesha kuanza na ubaguzi wa namna hiyo katika sera zao. Sisi Uhuru wetu tumeshirikiana Watanzania wote au wakati ule wa Tanganyika wote tumeshirikiana katika kudai uhuru wa nchi hii, tumeshikamana tangu wakati wa uhuru mpaka leo. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na sera ambayo ni ya kiubaguzi namna hiyo.

Sasa tafsiri ya Mtanzania sisi kwetu iko katika sheria kwamba Mtanzania huyu tunayemlenga ni nani, anaweza kuwa Mhindi, anaweza kuwa Mwarabu, anaweza kuwa mtu mweusi mtu yeyote yule lakini ilimradi ni Mtanzania. Wenzetu wanasema ni *Black Empowerment,* lakini hata wenyewe kwa sheria ambayo ninayo na sheria yao nao utakuta ni ndogo sana. Sheria kama ilivyokuja kwetu na wao wenzetu walianza kwa hatua hiyo hiyo. Maana yake hapa tumesema sheria ni finyu haifafanui. Sheria haiwezi kuwa na ufafanuzi wote. Baada ya sheria hata wenzetu baada ya hapo ndiyo wamekwenda kutayarisha mikakati ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeamua kutayarisha sheria ili kukipa hadhi chombo hiki kisheria ili kiweze kutayarisha mikakati. Sheria ya Afrika Kusini ukiangalia hapa ina kurasa tatu, lakini *definition* ya *Black People* katika sheria yao inasema: *"is a generity term which means Africans, colourant and Indians,"* kwenye sheria yao. Kwa hiyo, tunaweza tukafikiri kwamba *black* kwa maana ya rangi, lakini tafsiri yao kwa mujibu wa sheria yao ni yale yale ya Mtanzania. Hata ukiangalia kwenye utekelezaji wa sera zao hata kwa picha tu hao wanaowezeshwa unakuta hapa kama kuna Mzungu, unakuta kuna Mhindi, kwa hiyo, unaweza ukakuta ni *terminology* inayouza sura hiyo, lakini katika utekelezaji hawajabaguana na kwa sheria hii ambayo ninayo. Nafikiri hata Waheshimiwa Wabunge mkienda kwenye Internet mnaweza kupata *information* zote hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kusema tu kwamba hii amesema sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na wengine na Mheshimiwa Henry Shekiffu, amezungumza. Nataka kusema historia tunatofautiana kidogo. Sisi twende hivi lakini lengo letu linafanana tunaotaka kuwawezesha tunajua ni akina nani, ni Watanzania, lakini ndani ya Watanzania tunajuana wenyewe kwamba ni nani *the most disadvantage group* ndani ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba nijielekeze kidogo kwenye hoja kama ifuatavyo:-

Kwanza nianze na Kamati iliyochambua Muswada huu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe hawa tangu tukiwa Dar es Salaam mpaka hapa wameunga mkono na hoja zao tulizijibu. Moja, ilikuwa ni kuhusu suala la sheria hii kwa nini isitumike kote, lakini pia waliuliza juu ya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji kwa nini usifanywe na Baraza? Tukawajibu wakaridhika kwamba tunapendekeza kwa mujibu wa sheria Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza aendelee kuteuliwa na Rais na sababu tuliwaeleza. Lakini ipo hoja nyingine ya Kiongozi wa Upinzani hiyo moja ya ulinganisho na sheria ya Afrika Kusini nimelisema. Lakini Kiongozi wa Upinzani alitoa hoja kwamba Muswada huu unaelea hewani hautasaidia Watanzania walio wengi. Alitumia maneno mengi ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ufupi nataka nimjibu kwamba mimi binafsi sikubaliani na hilo na hasa baada ya kutoa maelezo na historia ya utekelezaji wa sheria na Serikali imefanya kazi kubwa sana kabla ya kuwasilisha Muswada huu Bungeni. Nitaeleza baadaye historia ya namna tulikoanzia kuandaa Muswada huu. Ninaamini kwamba matokeo ya utekelezaji wa Sheria hii yatanufaisha Watanzania walio wengi. Ipo hoja nyingine imetolewa hapa kwamba sheria hii kwa nini isiwe kwenye Ofisi ya Kuondoa Umaskini au kwa nini iwe katika Ofisi ya Waziri Mkuu, hoja hii imeulizwa na Kamati, lakini pia Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa George Lubeleje kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maelezo yangu ni kwamba suala la uwezeshaji kama nilivyowaeleza mwanzo hapa hakuna sekta hata moja ambayo inaweza kukosa fursa za uwezeshaji wa Watanzania. Kwa hiyo, suala la uwezeshaji ni mtambuka ni *cross cutting issue.*

Kwa hiyo, sisi tunafikiri kwamba bado Mheshimiwa Waziri Mkuu angeweze kuratibu hili vizuri zaidi. Kwa sababu kwa vyovyote vile utekelezaji wa sera hii na sheria hii utatekelezwa na sera mbalimbali. Baraza hili ambalo litakuwa chini ya Waziri Mkuu limeundiwa sheria yake litakuwa mahali fulani linajitegemea chini ya mwavuli tu wa Waziri Mkuu. Lakini kwa vyovyote vile utekelezaji utagusa sekta mbalimbali na Wizara mbalimbali za Serikali kulingana na sera zao ambazo zitaelekezwa ziendane sambamba na sheria hii na sheria mbalimbali ambazo zitafanyiwa marekebisho ili ziweze kufanana na madhumuni ya kuanzishwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba sheria hii pia itumike Zanzibar nilieleza kwenye Kamati. Lakini nafikiri maelezo yangu ni yale yale kwamba msingi wa sheria hii ni Sera ya Taifa ya Uwezeshaji ya Wananchi kiuchumi iliyopitishwa na Baraza la Mawaziri mwaka huu mwezi Februari, na inahusu kwa kweli Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na umuhimu wa suala hili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutashauriana na wenzetu ili tuone kama wanaweza na wenyewe wakatunga sheria yao kwa upande wa pili. Lakini katika kutekeleza sheria hii haitakuwa na ubaguzi kwa Watanzania wanaoishi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni Mzanzibar anaishi Tanzania Bara au Mtanzania wa Bara haitakuwa na ubaguzi, itawawezesha Watanzania wanaoishi katika eneo la Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unalenga kuwawezesha wenye nacho na kuwawezesha zaidi wakati ambapo wadogo watanyang'anywa na kile kidogo walichonacho. Haya ni maoni ya Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Kamati na Kiongozi wa Upinzani.

Kwa maelezo ya sera, sera inawagusa wananchi wote, kwa hiyo, hatuna mashaka kwamba sheria hii itawagusa wananchi wote wa vijijini na mijini.

Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, wamekuwa na mashaka kidogo na tafsiri ya mlengwa. Sera imetoa tafsiri ya mlengwa ambaye anastahili kuwezeshwa kwa mujibu wa tafsiri hiyo walengwa ni wananchi wa Tanzania ile tunapouliza hawa *disadvantages* ni akina nani, ni Watanzania kwa kundi hilo ndiyo tunaowalenga kwa maana ya sera hii. Serikali itazingatia maoni mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika utekelezaji bora wa sheria hii.

Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, wametaka ufafanuzi wa uwezeshaji. Tafsiri ya uwezeshaji imefafanuliwa vizuri sana katika sera na lengo lake ni kuwapa Watanzania fursa ya kushiriki kikamilifu zaidi katika uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja tena hapa ya uchangiaji kwenye mfuko huo wa uwezeshaji, uko ushauri umetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi Mheshimiwa

Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Isaac Cheyo. Kwa kiwango kikubwa mfuko huu utachangiwa na Bajeti ya Serikali ndiyo mapendekezo yaliyopo kwenye sheria. Lakini vile vile michango mingine itatoka kwa wahisani na michango ya hiari.

Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, alileta mapendekezo ya marekebisho haya. Nashukuru kwamba tulielewana kwamba marekebisho yale ataleta kama mchango wake na tutayapeleka kwenye Baraza, tutayafanyia kazi. Lakini tumekubali katika eneo lile la michango na eneo la vyanzo vya mapato ya mfuko kuongeza eneo la michango ya hiari yaani *donation* kwa ajili ya mifuko hiyo. Hii tumekubali tutaiweka kwenye sheria. Lakini maelezo mengine ya viwango tumekubaliana kwamba tutapeleka kwenye Baraza ili tuweze kufanya uchaguzi zaidi. Lakini neno lenyewe lile michango ya hiari tutaliweka kwenye marekebisho ya sheria hii.

Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, wamezungumzia sheria ya uwezeshaji *visa* na masuala ya kilimo kwamba kilimo ndiyo msingi tuwawezeshe wakulima. Sera na sheria ya uwezeshaji vinagusa sekta zote kama nilivyosema mwanzo. Kwa vyovyote vile kilimo ni mojawapo na kwa vyovyote vile kilimo ndiyo itakuwa msingi kwa sababu kilimo ndiyo msingi wa uchumi wetu. Lakini maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo tayari tunazo *Hansard* zake itakuwa ni miongoni mwa nyaraka ambazo Baraza wataanza nazo. Tumeamua tuwapelekee maoni kama yalivyo kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, ametoa ushauri wake juu ya kuimarisha sekta isiyo rasmi na pia mawazo yake ameyaeleza kama nilivyosema ya namna wafanyabiashara wakubwa kuchangia mfuko huu. Tumekubaliana na mawazo tutayachukua na isipokuwa lile neno lenyewe tutaliweka kwenye Muswada la uchangiaji wa hiari ambalo halikuwemo.

Lakini pia Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, wanasema sheria ya ununuzi nayo izingatie suala la uwezeshaji. Sasa mimi nafikiri hii sheria ya manunuzi imeshakuja na kwa mujibu wa Muswada huu tunaomba idhini Baraza lianzishwe ili Baraza hili likakae chini, liainishe aina ya sheria mbalimbali ambazo zitakuwa ni vikwazo katika kutekeleza zoezi hili la uwezeshaji.

Kwa hiyo, mimi nafikiri sheria hii imekuja kabla ya sheria hii kupitishwa na ziko sheria nyingi sana ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziendane na mahitaji ya sheria hii ya uwezeshaji. Kwa hiyo, mimi nafikiri tusiunganishe kati ya sheria iliyoletwa sasa na sheria mbalimbali. Sheria hii ya manunuzi tuione kama ni miongoni mwa sheria nyingi ambazo zitakuja ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Kwa hiyo, nilifikiri Waheshimiwa Wabunge wakubali sheria ya manunuzi ijitegemee, ije ipite kwenye taratibu zote na hatua zote kama ilivyoletwa na wala isihusishwe na Muswada huu kwa sababu Muswada huu kwa kweli utakapoanza kutekelezwa baada ya Rais kuidhinisha utagusa sera nyingi sana na sheria nyingi.

Hatuwezi kuanza kutekeleza kwa Muswada huu kwa sababu sheria yenyewe haijapita mpaka ikapate *endorsement* ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, yapo mawazo mengine ambayo yametolewa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, wanasema majukumu ya Baraza ni mapana sana, yawe *specific.* Lakini pia sheria itamke biashara ambazo zinafanywa na Watanzania wenyewe. Mojawapo ya kazi za Baraza ni kuainisha maeneo ambayo yatahusisha zaidi wananchi. Yupo Mheshimiwa mmoja hapa ametaja kwamba kuna mmoja aliwahi kujitokeza kusema aina fulani za biashara zisifanywe na watu fulani zifanywe na watu fulani, Serikali ikamkemea sana.

Lakini kuna mwingine tena amemjibu humu humu ndani, nafikiri mmoja amesema hapa Mzee Mzindakaya amesema kwamba hata hao watu wenyewe wanaotajwa wanauliza huko Serikalini si mmekaa wenyewe kwa nini muende kututangaza huko kwamba aina ya biashara sisi tusifanye anayetoa leseni si ninyi wenyewe Serikali tuko sisi. Kwa nini hamtubagui huko huko kimya kimya mpaka mfike kule na maelezo mkatangaze? Kama wewe unatoa leseni unaweka masharti kwamba leseni hii itolewe na picha. Picha ije, sasa ukiona hiyo picha huitaki si unakataa tu lazima ukatangaze kule mtu fulani wa rangi fulani simtaki.

Kwa hiyo, bahati nzuri Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, amemjibu hapo hapo kwamba hata huu uwezeshaji tunafikiri kwamba lazima tuwabague watu fulani hao tunao fikiri tunawabagua wanatuuliza. Serikali hii tunaongoza wenyewe kwa hiyo, lazima tupange mikakati wenyewe na tuna uwezo wa kupanga mikakati wenyewe ya kuamua nani tumwezeshe bila hata kufanya huo ubaguzi ambao wengine wanauzungumza.

Kwa hiyo, Baraza litaainisha hivyo katika sekta mbalimbali sekta za madini, sekta za uvuvi, sekta za biashara itaainisha kabisa kwamba eneo hili litafanywa na aina fulani ya wafanyabiashara. Kwa hiyo, sheria zitarekebishwa, Serikali itapelekewa mapendekezo hayo, ikiridhika italeta Miswada ya kurekebisha sheria ili utekelezaji wa mapendekezo hayo utekelezwe.

Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Raynald Mrope, wamependekeza mpango huu ugawanywe katika makundi mbalimbali ya walengwa na Mheshimiwa Leonard Shango, amependekeza tena zaidi kwamba mfuko ufanye utafiti zaidi kuhusu suala la dhamana kwa wananchi.

Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na Mheshimiwa Leonard Shango, wanapendekeza mtandao huu uwe mkubwa mpaka kwenye vijiji kwa sababu wana mashaka kwamba nani atakayewasaidia wananchi katika mikoa na Mheshimiwa Semindu Pawa, amezungumzia habari ya wawekezaji wageni wanaopendelewa mno. Kwa hiyo na Watanzania nao wasaidiwe.

Mheshimiwa Isaac Cheyo, amependekeza tuanze uwezeshaji wa sekta ya kilimo na elimu ambayo nimetolea maelezo na Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar,

tunashukuru sana ametupa masahihisho fulani fulani madogo madogo ambayo tumeyazingatia katika hii.

Katika hayo yote naomba niseme kwa ufupi kwamba tumepokea ushauri na yako mambo ambayo yatajionyesha moja kwa moja kwenye kanuni na kwa vyovyote vile Baraza litazingatia mambo haya na mtandao wa Serikali. Baraza limepewa uwezo kwa mujibu wa sheria hii kutumia taasisi yoyote ya binafsi au mtandao wa Serikali katika kufanya shughuli zake.

Kwa hiyo, hakutakuwa na uwazi katika ngazi mbalimbali kwa sababu Baraza litaainisha *agency* mbalimbali ambazo zitahusiana nazo katika kutekeleza mambo haya kuanzia ngazi za chini kabisa.

Mheshimiwa Aridi Uledi, amezungumzia habari ya mikopo ya wananchi vijijini iwe na masharti nafuu. Kwa vyovyote vile Baraza litaainisha.

Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, tuwe wawazi kuwataja Watanzania Waafrika. Nimeeleza kidogo tofauti yake na Afrika Kusini. Lakini pia Mheshimiwa Henry Shekiffu, amesema Muswada huu ungeletwa na marekebisho ya sheria nyingine. Nimesema kwa nini tumeleta huu peke yake bila marekebisho ya sheria nyingine. Lakini alikwenda zaidi kwamba huu ni ugali usio iva. Lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwamba hii ni pilau siyo ugali yaani ni chakula ya chini kabisa tunakula sisi Wahehe tu wenye nguvu. Lakini hii uione kama ni pilau imeiva hii kwa sababu Muswada huu umeshughulikiwa kwa muda mrefu sana na hatua zake ni nyingi labda niwakumbushe kidogo namna ulivyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, nilisema kwenye maelezo yangu kwamba mwaka 1999 Baraza la Mawaziri liliagiza. Lakini baada ya Ilani sasa ku-*endorse* kabisa mwaka 2000 na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Kamati tarehe 15 Desemba, 2000 ya Mawaziri. Kamati hiyo wakati huo iliongozwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, alikuwa Mheshimiwa Iddi Simba.

Kamati hii ilifanya kazi kubwa sana na ndiyo maana mnazungumza hata habari ya *public hearing*. Kamati hii ilifanya *public hearing* yenyewe, kila mkoa ilikwenda ikakutana na wafanyabiashara. Kwa mfano ninayo *minute* ambayo Mwenyekiti Mheshimiwa Iddi Simba, aliitisha wafanyabiashara, Arusha peke yake ina wafanyabiashara zaidi mia tatu na sabini walihudhuria katika mkutano wa kujadili na kupendekeza sera hii ya uwezeshaji. Kwa hiyo, Kamati hii ilikuwepo, imefanyakazi tangu mwaka 2000 sera hii tumeipata mwaka huu miaka yote hii ilikuwa inafanyiwa kazi.

Nikikusomea orodha ya wataalam ambayo ilikuwa na Manaibu Katibu Wakuu watatu mpaka na Mheshimiwa Rais akamteua na Mheshimiwa Sanare si mnajua huyu ameanzisha hata *TRA* na mafanikio yake, Naibu Katibu Mkuu uwezeshaji akapewa kazi hii yuko hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Henry Shekiffu, nataka uamini kwamba jambo hili lina historia ndefu na limetengenezwa na limepikwa vizuri kama pilau. Maana nataja pilau kwa sababu ina vitu vingi wanaweka magogo humo, nyama sijui na vitu gani. Kwa hiyo, hii imetengenezwa vizuri ukilinganisha na ugali ambao unawekwa unga tu. Kwa hiyo, nataka uridhike.

Mheshimiwa Spika, historia hii inatukumbusha kwamba jambo hili limetengenezwa vizuri. Kwa maana hiyo nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri waliohusika katika maandalizi ya awali ya Muswada huu na sera.

Namshukuru sana Mheshimiwa Iddi Simba, ambaye alikuwa Mwenyekiti katika awamu ya kwanza na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, aliteuliwa kuwa Mwenyekiti katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, waheshimiwa wafuatao walikuwa wajumbe wa Kamati hiyo ambao ni Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Balozi George Kahama, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Katibu Mkuu Kiongozi Mheshimiwa Marten Lumbanga. Pia Mzee wa Umaskini Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Elekeza maoni yako kwa Mheshimiwa Spika. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba jambo hili tumelishughulikia sana. Naomba radhi sana wakati tunawatambua hapa Waheshimiwa Wabunge waliochangia sikumtambua Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga. Naomba radhi basi bahati mbaya ametoka. Namtambua sana na ndiyo maana nimemtaja sana kwenye hoja zangu, bahati mbaya sijui nilitaja wamechapa vibaya samahani wametaja Danhi Makanga, kumbe alikuwa Dakta, tena wamesema Dr. Danhi Makanga kwa kweli wamechapa vibaya ilikuwa Dr. Makongoro Mahanga. Nimemtaja Makanga kama *doctor* ambaye kwa kweli wamechapa vibaya, naomba radhi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuwashukuru sana hao wote ambao wameshiriki lakini nawashukuru vile vile Kamati ya wataalam ambayo iliongozwa na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Kwayu wa Ofisi ya Waziri Mkuu halafu Naibu Katibu Mkuu wa Mipango na tulichukua wataalam wa kisekta zote muhimu kutoka benki kuu na Wizara mbalimbali zilihusika katika maandalizi ya hili.

Kwa hiyo, nataka turidhike kwamba kwa kweli kazi hii nataka kuwaonyesha kwamba hata suala la utayarishaji wa mikakati halitakuwa gumu kwa sababu hawa wataalam na Kamati hizi wameshamaliza. Nina *document* hapa zaidi ya kilo moja hapa ambazo tayari zimeshaainisha mikakati ya utekelezaji wa sera hii na sheria hii.

Kwa hiyo, Baraza likishaundwa tayari linazo *information* za kutosha ambazo Kamati ya Mawaziri walishapendekeza na Kamati ya utaalam wakashauri na wakafanya

uchambuzi wa kina. Tulishindwa kwamba hatuwezi kuunganisha ile mikakati kwenye sheria na wala hatuwezi kueleza yote kwenye sheria. Tulieleza machache sana kwenye sera na tunafikiri sasa Baraza litakuwa na kazi ya uchambuzi na kuyaainisha yale yote yaliyofanywa kwa hiyo, kazi kubwa iliishakamilishwa.

Baada ya maelezo hayo nataka niseme kidogo juu ya hoja moja ambayo alisema Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare juu ya Azimio la Arusha. Nataka nimweleze kwamba kwa kweli Azimio la Arusha kwa nchi hii bado linayo *record* ndiyo limetuletea usawa na umoja katika Taifa kama anavyosema yeye watu wengi walishiriki katika kuunga mkono katika kuunga mkono hata yeye alishiriki wakati huo tuliunga mkono na mafanikio yake ndiyo matunda tuliyonayo leo yanatokana na Azimio la Arusha.

Naomba kumwarifu pia MheshimiwaWilfred Lwakatare, kwamba hakuna mtu aliyewahi kufa wakati wa zoezi la *operation* vijiji wala utaifishaji mali. Maana amesema kuna watu walikufa wakati wa *operation* vijiji, hakuna aliyekufa na kwa sababu tu CCM kila mara hupanga siku zote kwa uhakika sera na mipango yake. Pamoja na Mheshimiwa Isaac Cheyo, anajua na Kambi nzima ya Upinzani inajua juu ya utekelezaji ulio mahiri sana wa mipango na sera mbalimbali za CCM za sasa na zilizopita. Kwa jambo hilo nafikiri Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, amelizua hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kama nilivyoahidi kwenye Kamati nitashirikisha Kamati ambayo inahusiana na Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuendelea kushauri juu ya maandalizi ya kanuni bora itokayokidhi matakwa ya Muswada na kiu ya Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Baraza litajitahidi kutumia ujuzi, uzoefu wa baadhi ya viongozi wakiwepo Waheshimiwa Wabunge katika maandalizi ya mpango wa utekelezaji na hata wa wakati wa utekelezaji wenyewe kwa sababu tutakuwa tunaleta hoja hizi kwenye Bajeti, mtatuhoji tu. Yapo mengi sana mmesema hapa kwa vyovyote yatakuwa *reflected* kwenye *speech* zetu za Bajeti mtapata nafasi ya kutuhoji lakini Baraza litakuwa Tanzania hapa litakuwa na wajumbe ambao mtakuwa mnawajua, mtaendelea kupata ushauri wa kila mara wa namna ya kushauri.

Mheshimiwa Raynald Mrope, mwisho alitoa ushauri kwamba tumsaidie, Baraza limsaidie katika kuwawezesha wale watengeneza Nipa kule kwake. Nipa kule Masasi ni gongo, wanaotengeneza gongo ya korosho tuwasaidie ili waweze kujitegemea kutumia gongo. Mimi nafikiri waendelee kufanya utafiti tu kama watafanya utafiti watafanikiwa kutengeneza pombe nzuri zaidi au konyagi ya Nipa Mungu atawasaidia tu. Lakini nafikiri wao ndiyo wafanye huo utafiti, Baraza haliwezi kujiingiza moja kwa moja kwenda kufanya utafiti wa pombe ambayo sasa imeshakuwa haramu.

Sera ya uwezeshaji tuliyoipitisha hapa na tuliyoizindua Bungeni, *Hansard* ambayo ina michango yote Waheshimiwa Wabunge na taarifa hizi mbalimbali ambazo zimetayarishwa na Kamati ile ya Mawaziri na wataalam zitakuwa ndiyo mwanzo mzuri wa utekelezaji wa mapendekezo yote na uundaji wa baraza na kanuni ambazo zitasimamia utekelezaji wa sheria hii. Naahidi kwa Waheshimiwa Wabunge kanuni zitakazotungwa zitakidhi haja ya sera na sheria hii na matokeo yake watayaona.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mbele yetu ambayo inahitaji kuamuliwa sasa ni kwamba Muswada unaoitwa *The National Economic Empowerment Bill, 2004* sasa usomwe mara ya pili.

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mwaka 2004 *(The National Economic Empowerment Bill 2004)*

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 10, Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa tu nahitaji ufafanuzi katika Kifungu hicho cha 10, Kifungu kidogo cha 6 katika ukurasa wa 12 Kifungu kidogo zaidi cha (b) pale anaposema: *"proceed to consider and decide the matter as if there was a quorum."* Hapo alikuwa anasema niliwahi kutoa maoni kwamba suala hili linaweza kuleta utata kwamba *quorum* haikutimia, *we assumed* kwamba ilikuwepo *quorum,* inaleta kidogo utatanishi nilitaka tupate ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ndiyo ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliliangalia sana jambo hili tukafikiri kwa vyovyote kwamba hii Kamati itakuwa ilipoitishwa ilikuwa tayari ina *quorum* kwa hiyo, kupungua kwa mjumbe mmoja ambaye ametoka nje kutokana na *interests* zake katika shughuli inayonayozungumzwa hakuwezi kusababisha athari.

**MWENYEKITI:** Maelezo unayaonaje Mheshimiwa William Shellukindo?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Nilikuwa nimetoa maoni kwamba kunaweza kusiwe na hoja kama amefanikiwa suala lake, lakini kama hakufanikiwa anayo haki ya kuomba rufaa hiyo tu ndiyo nilitaka niweke wazi kwamba inawezekana hivyo.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, saidia hapo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoongelewa hapa ni mgongano wa maslahi, yaweke mezani kwamba kwa suala hili ambalo liko mbele ya baraza mimi nina maslahi nalo. Ukishamaliza hiyo kwa sababu lazima uamuzi uchukuliwe wewe unaondoka. Sasa inaweza ikasababisha kwa sababu mlikuwa wa tano wewe ukatoka lakini mlipoanza *quorum* ilikuwa palepale ndiyo uhalali wa maamuzi ambayo yatafuata. Kwa hiyo, katika hatua hiyo hustahili hata kwa maamuzi haya yatachukuliwa ambayo wewe jambo hilo una maslahi nalo huwezi ukasema ulikatie rufaa.

**MWENYEKITI:** Maelezo yanaridhisha, baada ya maelezo hayo Kifungu cha 10 kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwanza kushukuru mchango ambao Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, alitoa wakati anachangia Muswada huu Bungeni na katika eneo hili alipendekeza na

Serikali inaona ni vizuri tukachukua pendekezo lake kwamba katika mstari wa pili kutoka chini katika 16 (1) baada ya neno *grants* weka, halafu tuingize maneno *contributions* (michango) ambayo watu wanaweza kutoa kwa hiari katika ku-*promote* sera hii ya uwezeshaji kiuchumi wananchi wa Tanzania.

Kwa hiyo, tunapendekeza tuingize neno hilo *contributions* kama alivyosema mtoa hoja wakati ana-*wind up.*

**MWENYEKITI:** Ni neno moja tu tunaliongeza. Hakuna haja ya *Hansard* ni neno moja tu tunaliongeza. Kama Kifungu cha 16 kilivyorekebishwa sasa hivi na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 18

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 18 kama kilivyo kinaafikiwa? Hapana ngoja kidogo, Mheshimiwa Aridi Uledi.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia jana kifungu cha 18 (c) kuna hilo neno la kwanza limeandikwa *proving.* Nilipendekeza kuwa tungeweka neno *providing* nadhani lingekuwa na maana zaidi sasa sijui Mheshimiwa Waziri anasemaje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, anakubaliana na hoja yako kwa hiyo kifungu hicho kinarekebishwa kwa kubadilisha neno *proving* liwe *providing.* Baada ya marekebisho hayo kinaafikiwa kifungu hicho?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

**MWENYEKITI:** Katibu eleza ili Kamati ijue mbona *print education* ina vifungu 41 na mpaka 44?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika orodha ya marekebisho ambayo tumegawa kwa Waheshimiwa Wabunge, Serikali imefanya ukurasa wa pili inaonyesha katika Kifungu cha 17 imefutwa hiyo. Sasa tunasema hiyo 18 iliyomo kwenye Muswada kama ulichapishwa sasa inakuwa 17 na yenyewe hiyo 17 tukaifanyia marekebisho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Kifungu cha 19 cha Muswada na chenyewe kimefutwa. Halafu Kifungu cha 20 kikaandikwa kiwe Kifungu cha 18 vikafutwa Vifungu vya 21 na 22 baada ya kufanya hayo yote sasa tunaziandika kwa kuzipatia namba upya 23 mpaka 44 sasa zifahamike kuwa ni 19 mpaka 40.

Jedwali la 1
Jedwali la 2

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mwaka 2004**
***(The National Economic Empowerment Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2004 *(The National Economic Empowerment Act, 2004)* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, Naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Mwaka 2004 Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**SPIKA:** Kabla ya sijamwita Mtoa hoja ningependa kufafanua kwamba Maazimio yatawasilishwa kwa pamoja ili yaweze kujadiliwa kwa pamoja na ndivyo tulivyopanga hivyo. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja wasilisha Maazimio yanayohusu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liliridhie Maazimio matano yanayohusu Usafiri wa Majini. Maazimio haya yanalenga kuimarisha usalama wa uchukuzi majini. Maazimio hayo ni kama yafuatayo:-

1. Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Uingiliaji Kati kwenye Bahari Kuu iwapo kunatokea ajali wa Mwaka 1969 na Itifaki ya Kuzuia Uchafuzi wa Mazingira unaotokana na Bidhaa nyingine zaidi ya Mafuta ya Mwaka 1973 *( The International Convention for Intervention on the High Seas 1969 and the Protocol for Marine Pollution By Substances 1973).*

2. Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa Mwaka 1972 *(The International Convention for Regulations for Preventing Collisions at Sea, 1972).*

3. Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utafutaji na Uokoaji Baharini wa Mwaka 1979 *( The International Convention on Maritime Search and Rescue 1979)*

4. Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kusaidiana Nyenzo za Utafutaji na Uokoaji *(East African Community Agreement Concerning Inter-State Use of Search and Rescue Facilities)*

5. Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Taratibu za Uendeshaji Vyombo vya Usafiri katika Mito na Maziwa ya Mwaka 2002 *(The East African Tripartite Agreement on Inland Waterways Transport, 2002).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Miundombinu ilijadili Maazimio haya na kupendekeza yaridhiwe na Bunge lako Tukufu. Nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, pamoja na wajumbe wote kwa michango yao mizuri iliyojaa hekima waliyoitoa wakati wakijadili Maazimio haya. Michango yao ililenga katika kuimarisha usalama wa usafiri majini ikiwa ni pamoja na uendeleza wa uchukuzi majini. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu Mikataba hii kama ifuatavyo:-

Mkataba wa Kimataifa wa Uingiliaji Kati kwenye Bahari Kuu ambapo utatokea ajali wa mwaka 1999 na Itifaki ya Uingiliaji Kati iwapo kutatokea Uchafuzi wa Mazingira unaotokana na Bidhaa nyingine zaidi ya Mafuta ya mwaka 1973 *(The International Convention Relating to Intervention on the High Seas 1969 and the Protocol for Marine Pollution By Substances 1973).*

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1969 unahusu Uingiliaji kati kwenye Bahari Kuu iwapo kunatokea ajali inayopelekea uchafuzi wa bahari kwa mafuta na Itifaki ya Uingiliaji Kati iwapo kutatokea uchafuzi wa mazingira unaotokana na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyomo kwenye Mkataba huu ni kwanza kutoa maelekezo kwa nchi wanachama kuhusu hatua muhimu za kuzuia na kuondoa hatari zinazoweza kutokea katika Pwani ya nchi zao na madhara yanayoweza kujitokeza.

Pili, Mkataba unaelekeza nchi mwanachama kuwapa msaada wahanga wa ajali na kuhakikisha kuwa mabaharia na meli husika inarudishwa nchini pasipo kizuizi chochote.

Mheshimiwa Spika, faida za Mkataba huu pamoja na nyinginezo ni kama ifuatazo:-

1. Kuweza kuepuka uchafuzi wa bahari na Pwani kwa kutumia vifaa maalum kwa kulinda mazingira na raslimali zetu.

2. Kuwa na uwezo mkubwa wa kushirikiana na nchi zingine katika kulinda mazingira ya bahari na Pwani yetu.

3. Kulipwa fidia kutokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvujaji wa mafuta na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya kukubali kuridhia Mkataba huo ni kubwa inapendekezwa kwamba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Uingiliaji Kati Kwenye Bahari Kuu iwapo kunatokea ajali ya mwaka 1969 pamoja na Itifaki ya Uingiliaji Kati Iwapo kutatokea Uchafuzi wa Mazingira unaotokana na bidhaa nyingine zaidi ya Mafuta ya mwaka 1973

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kusoma Azimio lenyewe.

KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa wa Mwaka 1969 unahusu Uingiliaji Kati kwenye Bahari Kuu iwapo kunatokea ajali:

NA KWA KUWA Mkataba una Itifaki wa Uingiliaji Kati iwapo kutatokea uchafuzi wa Mazingira unaotokana na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta:

NA KWA KUWA Mkataba unatoa maelekezo kuhusu hatua muhimu za kuzuia hatari katika Pwani ya nchi yetu na nchi nyingine husika kuhusu uchafuzi au tishio la uchafuzi wa mazingira, madhara yanayoweza kujitokeza na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa:

NA KWA KUWA faida ya kuridhia Mkataba huu ni pamoja na kuweza kuepuka uchafuzi wa bahari na Pwani yake kwa kutumia vifaa maalum kwa kulinda mazingira yake pamoja na raslimali zake, kuwa na uwezo mkubwa wa kushirikiana na nchi nyingine katika kulinda mazingira ya bahari na Pwani, kulipwa fidia kutokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvujaji wa mafuta na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta:

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu Bunge hili katika Mkutano wa 17 na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(a) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kwamba linaridhia Mikataba ya Kimataifa wa Uingiliaji Kati kwenye Bahari Kuu iwapo kunatokea ajali wa mwaka 1969 pamoja na Itifaki ya Uchafuzi wa Mazingira unaotokana na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta ya mwaka 1973.

Pili, Mkataba wa Kimataifa wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa Mwaka 1972 *(International Convention on the Regulations for Preventing Collisions at Sea, 1972).*

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1972 wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini ulitayarishwa kutokana na matukio mengi ya meli

kugongana na kusababisha madhara kwa watu na mali na kuharibu mazingira. Madhumuni ya Mkataba huu ni kuboresha usalama wa vyombo vinavyosafiri majini, abiria, wafanyakazi wa vyombo hivyo pamoja na kulinda uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu unatoa maelekezo kwa vyombo vya majini kuweka utaratibu wa vyombo vitakavyosaidia kuona na kusikia ili kuepuka matukio ya ajali mbalimbali. Unaelekeza kuwa meli zote ziendeshwe kwa mwendo wa usalama na kuweza kusimama pale inapostahili.

Mheshimiwa Spika, faida ambazo zitapatikana kwa kujiunga na Mkataba huu ni kama zifuatazo:-

1. Kutunza mazingira ya viumbe na bahari;

2. Kuweka mazingira mazuri kwa Wawekezaji watakaopenda kuwekeza raslimali zao nchini;

3. Kuwa na ushirikiano na nchi nyingine za Kimataifa;

4. Kuweza kuwadhibiti Manahodha wa meli wanaokwenda kinyume na taratibu za kuongoza meli.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya kukubali kuridhia Mkataba huo ni kubwa inapendekezwa kwamba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa mwaka 1972.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kusoma Azimio lenyewe. Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa Mwaka 1972.

KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1972 wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini ulitayarishwa na Shirika la Usafiri Majini yaani *(International Maritime Organisation (IMO)* baada ya kuona matukio mengi ya meli kugongana na kusababisha madhara kwa watu mali, viumbe wa baharini na uchafuzi wa mazingira:

NA KWA KUWA kuboresha usalama wa vyombo vinavyosafiri majini pamoja na kuwalinda watu, mali na mazingira Umoja wa Mataifa kupitia *(IMO)* ulitayarisha Mkataba huu:

NA KWA KUWA Kanuni za Mkataba huu zitatumiwa na vyombo vyote vilivyoko Bahari Kuu pamoja na njia zote za maji zinazotumiwa na vyombo vya majini zilizounganishwa na Bahari Kuu:

NA KWA KUWA faida ya kuridhia Mkataba huu ni pamoja na kutunza mazingira kwa ujumla na kupunguza uwezekano wa kutokea ajali, kuweka mazingira mazuri kwa Wawekezaji watakaopenda kuwekeza raslimali zao nchini na kuwa na ushirikiano na nchi nyingine ili kuwadhibiti manahodha wanaokwenda kinyume na taratibu za kuongoza meli:

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu Bunge hili katika Mkutano wa 17 na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kwamba linaridhia Mkataba wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa mwaka 1972 *(Ratification of the Convention on Intervention Regulations for Preventing Collisions at Sea 1972).*

Tatu, Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utafutaji na Uokoaji Baharini wa Mwaka 1979 *(International Convention on Maritime Search and Rescue 1979).*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa Sayansi na Teknolojia shughuli za bahari zinazidi kukua na hivyo kuonekana ipo haja ya kuwa na taratibu na mikakati ya kufuata ili kupunguza madhara yanayotokana na ajali bahari. Ili kukamilisha azma hiyo Umoja wa Mataifa kupitia Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini *(IMO)* uliandaa Mkataba wa Kimataifa wa Utafutaji na Uokoaji Baharini unaoelekeza taratibu za kufuatwa na Mabaharia na vyombo vya usafiri majini ili kupunguza madhara ya ajali. Tanzania ilijiunga na *(IMO)* mwaka 1974.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu unaelekeza yafuatayo nchi mwanachama kushirikiana na nchi nyingine kufanya matayarisho na utaratibu wa utoaji huduma ya utafutaji na uokoaji. Nchi mwanachama kutambua eneo la bahari ambalo limetengwa kuwa ni jukumu la Serikali husika kufuatilia matukio ya ajali na kutoa msaada inapotokea ajali.

Mheshimiwa Spika faida ambazo nchi yetu itapata ni kama zifuatazo:-

1. Kuweka mazingira mazuri kwa Wawekezaji watakaopenda kuwekeza raslimali zao nchini;

2. Kuwa na utaratibu unaoeleweka wa kutoa msaada kwa uokoaji inapotokea ajali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya kukubali kuridhia Mkataba huu ni kubwa, inapendekezwa kwa Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utafutaji na Uokoaji wa Mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kusoma Azimio lenyewe. Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utafutaji na Uokoaji Baharini wa mwaka 1979 *(The International Convention on Maritime Search and Rescue 1979)*

KWA KUWA shughuli za Baharini zinazidi kukua kutokana na kukua kwa Sayansi na Teknolojia na hivyo kuonekana ipo haja ya kuwa na taratibu na mikakati ya kufuata ili kupunguza madhara yanayotokana na ajali Baharini:

KWA KUWA Umoja wa Mataifa kupitia Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini *(IMO)* uliandaa Mkataba wa Kimataifa wa Utafutaji na Uokoaji Baharini unaoelekeza taratibu za kufuatwa na Mabaharia pamoja na vyombo vya usafiri majini ili kupunguza madhara ya ajali:

NA KWA KUWA Mkataba huu unataka nchi mwanachama mmoja mmoja au kwa ushirikiano na nchi nyingine ifanye Matayarisho na utaratibu wa utoaji wa huduma za utafutaji na uokoaji:

NA KWA KUWA faida za kuridhia Mkataba huu ni pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa Wawekezaji watakaopenda kuwekeza raslimali nchini hasa hasa katika vyombo vya usafiri Baharini kwa sababu watakuwa na uhakika kwa kuwa upo uwezekano wa kupata msaada wa uokoaji kisheria endapo itatokea ajali. Pili, kuwa na utaratibu unaoeleweka wa kutoa msaada wa uokoaji inapotokea ajali:

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu Bunge hili katika Mkutano wa 17 na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(a) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 linaazimia kwamba linaridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utafutaji na Uokoaji Baharini wa Mwaka 1979 *(The International Convention on Maritime Search and Rescue 1979.*

Nne, makubaliano ya Nchi za Afrika Mashariki kuhusu kusaidiana na kutumia nyenzo za utafutaji ya mwaka 2002 *(The East African Community Agreement Concerning Inter-State Use of Search and Rescue Facilities 2002)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania, Kenya na Uganda ni nchi za Afrika Mashariki ambazo zimesaini Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The Treaty of the Establishment of the East African Community).* Katika Mkataba huo kuna ibara zifuatazo 92, 93 na 94 zinazoelekeza umuhimu wa kuwa na mikakati ya kusaidiana inapotokea ajali. Ibara hizo ndiyo chimbuko la makubaliano ambayo nchi wanachama wa Jumuiya tunatakiwa kuridhia kabla ya makubaliano hayajaanza kutekelezwa. Aidha, msisitizo umewekwa na Mashirika ya Kimataifa yanayosimamia usalama wa usafiri wa ndege na meli yaani *The International Civil Aviation Organization (ICAO)* na *The International Maritime Organization (IMO).* Mashirika ambayo Tanzania ni mwanachama kuwa ni vyema nchi zinazopakana ziandae makubaliona ya kusaidiana inapotokea ajali. Kwa kutambua umuhimu huo wa kukabiliana na majanga ya ajali nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa pamoja zimeandaa makubaliano ya kuwezesha nyenzo za uokoaji kutoka nchi moja kuweza kutoa msaada kwa nchi zingine yenye janga au ajali. Makubaliano haya yana lengo la kurahisisha taratibu za kusafirisha nyenzo za uokoaji toka nchi moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi nchi nyingine. Tanzania kama mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ina jukumu la kuridhia na kutekeleza makubaliano yaliyosainiwa na wananchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki ya kupokea na kutoa msaada inapotokea ajali na pia kunufaika na misaada kutoka kwa majirani zetu tunapokuwa na ajali.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ni pamoja na yafuatayo:-

1. Kusaidiana kuratibu uokoaji mara taarifa ya kuhitaji msaada inapotolewa;
2. Kupelekwa nyenzo za uokoaji katika eneo la ajali la nchi mwanachama;

3. Kuandaa na kufanya mazoezi ya pamoja na kushirikiana katika kuandaa mikakati, mbinu, matumizi ya vifaa na nyenzo za uokoaji; na

4. Kusambaza haraka taarifa za ajali pale inapobidi kuomba msaada ili nyenzo za wananchi nyingine ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, makubaliano haya yatarahisisha taratibu za kufuatwa ili kufikisha nyenzo za uokoaji katika maeneo ya ajali katika nchi moja kwenda nchi nyingine na kwa haraka. Kwa hiyo, kuridhiwa kwa makubaliano haya kutatoa fursa ya utekelezaji wa makubaliano haya ambapo vifaa na nyenzo zitaweza kufika haraka katika eneo la ajali na hivyo kuokoa maisha ya wananchi na mali zao. Aidha, Tanzania itapata misaada ya haraka kutoka Kenya na Uganda wakati ajali zitakapotokea.

Kwa kuwa faida ya kukubali kuridhia Mkataba huo ni kubwa inapendekezwa kuwa Bunge lako Tukufu likubali kuridhia makubaliano ya nchi za Afrika Mashariki kuhusu Kusaidia na Kutumia Nyenzo za Utafutaji na Uokoaji ya mwaka 2002 *(The East African Community Agreement Concerning Inter-State Use of Search and Rescue Facilities).*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kusoma Azimio lenyewe. Azimio la Bunge la Kuridhia Makubalino ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu kusaidiana nyenzo za utafutaji na uokoaji,*(The East African Community Concerning The Inter-State Use of Search and Rescue Facilities).*

KWA KUWA nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Tanzania, Kenya na Uganda zimekuwa na utamaduni wa kusaidiana katika masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii:

NA KWA KUWA nchi hizi zilisaini Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The Treaty for the Establishment of the East African Community)* ambao unazitaka nchi wanachama kuweka mikakati ya kusaidiana inapotokea ajali:

NA KWA KUWA Mpango wa miaka mitano (2001- 2005) wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki unahimiza utekelezaji wa makubaliano ya kusaidiana inapotokea ajali:

NA KWA KUWA ibara ya 92, 93 na 94 za Mkataba ulioanzisha Jumuiya hiyo zinaelekeza kwamba nchi wanachama ziwe na makubaliano ya kusaidiana yatakayowezesha nyenzo za uokoaji kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine yenye janga au ajali na ambapo Serikali za Tanzania, Uganda na Kenya zilitiliana saini makubaliano ya kusaidiana wakati wa ajali mwezi Novemba, 2002:

NA KWA KUWA faida itokanayo na utekelezaji wa makubaliano hayo ni kufikisha nyenzo za uokoaji katika eneo la janga au ajali kutoka nchi moja mwanachama wa makubaliano hayo hadi nchi nyingine kwa haraka na hivyo kuokoa maisha ya wananchi na mali zao:

NA KWA KUWA matokeo ya kuridhiwa kwa makubaliano ni nchi yetu kuwa na uhakika kupata msaada kutoka nchi nyingine wanachama wa makubaliano hayo pale itakapotokea janga au ajali:

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya makubaliano haya Bunge hili katika Mkutano wa 17 na kwa mujibu wa ibara 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kwamba linaridhia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Kusaidiana Nyenzo za Utafutaji na Uokoaji *(East African Community Agreement Concerning Inter-State Use of Search and rescue Facilities).*

Tano, makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya Afrika kuhusu taratibu za uendeshaji vyombo vya usafiri majini katika mito na maziwa ya usafiri ya mwaka 2002 *(The East African Tripartite on Inland Waterways Transport, 2002)*

Mheshimiwa Spika, makubaliano haya yanahusu taratibu za uendeshaji wa vyombo vya usafiri majini na biashara ya uchukuzi wa vyombo hivyo katika Mito na Maziwa kwa nchi wanachama. Yana lengo la kuimarisha Miundombinu na taratibu za uchukuzi katika Mito na Maziwa ya nchi wanachama ili kuongeza tija katika usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria kwa kutumia mito na maziwa.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yaliyomo kwenye makubaliano ni pamoja na yafuatayo. Taratibu za vyombo vya usafiri wa majini kufanya safari za Kibiashara toka nchi moja hadi nyingine. Taratibu za udhibiti wa vyombo vya usafiri maji

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania kuridhia makubaliano haya faida zake ni pamoja na zifuatazo:-

1. Kuimarisha Miundombinu ya usafiri katika maziwa na mito;

3. Kuimarisha udhibiti wa usalama wa usafiri katika maziwa na mito;

4. Kurahisisha taratibu za biashara ya usafirishaji kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa faida ya kukubali kuridhia makubaliano haya ni kubwa inapendekezwa kwamba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu taratibu za uendeshaji wa vyombo vya usafiri majini katika mito na maziwa ya mwaka 2002. *(The East African Tripartite on Inland Waterways Transport, 2002)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kusoma Azimio lenyewe. Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu taratibu za Uendeshaji wa Vyombo vya Usafiri katika Mito na Maziwa ya mwaka 200 *(The East African Tripartite on Inland Waterways Transport, 2002)*

KWA KUWA tangu kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999 kumekuwepo na makubaliano mbalimbali kati ya nchi wanachama wa Jumuiya:

NA KWA KUWA mojawapo ya makubaliano hayo ni yale yanayohusu taratibu za uendeshaji wa vyombo vya usafiri wa majini na biashara ya Uchukuzi katika mito na maziwa kwa nchi wanachama wa Jumuiya Afrika Mashariki. *(The East African Tripartite on Inland Waterways Transport, 2002)* yaliyotiwa saini mwaka 2002:

NA KWA KUWA makubaliano hayo yana lengo la kuimarisha miundombinu na taratibu za uchukuzi katika mito na maziwa ya nchi wanachama ili kuongeza tija katika usafiri na usafirishaji wa mizigo na abiria na kwa kutumia mito na maziwa:

NA KWA KUWA nia ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuweka misingi ya kisheria itakayosaidia katika kuboresha huduma za uchukuzi katika maziwa na mito kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu kama zilivyoanishwa kwenye makubaliano:

NA KWA KUWA Serikali zetu tatu za nchi wanachama wa Jumuiya zimeazimia kutekeleza matakwa ya vifungu nambari 93, 94, 95 na 100 vya Mkataba uliosainishwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki:

NA KWA KUWA matakwa ya Mpango wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa miaka mitano (2001- 2005) yanataka kuwepo kwa usafiri mzuri na wa

uhakika wa abiria na mizigo baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kuwezeshwa ukuaji wa uchumi wa nchi wanachama:

NA KWA KUWA matokeo ya kuridhiwa kwa makubaliano hayo ni kuwepo kwa mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji katika biashara ya usafirishaji na hivyo sekta ya uchukuzi kuweza kutekeleza jukumu lake la kuwezeshwa sekta nyingine kutekeleza majukumu yao:

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu Bunge hili katika Mkutano wa 17 kwa mujibu wa ibara ya 63 (3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kwamba linaridhia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu taratibu za uendeshaji wa vyombo vya usafiri katika mito na maziwa ya mwaka 2002 *(The East African Tripartite on Inland Waterways Transport, 2002).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono kabla sijamwita Mwenyekiti niwaarifu tu kwamba waliojiandikisha kuchangia Maazimio yote haya wako watatu. Mheshimiwa Prof. Maghembe, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala. Inawezekana. Nasema inawezekana mtoa hoja kama atasema kwa ufupi mtoa hoja akajibu na kazi iliyoko kwenye *Order Paper* ikaisha asubuhi hii. Kwa hiyo, kwa kuwa tuna Maazimio mengi ninakuwa nashauriana na *Chief Whip* wa Serikali kwamba pengine tutoe *Order Paper* ya nyongeza Azimio moja zaidi liweze kushughulikiwa kipindi cha mchana linatokana na Wizara ya Mheshimiwa Edward Lowassa.

Sasa ni vizuri basi Kamati inayosimamia ajiandae kutoa maoni ya Wizara Mheshimiwa Simpassa yatakapowasilishwa na vile vile Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Khalifa, kama hayupo hapa sasa hivi utamtafuta umwarifu kwamba inawezekana Azimio la Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo linalowasilishwa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo likawa kwenye *Order Paper* ya mchana ili wajiandae kutoa maoni ya vyombo vyao.

Kwa sasa namwita Mwenyekiti *or rather* Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Maazimio haya naye atawasilisha kwa ujumla. Lakini kabla hujafanya hivyo namwomba Mheshimiwa Simpasa anipokee kiti kwa sababu mimi nimepangiwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge wa *SADC* niliowatambulisha asubuhi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA MIUNDO MBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundo Mbinu, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati kuhusu Maazimio ya Bunge kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyowasilishwa chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu 63 (3) (c) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 Bunge litajadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano ambayo kwa masharti yake inapaswa kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu pia wa kanuni ya Bunge Kanuni ya 88 (2003) Kamati ya Bunge ya Miundo Mbinu ilipata fursa ya kuipitia Mikataba iliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwenye Kamati ili kujadiliwa na kupata maoni na ushauri wa kuliwezesha Bunge lako tukufu kujadili na kuridhia Mikataba ya makubaliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba iliyopitiwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

Azimio la kwanza la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa uingiliaji kati kwenye bahari kuu iwapo kunatokea ajali wa mwaka 1969 na itifaki ya uingiliaji kati iwapo kutatokea uchafuzi wa mazingira unaotokana na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta ya mwaka 1973*(International Convention Relating to Intervation on high seas 1969 and Protocol for marine Pollution by substances 1973).*

Azimio la pili la kuridhia Mkataba Kimataifa wa kanuni za kuzuia kugongana kwa meli baharini ya mwaka 1972 *(Conventional on the International Regulations for Preventing Collision at Sea 1972).*

Tatu, Azimio la kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu uokoaji baharini wa mwaka 1979 *(International Conventional on Maritime Search and Rescue 1979).*

Nne, Azimio la kuridhia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kusaidiana nyenzo za utafutaji na uokoaji *(The East African Community Agreement Concerning the Inter- state use of Search and Rescue Facilities).*

Tano Azimio la kuridhia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu taratibu za uendeshaji vyombo vya usafiri katika mito na maziwa ya mwaka 2002 *(The East African Tripartite Agreement on Inland Waterways Transport 2002.*

Mkataba wa Kimataifa wa kujiandaa kukabiliana na janga la kuvuja kwa mafuta wa mwaka 1990 *(The International Conventional for Oil Pollution Preparedness Response and Cooperation 1990). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa kamati, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge 88 (9) ya mwaka 2003 kwa ujumla sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu azimio la kuridhia Mikataba iliyowasilishwa na Serikali kama ilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake zilizoleta manufaa makubwa kwa taifa letu. Aidha Kamati inaishauri Serikali ifanye linalowezekana ili mikataba kama hii iwe inaridhiwa na Bunge lako tukufu mapema na wakati unaotakiwa. Hili linagusa sana mikataba inayohusu Jumuiya ya Afrika Mashariki Tanzania ikiwa mojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kutokana na umuhimu wa mikataba hii katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, kutunza mazingira, kulinda viumbe vya majini, kulinda vyombo vya majini na watumiaji wake, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati ya kuwezesha kutekelezwa kwa Maazimio haya. Hii ni pamoja na kulipa ada stahili kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa misaada inayoletwa Bungeni ishabihiane na kukidhi mahitaji kulingana na mikataba inayoridhiwa. Aidha katika kuhakikisha kuwa mikataba hii inatekelezeka Serikali inapaswa kuzifanyia marekebisho sheria zilizopo ambazo bado zina upungufu au kutunga mpya kwa maeneo ambayo bado hayana sheria.

Nne, Serikali imechelewa katika utekelezaji wa azimio la kuridhia makubaliano ya Nchi za Afrika Mashariki kuhusu uokoaji baharini wa mwaka 1970 *(International Conventional Maritime Search and Rescue 1979).* Kwani kama yangefanyiwa kazi mapema huenda majanga kama ya *MV Bukoba* na mingine yasingekuwa makubwa. Kamati inashauri Serikali iunde chombo maalum kwa ajili ya kufuatilia vyombo vya majini hususan katika maziwa yetu makuu ili kusiwe na ukiukaji wa sheria.

Tano, Kamati inaishauri Serikali kujiandaa katika kukabiliana na majanga kwa kuhakikisha kuwa kuna vitendea kazi na watalaam wa kutosha. Aidha elimu ya kutosha itolewe mara kwa mara kwa wenye vyombo vya majini pamoja na watumiaji wake ili kulinda vyombo majini na watumiaji na viumbe vinavyoishi majini.Ushauri wa sita, ili kuwepo na utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa kujiandaa kukabiliana na janga la kuvuja kwa mafuta wa mwaka 1990 *(The Intenational Convention for all Pollution Preparedness Response in Cooperation year 1990)* Kamati inashauri kuwa kwa vile Tanzania ina eneo kubwa la ufukwe Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi iweke utaratibu wa kufuatilia meli zinazopitia nchini ili kuhakikisha kuwa hazimwaga mafuta. Juhudi za makudi zifanyike kununua rada na boti ziendazo kasi kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba saba Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuwezesha utekelezaji wa mikataba inayoridhiwa ili kufungua wigo wa ushirikiano wa Kimataifa katika uchumi na uwekezaji.

Hitimisho, awali ya yote namshukuru Mheshimiwa Dr. Maua Daftari Mbunge Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na watendaji wote wa Wizara yake kwa kuwasilisha Maazimio haya kwa ufasaha jambo ambalo linairahisishia kazi Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Miundo Mbinu kwa ushirikiano wapo pamoja na moyo wa kujitoa katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Baada ya maoni na ushauri huo sasa naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Kamati ya Miundo Mbinu, imejadili Maazimio yote na kwamba yamezingatia mahitaji ya nchi. Kwa hiyo, basi Kamati inaliomba Bunge lako tukufu lijadili na kuridhia Maazimio na Mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu kuridhia Makubaliano na Mikataba mitano ya Kimataifa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kutoa Maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1) toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuleta maazimio haya kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge hili, kwani Tanzania ilikwisha kubaliana na mambo yote yaliyomo kwenye Mikataba yenyewe, kutekeleza Mikataba hii itaisaidia Tanzania isipatwe na majanga makubwa na mabaya ambayo yaliwahi kutokea kwa kipindi cha miaka ya nyuma ili yasiweze kutokea tena.

Moja, Azimio la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa uingiliaji kati kwenye bahari kuu iwapo itatokea ajali ya mwaka 1969 na itifaki yake iwapo kutatokea uchafuzi wa mazingira unaotokana na bidhaa nyingine zaidi ya mafuta ya mwaka 1073. *(International Convention Relating to Intervention on the high seas 1969 and the protocol for marine pollution by substances 1973)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haina pingamizi ya uridhiwaji wa azimio hili, ila inatoa ushauri katika mambo yafuatayo, kwanza, Serikali iwe na vifaa vya kuangalia vyombo vinavyopita na kufanyakazi katika *high seas,* kitu kitakachosaidia na kuwa mshiriki halisi katika mkataba huu.

Pili, Serikali ianzishe utaratibu wa kuzungukia maeneo yake katika high seas kuangalia umiliki na shughuli za vyombo vilivyo kwenye maeneo hayo. Tatu, tuwaandae wataalam wetu kiteknolojia na kinyenzo za kisasa ili waweze kufanya ukaguzi wa vyombo vinavyoingia na kutoka kwetu kuhakikisha kuwa viko kwenye standards

zilizobainishwa ndani ya mkataba huu tunaouridhia. Mheshimiwa Waziri amesema kuwa moja ya faida za kusaini mkataba huu ni fidia inayotokana na uharibifu. Katika hili Kambi ya Upinzani bado haijaona fidia kuoanishwa na uharibifu, hivyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri, weka wazi ni fidia kiasi gani inayoendana na kiwango gani na aina gani ya uharibifu, kwani tulisha soma malalamiko ya nchi za Africa ya Magharibi ambapo meli za kigeni zilikuwa zinamwaga mabaki ya kemikali ya *nuclear* kwenye maeneo ya nchi zao, hili nalo fidia itakuwa ni sawa na kuvuja kwa mafuta mapipa kumi? Azimio la kuridhia mkataba wa kimataifa wa kanuni za kuzuia kugongana kwa meli baharini wa mwaka 1972. *(International Convention for Regulations for Preventing Collisions at sea, 1972)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani tunaunga mkono kuridhia mkataba huu, lakini tuaishauri Serikali iweke utaratibu wa kukagua vyombo vyetu ili viwe na vigezo vilivyomo kwenye mkataba huu yunaouridhia kabla hatujaanza kuangalia na kukagua vyombo vya wengine vinavyopita au kuja kwetu. Ajali za meli sio lazima ziwe meli kwa meli tu, bali hata meli na mwamba au hata kugonga vyombo vidogo vinavyotumiwa na wavuvi wetu hapa nchini wanaotumia vyombo ambavyo havina vifaa vilivyoainishwa. Azimio la kuridhia mkataba wa kimataifa unaohusu uokoaji baharini wa mwaka 1979. *(International convention on maritime search and rescue 1979).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sisi hatuna matatizo na kuridhia mkataba huu, lakini tunauliza kama nchi yetu kiuchumi iko tayari kutimiza matakwa yaliyoainishwa katika mkataba wenyewe? Kwa kuwa Mkataba huu umeainisha vifaa vya uokoaji ambavyo gharama zake ni kubwa kulinganisha na uchumi wa nchi kama ya kwetu. kwa kuwa uokoaji ni taaluma Chuo cha *Dar es Salaam Maritime Institute* kiimarishwe kitoe taaluma hii kwa vijana wa nchi hii na nchi za jirani. Ni jambo la aibu nchi inapopatwa na janga kama la kuzama kwa meli, nchi inahangaika kupata waokoaji kutoka nchi zingine. Tunashauri Serikali ijitayarishe kuwa na nyenzo ili iweze kuwa mwanachama hai katika kutekeleza mkataba huu, vile vile itakuwa imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta iusuyo usafiri na uvuvi baharini.

Azimio la kuridhia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kusaidiana nyenzo za utafutaji na uokoaji 2002. *(East African Community Agreement Concerning Inter-state use of Search and Rescue Facilities 2002)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Ibara ya 2 mpaka ya 7 ya makubaliano haya ni muhimu katika kufanikisha utafutaji na uokoaji, hasa kwa kuzingatia uhaba na uduni wa nyenzo uliopo katika nchi moja moja. Ajali ya meli ya *MV Bukoba* mwaka 1996 kule Ziwa Victoria Mwanza ilionyesha wazi ukosefu wa zana za kisasa na za kutosha za uokoaji na utafutaji unavyoweza ukawa na athari kubwa katika maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri. Ili kuimarisha mchango wake katika makubaliano haya ni lazima Tanzania ijiimarishe kwa vifaa na mafunzo kuhusu utafutaji na uokoaji. Usimamizi na udhibiti wa usafiri wa majini kwa maana ya mito na maziwa na

hata baharini ni lazima uboreshwe. Tanzania isiingie katika makubaliano kwa kuamini Kenya na Uganda zina vifaa bora vya utafutaji na uokoaji, hivyo nchi hizo zitaibeba Tanzania. Aibu ya kuita wana maji na waokoaji kutoka Afrika Kusini wakati wa ajali ya *MV Bukoba* kulionyesha ukosefu mkubwa wa utayari wakati wa majanga. Umoja na ushirikiano ni kuchangia nguvu na siyo taifa moja kutegemea kubebwa na mengine kwa kushindwa kuimarisha uwezo wake wa ndani.

Azimio la kuridhia makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Africa Mashariki kuhusu taratibu za uendeshaji vyombo vya usafiri katika mito na maziwa ya mwaka 2002 *(The East African Tripartite on Inland Waterways Transport, 2002)*

Mheshiwa Mwenyekiti, tunaunga mkono makubaliano haya kwani itakuwa chachu ya kukuza uchumi na kudumisha ushirikiano wetu. Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kuwa na maziwa na mito mingi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kazi mbalimbali kama kilimo, usafirishaji na ufuaji wa nishati. Hata hivyo maziwa na mito yetu haitumiki ipasavyo kutokana na kuwa na miundo mbinu duni. Hii inatokana na kuwa hatutoi kipaumbele kwenye maziwa na mito yetu kwa ajili ya usafirishaji. makubaliano haya yasiwe na upendeleo wa uendelezaji na uimarishaji wa miundo mbinu kwa bandari za Ziwa Victoria tu na kusahau sehemu zingine za mito na maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati wa kuendeleza yale yote ambayo yameainishwa katika makubaliano haya na naamini makubaliano haya yataleta changamoto ya kuendeleza miundo ambayo kwa njia moja ama nyingine itazinufaisha si nchi zilizomo kwenye makubaliano tu bali hata zile zisizo kuwemo kwenye makubaliano kama vile Malawi, Zambia, Msumbiji na Jamhuri ya watu wa *Congo (DRC)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika maazio haya ambayo Bunge limeombwa kuyapitisha. Niseme hapa mwanzo kabisa kwamba sina matatizo na mikataba hii. Ila ningependa nitoe mawazo hasa yanayohusu kuhakikisha kwamba njia za maji Afrika ya Mashariki hasa katika azimio la tano kwamba njia hizi za usafirishaji *(The East African Tripartite Inland Waterways Transport)* zinakuwepo. Kwamba nchi moja haichukui hatua ambazo zinafanya njia za usafiri wa maji zitoweke.

Kwa hiyo, napenda nishukuru Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa busara kubwa ya kuleta Maazimio haya yaweze kuridhiwa na Bunge na kwamba makubaliano mengine yamekuwa muda mrefu lakini mimi nadhani bado ni wakati muafaka wa kuyapitia na kuyapitisha. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitashughulika zaidi na azimio lile la tano na la mwisho maana lile linagusa hasa jimbo langu uchaguzi. Katika jimbo langu la uchaguzi ziwa la Jipe limekauka na suala hili tumelileta hapa kwenye Bunge mara nyingi, kwa njia ya maswali na kwa njia ya kuchangia katika hotuba za bajeti.

Lakini inaelekea kwamba halichukuliwi maanani na kuchukuliwa hatua inayostahili. Ninalisema hili kwa sababu katika *Tripartite Inland Waterways,* kukauka kwa ziwa kunaondoa kabisa hiyo *transport system*. Kwamba hiyo *transport system* inaondoka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziwa hili limekauka kwa sababu ya hatua ya hizi ambayo nchi nitaija kwa jina kabisa. Kwa sababu ninaamini kabisa kwamba *tripartite* ina maana ya Tanzania, Kenya na Uganda na kwa sababu hiyo, sitasema nchi ya jirani, nitasema nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa la Jipe limekauka kwa sababu nchi ya Kenya imezuia mto unaoingia kwenye ziwa na kuupeleka kufanyia shughuli zake. Nimeambiwa kwamba wanamwagilia. Lakini wamechukua mto mzima unaoingia kwenye ziwa na kuupeleka kumwagilia maji. Kwa hiyo, sasa ziwa linakauka na hakuna tena *medium ya transportation* katika eneo lile. Kukauka kwa ziwa kuna athari kubwa sana pamoja na kuondoa kabisa njia ya kufanyia safari kwenye ziwa lile. Unawanyima wananchi wa Kata za Jipe na Kwakoa katika Vijiji vya Kitoghoto, Jipe, Butu, Ugweno eneo la Mkisha, Ruru na Toloha hakuna maji ya kunywa. Unawanyima wananchi hao maji ya kuwapa mifugo yao. Hakuna maji ya kuwapa mifugo. Nasikia kuna mkutano mwingine humu. *(Kicheko)*

Lakini pia unawanyima wananchi wa kata hizi njia ya kujikimu kwa kutoweka kwa shughuli za uvuvi ndani ya ziwa. Hakuna uvuvi tena. Samaki wamekufa wameondoka, kinaua viumbe hai au banuwai yetu *completely.* Hakuna kitu kinabaki pale. *Valuable genetic resources* inaondoka ya mimea, ya wanyama kama samaki, ndege, wadudu na wanyama wakubwa wa maji, wote wanatoweka.

Sasa kukauka kwa ziwa kumefanywa kwa hatua *unilateral* iliyochukuliwa na nchi ya Kenya. Imechukua *unilateral action* kufunga mto, kuchukua hatua ya peke yake bila ya kushauriana na sisi, bila kushauriana na mtu yeyote, *unilateral action.* Kufunga mto na kukausha ziwa lote bila kujali madhara yake kwetu ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki ni kiburi cha ajabu sana, kwa sababu Serikali ya Kenya haijali shida inayowapata wananchi wa Tanzania wanaokaa karibu na ziwa hilo. Sasa pamoja na faida ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri na mimi kwa kweli ninazikubali. Hali halisi ya kiburi hiki haiwezi kuachwa ikaendelea tu kwa sababu sisi tutapata faida hizo. Haiwezekani.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue hatua ya haraka kuiambia Serikali ya Kenya ifungue maji yanayoingia kwenye ziwa Jipe mara moja. Wala lisiwe suala la kubembelezana maana kama wanaweza kufunga mto unaoingia kwenye ziwa, hivi sisi tunashirikiana nao kwa sababu gani? Kama hawana huruma na wananchi wetu tunashiriki nao namna gani? Sasa hivi vijiji nilivyotaja wananchi wanahama.

Sasa kama mtu kweli tunashirikiana naye hana huruma, anawanyima wananchi wetu maji ya kunywa, hivi tunashirikiana naye kwa sababu gani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ichukue hatua ya haraka ku-*restore* hiyo *waterway* chini ya mkataba huu. Sasa sijui kama *conservation kuchukua all necessary measures za ku-conserve waterways* na kuhakikisha zinakuwepo in *perpetuity* sijui kama iko katika mkataba huu. Lakini kama haipo ni vema kwa mfano huu ikawekwa kwenye mkataba. Ni vema mkataba huu ukaona kwamba una-*short comings* kubwa kabisa ambazo hazina *provision* ya kuhakikisha kwamba *waterways* zenyewe ambazo tunaziwekea mkataba zinakuwa na *sustainable management.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ya mfano huu ingekuwa vizuri katika mkataba huu kwa kweli kukawa na *instrument* ya kushauriana kabla ya nchi yeyote haijachukua *unileteral action* ya maji ambayo yanahusu au yana maslahi kwenye nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ingekuwa vizuri pia njia za maji za mito, maziwa yanayohusu mkataba huu yaorodheshwe *very clearly* na yawekwe kama *appendix* ya huu mkataba. Ili kukiwa na nia ya kutumia maji ya mito na maziwa hayo basi kuwe na ushauriano na nchi zile zingine ambazo zinahusika.

Jumuiya ya Afrika Mashariki, iwe na kitengo ambacho kinaweza kupokea, kuratibu na kutoa ushauri wa haraka kuhusu matumizi haya. Maana yake *consequence* za matumizi ambayo ni *unileteral* zinaweza kuwa *very far reaching* kwa majirani zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri pia kwamba Serikali ichukue hatua kuona kwamba Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki linakuwa na Kamati ambayo inaratibu mambo haya. Inaratibu utaratibu huu wa utumiaji wa mali asili ya maji ambayo ni *common* katika zaidi ya nchi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo na natumaini kwamba Serikali itayapokea na kuyashughulikia mapema iwezekanavyo maana wananchi wanahama katika sehemu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawashukuru sana na nitaunga mkono hoja hii kwa sababu italeta mbele ya macho ya wananchi wote matatizo yanayohusu *waterways* hizi na faida ambazo tunaweza kupata kwa kuridhia mkataba huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kidogo katika maazimio haya yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe utakuwa shahidi wakati nimeomba Kamati ya Kilimo kwenda Mtwara na Lindi na Serikali ikakubali na Bunge likakubali ili kwenda kupata uhakika wa matatizo ya wakulima wa Korosho bei na upatikanaji mgumu wa pembejeo. Tulikubaliana na Kamati tukaenda sehemu moja inaitwa Msimbati. Msimbati tukajionea mambo mengi pamoja na Pwani nzuri, kuna *beach* ambayo unaweza uka-*drive* kwa zaidi ya kilometa 20 kwa gari ya uzito wowote ule. Lakini kuna mchanga ukitembea unalia fedha, fedha, fedha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, sisi Wamsimbati tumeamua kwa makusudi kuhifadhi na kulinda Pwani ile. Lakini kuna meli sijui zinatoka nchi gani zinakuja kutuharibia mazingira yetu ya Msimbati, kwa sababu sisi nia yetu ni kulinda mazingira yale ili kuvutia wawekezaji watakaokuwa na uwezo wa je kuja kujenga Mahoteli makubwa makubwa pale ya kitalii. Kwa kupitia Muswada huu na mchango huu, natangaza rasmi kwamba wenye uwezo wa nje na ndani waje kujenga mahoteli makubwa makubwa Msimbati. Karibuni sana. *(Kicheko)*

Lakini sifa ya Msimbati ni *Clinic* ya kuzalia au kujifungulia wanyama wa bahari wanaoitwa nyangumi. Tumeelezwa pale na mtaalam mmoja kwamba nyangumi wanatoka Afrika ya Kusini wanakuja Msimbati kuja kujitazamia muda wao ukiwa karibu na kujifungua wanakuja kujifungulia pale kisha wanakaa...

**MBUNGE FULANI:** Kuzaa.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Kuzaa eh!

**MWENYEKITI:** Kwa lugha iliyo sahihi sio kujifungua, ni kuzaa.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Kumbe ni kuzaa!

**MWENYEKITI:** Eeh.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Wanakuja kuzaa halafu watoto wao wakiwa na nguvu wanarudi tena Afrika Kusini na sehemu nyingine. Kwa hiyo, maeneo yale ni mazuri sana kwa utalii. Sasa kuna meli za nje zinakuja kuvua nyangumi wale na sisi watu wa Msimbati wanatuharibia mazingira yetu. Sasa katika Maazimio haya nilikuwa naomba Serikali itafute namna ya kuchomeka hili ili kuweza kufuatilia na kuzuia uharibifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa na watu wa Msimbati kuja kulielezea Bunge habari hizi na kuiomba Serikali iweke mikakati ya kukomesha hili. Ahsanteni sana.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie maazimio haya. Nashindwa kusema matano kwa sababu mahesabu yangu yamekwenda vibaya kidogo na nitaeleza.

Mimi nilidhani hili Azimio la kwanza la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Uingiliaji Kati Bahari Kuu iwapo Itatokea Ajali ya Mwaka 1969; halafu na Itifaki ya Uingiliaji Kati iwapo Kutatokea Uchafuzi wa Mazingira ya Mwaka 1973, nilidhani mawili halafu yatakayofuata haya yatakuwa sita. Kwa hiyo, naona walivyosoma wenzangu walisema matano, lakini hata hivyo yote ni Maazimio ambayo yameeleweka kwa sababu kila kitu kina maelezo yake. Kwa hiyo whether yako sita au matano, lakini yote yanalenga katika utaratibu ule ule. Isiwe kama mimi leo asubuhi nilinunua kadi, nimeuliza mna kadi ya *Vodacom?* Wakanimbia zipo. Naomba kadi moja ya dola mbili. Sikutaja jina, nikamwambia naomba basi nipe kadi moja. Nilitaka kadi ya dola mbili, sasa nikamwambia anipe moja, sasa akanipa dola moja kwa sababu tumeelewana kimahesabu, tulikuwa hatukuelewana pale. Sasa kwa hapa kwa Maazimio yamekwenda kwa haraka katika utaratibu.

Sasa baada ya kusema hayo nilitaka kusema kwamba *what is the next,* baada ya kuridhia kwamba wenzetu mmekutana na mkasaini kule, sasa kipi kinachofuata baadaye? Nadhani baadaye nchi zinazohusika katika orodha waliyoshirikiana, watakaa chini kutunga sheria ambazo zinakazia katika nchi zao ili kusimamia mambo haya. Nadhani nchi yetu ni moja katika haya. Sasa kama zipo sheria ambazo zilishatungwa ambazo zinalingana na Maazimio haya, basi kama kuna mapungufu pamoja na kwamba Azimio limekuja leo, basi sheria hizo ziimarishwe. Kwa sababu zipo sheria kama za Uchafuzi wa Mazingira, sheria kama ya Mazingira, Ajali, Mioto, Uchafuzi, Bioanuwai, zilishatungwa tayari, maeneo chepechepe. Kwa hiyo hizi zitakuwa zinalingana ili kuweza kukidhi ziendane na wakati na haya Maazimio ambayo tunayapitisha. Lingine ambalo nimeliona kwenye Azimio ni kwamba nchi zilizoazimia bahati mbaya hazipo, lakini kuna idadi katika Azimio la kwanza na la pili, tumeona kuna orodha ya kemikali ambazo ziliorodheshwa katika hili. Sasa hizi pengine kwa sababu Azimio la mwaka 1973 pengine kuna kemikali nyingine zimeongezeka kwa sababu kuna chama *polymers.* Teknolojia kemikali imeongezeka naona kuna panya *and smell and evacuated compounds hazimo, polysterick and dehydration, highly inflammable substances; kuna deliqoconsent,* kuna vitu kama *hydroscopic,* mtu anaweza kupeleka chumvi ambayo *hydroscopic* ikawa nyingi ikaharibu mazingira kwa ku-*peak out the humidity* ya eneo lile la mwambao.

Halafu kuna *preventive solvents* na vitu vingine vinatupwa baharini. Halafu lingine nimekuta kwenye kemikali nyingine zimeandikwa na *percentage* kwa mfano *nitric Acid 40%, citric* yaani *hydroid 90%, benzyl hydroid* wanaandika na *percentage.* Sasa zitakapomwagika baharini, sijui ile *percentage* nitaijuaje kwa sababu tayari itakuwa *diluted.* Sasa hizi *percentage* watu waadhibiwe tu kwa aina ya dawa ambayo imetupwa baharini, wasiadhibiwe kwa kiasi cha asilimia kilichotajwa kwenye orodha maana watu ni wajanja wanaweza wakakiuka kwamba kisheria hapa imeandikwa *mercury acid 40%* sasa ikiwa kwenye bahari ikishamwagwa tayari haiwi 40%. Kwa hiyo, itakuwa imekuwa *diluted.* Kwa hiyo, hiyo ilikuwa pengine ni ujanja wa wakubwa tu katika kuweza kuzidhalimu nchi maskini. Sasa bahati nzuri tunayo mitambo mizito na mizuri katika Ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu, kwa hiyo inaweza ikafanya kitu kama hiki kuona kwamba kitu hiki ni kitu fulani. Kwa hiyo, kwa *percentage* kwenye bahari kwa sababu maji ya bahari ni *solvents* kwa hiyo ukichukua sample kwenye bahari

kutaka ku-*check* utaona aina tu lakini utapata *part per* milioni kwa sababu ya kiasi kitakachotupwa. Kwa hiyo, adhabu au faini tutakazowapa Serikali kwa hao watu watakaomwaga tuwape kwa aina ya orodha iliyotolewa hapa. Nyingine zinakuwa ni *soluble* katika maji na nyingine zinakuwa zinaelea.

Kwa hiyo, unakuta kwamba na madhara ambayo yataletwa yanachukua muda mrefu kwa mfano kama *hydrogen sulphate* inachukua t*en years* mtu akagundua akaanza kuchanganyikiwa vitu vingine. Kwa hiyo, watu waweze ku-*identify* halafu watasema kitatokea hiki. Kwa hiyo, nchi iweze kushitaki kwa kufanya references, unatumia tu vitabu vilivyopo kama *Britphamacopier* na mengine *word phamacopier* kuweza kujua vitu kama hivi kuweza kuwachukulia hatua. Wataalam mnao, vitu tunavyo na uwezo tunao.Baada ya kusema hayo, ni kwamba sheria hii sasa katika hizi, tuliona Maazimio kwa maana ya *East African Community,* mambo ya maziwa, upande wa maziwa. Kwa mfano kuna maziwa mengine tunasema *East African Community*, lakini kwa maziwa ambayo yana nchi ambazo sio *East African Community,* kwa mfano Ziwa Nyasa, ipo nchi Malawi ambayo siyo *East Africa.* Halafu kwa mfano Ziwa kama Tanganyika lipo Zaire ambayo sio *East Africa,* ambayo kwa mfano Mto kama vile wa Nile uko nchi moja. Kwa hiyo, hapo jinsi ya kudhibiti kuwepo na hii sheria na ukubaliano wa nchi hizo katika kusimamia mtu na mwenzake, mwenzake na mtu, kwa hiyo tunakuwa pamoja ili kuweza kushirikiana kwa vizuri zaidi. Pamoja na kwamba nchi hazikutajwa, lakini zikifanya matatizo tutakutana katika nchi za maziwa makuu ili kusudi tuweze kuwaingiza na wao. Kwa sababu mwaka wa nzige panzi nao walikula. Naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtoa hoja, nafikiri muda unatosha. Kwa jinsi tunavyofahamu, muda utakutosha tu. Karibu sana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Henry Shekiffu aliyezungumza kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, Kamati ambayo tumebahatika kufanya nayo kazi na kila wakati tumebahatika na hekima, busara, umuhimu na uzito wa michango inayotokana na Kamati hiyo. Kwa hiyo, namshukuru sana. Kwa kweli kwa yote aliyoyazungumza hasa ushauri alioutoa ni katika maeneo saba. Mimi naomba niseme tu kwa mpigo kwamba yote hayo saba tutayazingatia katika utekelezaji wa mikataba hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Faki, Mbunge wa Ole na Waziri ambaye kwa muda mrefu sana ataendelea kukaa kivulini akingojea nafasi ambayo haitakuja ya *CUF* kuchukua uongozi nchi hii, lakini leo amezungumza utafikiri Mwana-CCM. Ametuunga mkono, tena amezungumza kwa hekima ya hali ya juu. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwa yote aliyoyazungumza na kwamba tutayachukua na tutayazingatia yote ambayo ametusaidia katika kuboresha utekelezaji wa Itifaki na Makubalino haya yote. Moja alilozungumzia ni kuhusu fidia kwamba hatukuainisha katika maelezo yetu na vile vile, hatukuyazungumzia. Hiyo ni kwa sababu kuna mikataba mingine miwili ya Kimataifa inayozungumzia suala la fidia tu katika matukio ya namna hiyo. Mikataba hiyo ni *The Fund for Compensation on Oil Pollution* pamoja na mkataba wa *Civil Liability*

*Convention,* Mikataba ambayo Bunge hili Tukufu tayari limesharidhia. Kwa hiyo, yote yaliyotaka yaainishwe yameainishwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Maghembe, kwa style ya Bunge hili amejaribu kuunganisha kama vile nikisema nina tatizo Rungwe Mashariki, basi kama unataka swali la nyongeza lazima useme naunganisha na lile la Rungwe Mashariki. Kwa sababu hili sisi tunazungumzia uchukuzi, sikutegemea kabisa kwamba ingeunganishwa na *Lake Jipe* na Uchukuzi. Kwani sikujua kwamba *Lake Jipe* vile vile lilikuwa maarufu kwa uchukuzi. Najua lilikuwa maarufu sana kwa *fishing* kwa maana ya uvuvi pamoja na kilimo na mambo mengine. Lakini aliyoyazungumza ni ya msingi sana. Nimejaribu kuangalia ni mambo gani tunaweza tukayazingatia katika maeneo yanayohusu uchukuzi na kukauka kwa Ziwa Jipe. Lakini naomba Mheshimiwa Profesa Maghembe akubali tu kwamba hili suala kimsingi ni la mazingira na Mheshimiwa Ntagazwa amelizungumzia mara nyingi sana hapa na nina uhakika kwamba Wizara inayohusika na mazingira ni Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), tayari imeshawasiliana na Serikali ya Kenya kuhusu jambo hili kutokana zaidi na mchango wa Mheshimiwa Profesa Maghembe, lakini vile vile kutokana na tatizo hili ambalo ni kubwa. Vile vile katika mazungumzo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania vile vile inalichukulia hili suala kwa umuhimu wake, ni suala muhimu na tutaendelea kulifuatilia kama Serikali. Hilo ndio linaweza kuwa jibu kwa sasa kwa hoja ya Mheshimiwa Profesa Maghembe. Lakini kwa kweli ni kitu muhimu, kama haliwezi kuzungumziwa kwa maana ya Mkataba huu, lakini lazima kulizungumzia kwa maana ya Mikataba mingine kwa sababu tuna Mto Kagera, Mto Mara, kuna maeneo mengi ambayo yanahusisha nchi zaidi ya moja katika Afrika Mashariki; tuna matumizi ya Ziwa Victoria vile vile. Kwa hiyo, kukauka kwa chanzo cha uchukuzi kunakoleta athari za kimazingira lazima tuweze tukazungumza kwa njia hii kupitia Mkataba huu, lakini vile vile kupitia Mikataba mingine ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Amelizungumza kwa uchungu sana, lakini ndio maana tuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili tuweze tukayazungumza masuala ya namna hiyo kwa undugu. Hili vile vile naamini tutalimaliza kwa undugu huo huo.

Mheshimiwa Namkulala amezungumzia kwa uchungu kuhusu Msimbati. Msimbati, naweza kusema ni bahari au ni tuzo ambayo Mwenyezi Mungu ameipa Tanzania. Ni eneo la ajabu kabisa na eneo zuri sana. Nimefika kule mimi mwenyewe, lakini anavyosema mchanga unakanyaga unasema fedha, fedha! Ni kweli. Kwa sababu Msimbati tumepata gesi kule! Kwa hiyo, huenda baada ya uchunguzi zaidi tukapata mafuta. Msimbati kuna kitu kinaitwa *oil sand,* mchanga wenye mafuta lakini hatujagundua hayo mafuta yako wapi. Kwa hiyo, ninayozungumza ni mambo muhimu sana. Tutazungumza na wenzetu Mheshimiwa mhusika na Maliasili yuko hapa amesikia kuhusu hao nyangumi na tutajitahidi kufanya kazi pamoja na vile vile Mheshimiwa anayehusika na Mheshimiwa Waziri mwenzangu anayehusika na mazingira ili tuweze tukaliangalia na sisi tunahusika na meli, yote hayo tutaangalia kwa pamoja kwa sababu yana uwiano. Kwa hiyo, namhakikishia tutafanya hivyo kwa sababu ya umuhimu wa Msimbati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Semindu Pawa, kwanza ametukumbusha kwamba kwa kweli kuna Mikataba sita hapa, ule mmoja ni kama umebebwa na mwingine. Ule Mkataba wa

kwanza unazungumzia meli zikigongana mafuta yakimwagika basi uingiliaji kati unakuwaj? Baadaye wanachama wakasema tufanye nini iwapo hizo meli hazijabeba mafuta isipokuwa zimebeba bidhaa nyingine zaidi ya mafuta? Kwa hiyo, wakaandaa Itifaki iliyobebwa na huo Mkataba. Kwa hiyo, tukaona tulete Mkataba na mtoto wake kwa pamoja. Kwa hiyo, nashukuru kwamba ameoliona hilo. Kwa kweli ni Mikataba sita. Lakini hapo hapo niongeze kusema kwamba alipokuwa akiwasilisha Mheshimiwa Shekiffu aliwasilisha pia maoni ya Kamati kuhusu Mkataba ambao kwa kweli tutauleta tena baadaye na Mkataba huo ni *International Convention on Oil Pollution Preparedness Response and Cooperation of 1990.* Huu kwa bahati, kwa sababu ya taratibu za kiutawala haukuweza kutolewa katika orodha ya shughuli za Bunge za leo. Kwa hiyo, sisi katika maelezo yetu hatujauleta, isipokuwa tunashukuru kwamba tayari Kamati imeshaupitisha na imeshauzingatia. Tutakapokuja kuuleta rasmi Bungeni tutautolea maelezo, vinginevyo kungekuwa na Mikataba saba. Hayo ndiyo tunayoweza kujibu kwa sasa, tunaomba kurudia kuliomba Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Mikataba na Itifaki hizo tano au kwa maelezo ya Mheshimiwa Semindu Pawa, sita kwa ujumla wake na mmoja ukiwa umebebwa na mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa kwa sababu Maazimio yako matano, tutatoa maamuzi moja baada ya jingine. Huo ndio utaratibu.

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Uingiliaji Kati kwenye Bahari Kuu iwapo Kunatokea Ajali wa Mwaka 1969 na Itifaki ya Uingiliaji Kati iwapo Kutatokea Uchafuzi wa Mazingira Unaotokana na Bidhaa Nyingine Zaidi ya Mafuta wa Mwaka 1973.

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kanuni za Kuzuia Kugongana kwa Meli Baharini wa Mwaka 1973

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Uokoaji Baharini wa Mwaka 1979

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kusaidiana Nyenzo za Utafutaji naUokoaji

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Taratibu za Uendeshaji Vyombo vya Usafiri katika Mito na Maziwa wa Mwaka 2002

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Naona shughuli za Asubuhi zimeishia hapa. Kama Spika alivyotangaza, tutakuwa na Azimio lingine na shughuli nyingine tena leo jioni. Kwa hiyo, kwa sababu hatuna shughuli nyingine sasa hivi, tunasitisha shughuli za Bunge mpaka hapo saa 10.00.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**Azimio la Kuridhia Itifaki Kuhusu Maendeleo Endelevu katika Ufukwe Ufukwe wa Ziwa Victoria (*Protocol for Sustainable Development of Lake Victoria Basin)***

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio la Bunge kuhusu Tanzania kuridhia Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Ardhi na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa kuchambua Mkataba huu na kuukubali uletwe mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Tanzania, Kenya na Uganda zina uhusiano mkubwa na wa kihistoria katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii hususan shughuli za biashara, viwanda na utamaduni. Kijiografia nchi hizi zinaunganishwa na Ziwa Victoria pamoja na bonde lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki ulitiwa saini na Marais wa nchi zetu tarehe 30 Novemba, 1999. Mkataba huo pamoja na mambo mengine una lengo la kuitunza na kuliendeleza Bonde la Ziwa Victoria na kuzitumia kwa ufanisi rasilimali zilizomo katika bonde ili kuinua kipato cha wananchi wetu waondokane na umaskini. *(Makofi)*

Baada ya kusaini mkataba huu mwaka 1999 nchi wanachama wa Jumuiya hiyo zilitangaza bonde la Ziwa Victoria kuwa ni eneo la kukuza uchumi kwa nchi hizo. Aidha,

nchi zote tatu zimetayarisha dira na mkakati kwa kushirikiana na wadau wa bonde hilo na dira hiyo ilipitishwa na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mkataba huo wa kuunda Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, hususan kifungu Namba 151 kumeainishwa maeneo ya ushirikiano baina ya asasi mbalimbali katika Jumuiya hiyo. Miongoni mwa maeneo hayo ambayo yanakuwa sehemu ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni maendeleo endelevu ya bonde la Ziwa Victoria. Ili kutimiza azma ya mkataba makubaliano ya maendeleo endelevu ya bonde la Ziwa Victoria yalitiwa saini na nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 29 Novemba, mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Jumuiya ya Afrika, zinatambua usimamizi hafifu wa rasimali na mazingira kuwa unaweza kudumaza na kuathiri mazingira na rasimali zilizopo kwenye bonde. Hivyo, itifaki hii itakuwa ni chombo cha kusimamia hifadhi na mazingira na kukuza matumizi bora na endelevu ya rasilimali katika bonde. Aidha, Itifaki itaziwezesha nchi wanachama kuwa kitu kimoja katika kujadiliana masuala yanayohusu bonde hilo yaani *ku-negotiate as a block.*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo muhimu ambayo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutekeleza na ambayo yamezingatiwa katika itifaki ni haya yafuatayo:-

Kwanza, kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya hifadhi na matumizi endelevu ya rasimali hususan katika maeneo ya biashara, maendeleo ya viwanda, utalii, uimarishaji wa miundombinu, maji, nishati, usalama wa safari za majini, ubadilishanaji wa habari na taarifa. Hifadhi ya mazingira, ushirikishaji wa jinsia zote katika kupanga na kutoa maamuzi.

Pili, kuongozwa na misingi imara katika usimamizi na matumizi ya rasimali za bonde, hususan matumizi ya haki na usawa *(equitable and reasonable utilization)* ya maji na kadhalika.

Tatu, kuwa na sheria na sera zinazozuia vyombo vya usafiri wa majini, kumwaga takataka kwenye jua na kudhibiti uchafuzi wa maji kwenye bonde kutokana na takataka zenye sumu.

Nne, kuanzishwa Kamisheni ya Ziwa Victoria, *(Lake Victoria Basin Commission)* kwa ajili ya kusimamia na kuratibu shughuli za bonde. Kimuundo Kamisheni itakuwa na Baraza la Kisekta na Kamati ya Uratibu. Tanzania kama nchi mwanachama itahitajika kuchangia fedha kupitia bajeti yake ya kila mwaka kwenye Kamisheni ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kifungu cha 48 kinatoa msimamo wa nchi zetu juu ya uhusiano kati ya itifaki hii na mikataba mingine au mikataba ya zamani kuhusu Ziwa Victoria na inasema, nanukuu,“Endapo mikataba hiyo inakwenda kinyume na itifaki hii basi mikataba hiyo

itakuwa batili kulingana na kiasi au jinsi inavyopingana na itifaki hii." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ikiridhiwa na kutekelezwa, tunategemea nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kufaidika kwa njia mbalimbali kutokana na ushirikiano utakaopatikana katika utekelezaji wa miradi na kupunguza matatizo mbalimbali yanayohusu hifadhi, uendelezaji, matumizi na usimamizi wa rasimali za maji na mazingira ya bonde la Ziwa Victoria. Matokeo mengine ni kama yafuatayo:-

Kwanza, nchi zote tatu zitatumia rasilimali za maji katika bonde la Ziwa Victoria kwa misingi ya haki na usawa.

Pili, tutaweza kuweka mikakati ya pamoja na kubadilishana taarifa na takwimu zinazohusu rasilimali za maji katika bonde ili kuendeleza usimamizi madhubuti.

Tatu, kutakuwa na uendelezaji wa utalii, biashara na viwanda.

Nne, tutaweza kudhibiti na kuhifadhi bonde na mazingira yake kwa ufanisi zaidi.

Tano, kuongezeka kwa uwekezaji katika bonde kutaongeza shughuli za kiuchumi na kijamii katika eneo hilo na hivyo kuongeza uzalishaji na mapato kwa nchi wanachama.

Sita, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki tutashirikiana zaidi na kuwa kitu kimoja katika majadiliano yake yote ya masuala yanayohusu bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii itatumika kama sehemu ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itaanza kutumika baada ya kuridhiwa na nchi zote wanachama na nchi hizo kuweka nyenzo za uridhiaji kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo pale mjini Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kuwasilisha Azimo la Bunge kama ifuatavyo:-

**Azimio la Bunge kuhusu Tanzania kuridhia Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria (*Protocal for Sustainable Development of Lake Victoria Basin).***

KWA KUWA Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ambazo zina uhusiano mkubwa wa kihistoria katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii:

NA KWA KUWA Mkataba wa kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki ulitiwa saini na Marais wa nchi zetu tarehe 30 Novemba, 1999 ambao pamoja na mambo mengine, una lengo la kulitunza na kuliendeleza Bonde la Ziwa Victoria ili kuinua maisha ya wananchi wake katika kupambana na umaskini:

NA KWA KUWA baada ya kusaini Mkataba huo nchi wanachama zilitangaza Bonde la Ziwa Victoria kuwa eneo la kukuza uchumi kwa nchi hizo ambazo kwa pamoja zimetayarisha Dira na Mkakati kwa kushirikiana na wadau wa bonde hilo, dira hiyo ilipitishwa na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya mwaka 2003:

NA KWA KUWA ili kutimiza azma ya mkataba huo, makubaliano ya maendeleo endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria yalitiwa saini na nchi wanachama wa Jumuiya tarehe 29 Novemba, 2003:

NA KWA KUWA Tanzania inatambua umuhimu mkubwa wa kuwa na maendeleo endelevu katika Bonde la Ziwa Victoria, na kwamba usimamizi madhubuti utafanikiwa tu endapo nchi zinazohusika zitashirikiana kikamilifu katika uendelezaji endelevu wa Bonde la Ziwa Victoria:

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii kwa taifa letu na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Saba, sasa linaazimia Tanzania kuridhia Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria, (*The Protocal for Sustainable Development of Lake Victoria Basin).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Hoja na Azimio vimewasilishwa. Sasa naomba kuwajulisha kwamba mpaka hivi sasa sina orodha ya wachangiaji. Hakuna aliyeomba, kwa hiyo nafasi ipo. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti ambaye amepitia Azimio hili, Mheshimiwa Eliachim Simpassa.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO NA ARDHI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu Itifaki na Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria *(Protocol for Sustainable Development of Lake Victoria Basin).*

Awali ya yote naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ambao walihusika katika kuchambua Azimio hili. Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa - Mwenyekiti. Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa Robert K. Mashala, Mheshimiwa Masoud Abdallah, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Musa A. Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam,

Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Philip A. Magani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akiwakilisha Itifaki hii mbele ya Kamati yangu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, alifafanuwa kwa kina kuwa Itifaki hii kitakuwa chombo cha kusimamia mazingira na kukuza matumizi bora na endelevu ya rasilimali ya Ziwa Victoria na kwamba itaziwezesha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kujadili masuala yanayohusu bonde hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imechambua na kuridhika kuwa Itifaki hii ni muhimu sana kwani itawezesha bonde la Ziwa Victoria kutumika katika hali ya usawa, haki na uwiano mzuri hivyo kunufaisha wananchi wa nchi wanachama siyo tu wale wanaolizunguka bonde hilo, bali pia wote kwa jumla katika Afrika Mashariki. Aidha, itawezesha nchi wanachama kuweka mikakati ya pamoja na kubadilishana taarifa na takwimu zinazohusu vyanzo vya maji katika bonde la Ziwa Victoria ili kuendeleza usimamizi madhubuti.

Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetoa maoni kadhaa katika kuboresha utekelezaji wake. Katika kifungu cha 4, kinafafanua misingi ya usimamizi na matumizi ya rasilimali ya bonde ambapo kifungu kidogo cha kwanza kimeeleza kuwa kutakuwa na matumizi ya haki na usawa wa maji. Katika nchi zote wanachama Tanzania ina eneo kubwa la maji na bonde kuliko nchi zote zinazohusika. Hivyo, kusema kwamba tutatumia rasilimali hiyo kwa usawa kunaweza kuleta utata au matatizo baadaye.

Ili kuepusha hilo Kamati yangu imeshauri Serikali kuwa huu usawa uondolewe, yaani neno usawa liondolewe na badala yake iandikwe, “matumizi yake kuwa ya haki na uwiano nzuri.” Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali au kupitia kwa Mheshimiwa Waziri ilikubali kufanya hivyo katika kifungu hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 48 kinahusu msimamo wa nchi wanachama juu ya uhusiano kati ya Itifaki hii na mikataba mingine au mikataba ya zamani kuhusu Ziwa Victoria. Kinasema hivi, “kama mikataba hiyo inakwenda kinyume na Itifaki hii basi mikataba hiyo ni batili kulingana na jinsi inavyopingana na itifaki hii.”

Kuhusu suala hili, Kamati inaona kwamba ili kuwa na uhakika ingefaa mikataba hiyo ya zamani iainishwe ili ile inayokwenda kinyume na Itifaki hii ijulikane au kama haijulikani basi neno kama katika mstari wa kwanza wa kifungu hicho iondolewe na badala yake iwe “endapo”, au “ikiwa”. Nafurahi vile vile kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Waziri alikubaliana na ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na vyanzo vingi vya maji na vya kuaminika. Hata hivyo bado wananchi hawafaidiki na vyanzo hivi na baadhi ya vyanzo hivi havitumiki kama inavyostahili. Lakini pia Kamati imeelezea masikitiko yake juu ya kasi kubwa ya ukataji wa miti hiyo kwa ajili ya mkaa na magogo ya biashara. Jambo ambalo limeathiri kwa kiwango kikubwa vyanzo vya maji na ukame mkubwa nchini.

Kamati inashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine zinazohusika kama vile Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji vinatunzwa hasa kwa kuwa maji yanasaidia pia katika maeneo mengine hasa katika uzalishaji wa umeme ambapo kwa sasa nchi yetu inatumia sana umeme unaozalishwa kwa nguvu za maji. Hivyo upungufu wa maji unapotokea uzalishaji wa umeme pia unaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Itifaki hii, na ukweli kwamba tayari viongozi wetu wamekwisha saini Itifaki hiyo, Kamati yangu haina pingamizi kwa Bunge lako Tukufu kuiridhia.

Kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, naunga mkono hoja hii na naliomba Bunge lako Tukufu liridhie itifaki hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Namba 43(5)(b(c) na kifungu cha 81(1), Toleo la 2004, kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la kuridhia Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria (*Protocol for Sustainable Development of Lake Victoria Basin).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, (Mb.), kwa kuleta Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuridhiwa kwani nchi yetu tayari ilishakubaliana na yote yale ambayo yamo katika Mkataba wenyewe.

Aidha, juhudi anazozichukua katika kusimamia suala zima la matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kwa manufaa ya Watanzania nayo zinahitaji kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauona umuhimu kwa Bunge letu Tukufu kuridhia Itifaki hii kutokana na maandalizi ya utaratibu ambao utaziwezesha nchi zilizomo katika bonde la Ziwa Victoria kutumia rasilimali zilizomo katika bonde hili kwa uwiano na itakavyoonekana ni haki kwa manufaa ya wananchi wa nchi hizo. Kadhalika taratibu zimeandaliwa kuhakikisha kwamba matumizi ya rasilimali hizo yanakuwa endelevu kwa kuwapo na usimamizi ulio madhubuti wa raslimali zenyewe.

Aidha, Itifaki hii inatoa msimamo madhubuti wa kupinga mikataba yote iliyoingiwa na wakoloni ambayo haina manufaa kwa wananchi wa nchi zetu. Kwa kufanya hivyo, Mheshimiwa Naibu Spika, kunazifanya nchi zetu tatu za Afrika Mashariki kuwa na nguvu na sauti moja katika kusimamia, kuendeleza na kutumia kwa umakini rasilimali zilizomo katika bonde la Ziwa Victoria kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri mengi yaliyomo katika Azimio hili lakini Kambi ya Upinzani inapenda kutoa ushauri mdogo ili kuboresha mazingira yaliyomo katika itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 3 ambayo inazungumzia kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya hifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali hususan katika maeneo ya biashara, viwanda na utalii na kadhalika, Kambi ya Upinzani inapatwa na wasiwasi juu ya wingi wa viwanda vya samaki vilivyojengwa kando kando mwa Ziwa. Hali hii inaashiria kwamba uvunaji wa samaki unaweza ukapindukia rasilimali iliyomo katika Ziwa. Hali hii inakwenda kinyume na dhamira mzima ya Itifaki yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri basi Itifaki tunayoridhia leo hii iwe ni chachu ya kulitazama suala hili kwa makini kabisa na hatua madhubuti zichukuliwe ili kuinusuru hali hii mapema iwezekanavyo kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho.

Kadhalika, Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 4 cha Itifaki kinazungumzia jinsi na orodha ya wadau mbalimbali walioshirikishwa katika utayarishaji wa Itifaki hii kupitia warsha na mikutano mbalimbali. Ni vema basi tukashauri katika kila hatua ya utekelezaji wa Itifaki hii wadau wakuu ambao ni jamii iliyomo katika maeneo hayo na ambayo ndiyo inayotumia rasilimali ya bonde la Ziwa Victoria wanashirikishwa kikamilifu.

Aidha, kambi ya upinzani ingependa kujua makubaliano yaliyofikiwa na nchi hizi tatu, Kenya, Uganda na Tanzania kuhusu Azimio hili yanaoanishwaje na programu za kuendeleza *Nile basin* hali tukijua wazi kwamba *Ziwa Victoria* ni moja kati ya vyanzo vya maji ya Mto Nile.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimepata wachangiaji wawili, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, atafuatiwa na Mheshimiwa Nazir Karamagi.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kabla sijaanza mchango, nisije nikasahau, niunge mkono Azimio hili asilimia mia. *(Makofi)*

Mimi naona tumechelewa kuleta vitu kama hivi. Na napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kuleta Azimio hili. Sasa ndiyo ninakubali kwamba kweli kuna askari wa miavuli. Lakini askari wa miavuli wakitelemka wanapiga, siyo wanatelemka tu halafu ndiyo wanapigwa, haina maana. Wakitelemka wanapiga siyo mchezo. Maana Watanzania tuna mipango mizuri sana. Lakini utekelezaji wake una matatizo. Sasa katika hili isiwe tumepanga vizuri lakini kwenye utekelezaji ikawa tabu. Ndiyo majeshi, askari wa miavuli wametelemka halafu hawapigi wanapigwa.

Mimi nina imani kwamba miavuli hii na kama mingine ilivyotelemka itafanya kazi yake barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba uzoefu utakaopatikana katika utekelezaji wa hili basi uhamishiwe pia katika maeneo mengine ya mabonde maarufu tuliyonayo hapa nchini, kama Nyasa na Mto Ruvuma, Mto Rufiji na kadhalika. Naishauri Serikali kutumia nafasi hii katika ule mpango wa *irrigation.* Wala si vibaya tukienda kujifunza kwa wenzetu kama Egypt, njia bora za kumwagilia. Mimi nashangaa tuna mabonde kama Rufiji, Ruvuma, lakini mwaka jana tumeathirika na njaa kiasi ambacho kwenye jimbo langu la Mtwara kuna watu wamepata ulemavu kwa ajili ya kula vitu vya ajabu ajabu wakati wa njaa, wakati tuna mabonde ya kumwaga.

Kwa hiyo basi, naiomba Wizara iwe imepata vyanzo vya utekelezaji wa ule mpango wa kilimo cha umwagiliaji. Naishauri Serikali kwamba iache uvivu wa kutekeleza isiwe inapanga tu, ili tufaidike na rasilimali tulizonazo isiwe inawaacha wanafaidika wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba na mabonde mengine pia yatumike hasa tutakapopata uzoefu katika utekelezaji wa Itifaki hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda kuchukua nafasi hii vilevile kumpongeza Waziri, Ndugu Lowassa kwa itifaki hii aliyotuletea hapa mezani ambayo kama msemaji aliyepita ni kwamba kweli ingekuwa imefika zamani kwa sababu hii inaanza kuleta nuru katika hizo *areas* zote ambazo zinazunguka *Lake Victoria*. Sana sana ukiwepo Mkoa wa Kagera. Kikubwa ambacho nataka kuchangia hii Itifaki ni nzuri na kwamba tunaingia na nchi nyingine ambazo ni Uganda na Kenya. Na tunavyoingia tunajua kila nchi ina mipango yake na kila nchi itapanga jinsi ya kuwanufaisha wananchi wa nchi hizo.

Kwa hiyo, na sisi kama Tanzania tunapoingia katika mikataba hii ambayo inahusiana na nchi nyingine tukirudi nyumbani lazima tuwe na mikakati ambayo tumeiweka hususan kwa kufuata ule mkataba tuliosaini, namna gani tutaweza kupata ile *advantage* kubwa ya ule mkataba tuliouweka.

Nikiangalia Ziwa Victoria eneo kubwa liko Tanzania. Lakini kwa mfano kama *Article Number* 8 iliyokuwa inazungumzia *Sustainability development management of fisheries resources,* samaki hawana mipaka. Sasa hivi ukienda, wavuvi wa *Lake Victoria* wanaanza kupata matatizo na upungufu wa samaki. Na wakati mwingine inatokea kwamba labda sehemu ya Tanzania inaweka sheria za kufuata katika uvunaji wa hao samaki, inatokea kwamba nchi nyingine labda haifuati. Kwa hiyo, nchi kama Tanzania tutaathirika, siyo kwa sababu tu ni sababu yetu labda kwa nchi nyingine.

Kwa hiyo, mikataba kama hii ikiwepo inatupa nafasi nzuri ya kuweza kuwapa Mawaziri wetu, maofisa wetu wanapoingia kwenye kuhakikisha kwamba hiki kitu kinalindwa kwa kufuata Itifaki yetu. *(Makofi)*

Kuna *Articles* nyingine ni nzuri ambazo kwa upande wa Kagera, ukifika Kagera kuna mabonde makubwa ya *Nile,* ina hali ya hewa nzuri. Mvua zinanyesha mpaka sasa hivi. Lakini wananchi ni maskini. Sasa vitu kama hivi vinapotokea ndiyo sababu naomba mikakati ya Serikali kwa sababu haya mambo ya *promotion* ya *trade, commerce industries* na kila kitu kinahitaji uwe umeandalia miundombinu. Usipoweka miundombinu mizuri maana sana sana hapa tunawaangalia sekta binafsi ije iwekeze katika hizi *trade, commerce*. Serikali haiwekezi katika vyote hivi. Tunaangalia miundombinu.

Kwa hiyo, tutaomba hata sekta nyingine za Serikali ziunge mkono Wizara ambayo imetuletea hizi itifaki. Hapa ziunge mkono ili baadaye tusije tukawalaumu, mbona hivi, kwa sababu Serikali peke yake haiwezi kufanikisha. Waungwe mkono na sekta nyingine waanze kuimarisha miundombinu kusudi na sisi Tanzania tuweze kunufaika na Itifaki hii. Katika hiyo, nina maana kwamba mawasiliano yaboreshwe ikiwa ni simu za mikononi na *land line,* umeme ambao utasaidia katika mambo ya umwagiliaji na viwanda, barabara na kadhalika. Sasa hivi tuna bahati kwamba barabara zimeanza kutengenezwa, kuunganisha nchi nyingine, tunashukuru.

Bandari ambazo ziko maeneo hayo, ziingizwe katika mikakati hiyo ya kunufaika na hizi itifaki, hata na viwanja vya ndege. Tukifanya hayo yote tukiyaweka katika mkakati na kujiwekea muda tutakuwa tumetumia fursa hii ambayo tunapewa katika Itifaki hii namna gani ya kuboresha maeneo hayo na sisi tukaingia katika ushindani mzuri na zile nchi ambazo tumeingia nazo katika Itifaki. Tukizingatia kwamba nchi zilizotuzunguka sisi ambao tuko katika maeneo ya *Lake basin* ambayo yana *Lake Victoria Basin,* tunajua kwamba Uganda wana mji mkubwa ambao ni Kampala-Entebe.

Kwa hiyo, watakuwa na *base* kubwa tayari ya kuweza kushindana na sisi. Kenya wanayo Kisumu, imezuka pale juu, wamejitayarisha vizuri. Sasa sisi tukiwa dhaifu, tusipoweka miundombinu yetu sawasawa ambayo inalingana ama inazidi ya wenzetu tutajikuta kwamba hatutanufaika kwa sababu tumeingiza utandawazi, biashara yetu itakwenda bila ya kuangalia mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache ndiyo mchango wangu katika Itifaki hii. Naiunga mkono hoja hii moja kwa moja. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Edward N. Lowassa kwa kuleta hii itifaki ili tuweze kuiridhia. Ukweli Mheshimiwa Naibu Spika, hii kazi ilitakiwa kufanywa miaka mingi tu resources inayozunguka Ziwa Victoria imekuwa ikitumiwa vibaya na nchi kadhaa inayoizunguka. Tulikuwa hatuwezi kuuliza lakini kufuatana na mkataba huu unaposoma *Article 15* anasema, "*.. when utilising the resources of the Basin in its jurisdiction, take all appropriate measures to prevent significant environmental harm to other Partner States*." Hii ni muhimu sana ni kwamba sisi tukitumia vibaya hapa basi wenzetu watakuwa na haki ya kutuuliza huku Kenya ama Uganda na hili ni jambo la muhimu,

*environment* ni jambo la kulinda. Vilevile ukifanya *pollution* wanasema kwamba unaweza kulipa. Sasa haya ni mambo ya mwanzoni kabisa.

Lakini kitu ambacho tunataka kusema kuhusu *Lake Victoria,* sisi haya maji yapo hapa kwetu. Juzi nilikuwa naenda Brussels, nikakaa kwenye dirisha nikawa naangalia Mto Nile. Nilipofika kule Sudan mambo yanakwenda, kufika kule Cairo unaona tu umwagiliaji safi. Leo pale kwa Mheshimiwa Professor Phillemon M. Sarungi pale Kineti, kwanza hana maji ya kunywa watu wanalala njaa. Serengeti ambayo iko kilomita 6 kutoka pale hatuna maji ya kunywa, ng'ombe wanakufa, maji yamejaa *Lake Victoria.* Ukija huku Mgango hamna kitu. Sasa kweli tunaweza kuacha maji kuyatumia kusema kwamba kuna mikataba iliwekwa na wakoloni si uhuru ulishapatikana na uhuru ulipopatikana na mikataba ya kikoloni iliishia pale na Mheshimiwa baba wa Taifa alisema Umoja wa Mataifa kuwa mikataba hiyo ameifuta. Leo tunaiheshimu mikataba iliyowekwa na wakoloni, watu wanakufa na maji yanaonekana kwenye *Lake Victoria.* Tunaomba Serikali kwa heshima na taadhima ichukue hatua ya kuhakikisha kwamba maji ya *Lake Victoria* yanatumika kwa ajili ya Watanzania. Hiyo mikataba ilikwishaisha, Baba wa Taifa alishaifuta, leo nashukuru maji yanakuja Shinyanga.

Kwa kweli Shinyanga imekuwa na matatizo ya kupata maji lakini wapo watu wengine je? Serengeti maji yako wapi? Mto Mara unapita pale kwetu unakwenda kumwaga maji *Lake Victoria,* yanapita kule, yanakwenda Misri. Afadhali yangetumiwa na watu wa Shinyanga lakini kwa kweli Mheshimiwa Spika, *resource* hii *we need to use it*. Tusikae wewe maji ukipita kwenye jangwa unaona angalia pale Sudan mambo yalivyo. Sisi tumelala mikataba hiyo ilikwishaisha Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha tunatumia maji *for Irrigation* kwa ajili ya kunywa na mifugo. Namshukuru Mheshimiwa Lowassa kuna siku moja ulitamka ukasema hii ilikwishafutwa na Baba wa Taifa na ukaenda huko na hakika unafanya maandalizi mazuri, maji lazima yatumike kwa Watanzania na muda ni huu. Baada ya kusema hivyo Mheshimiwa Naibu Spika hiki siyo kitu cha kupinga wakubwa wetu wameshasaini hapa, kwa hiyo, mimi nakubaliana na naungana mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango mzuri wa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Waziri kufafanua vizuri Azimio hili, nimesimama kutoa ushauri wa mambo matatu:-

(i) Naipongeza Serikali kwa kupokea ushauri wa ile Kamati kwamba matumizi ya ziwa hili yaangalie uwiano wa ukubwa wa ziwa. Katika nchi hizi tatu tunaishi karne ya 21 tuwe waangalifu tusifanye mikataba kama ile ya Carl Peters. Tunaweka mikataba bila ya kuelewa madhara yake na maana yake na baadaye tunakuja kujikuta tumeuza nchi. Kwa hiyo, hili nawapongeza sana wenzetu Wanakamati kwa niaba yetu.

(ii) Ziwa Victoria nadhani ni ziwa la tatu kwa ukubwa katika dunia, la pili! nawashukuru kueleweshwa. Fikiri kama nchi tatu hizi zisingekuwa na Ziwa Victoria kwamba ingebidi tutengeneze barabara ya kwenda Kenya, Uganda, Kongo, ya kwenda wapi lakini tumepewa maji na tunapitisha vyombo vya usafiri bila ya gharama ya kuhudumia kila wakati kama tunavyohudumia barabara ambazo zinachakaa. Kwa hiyo,

ni bahati tuliyopewa na Mwenyezi Mungu na tunatakiwa kuitumia vizuri. Ni bwawa la Mungu, ni bwawa la asili la Mungu hatuna bwawa kubwa la namna hiyo. Hebu fikiria hawa watu wanaokaa kuzunguka ziwa lile wasingekuwa na Ziwa Victoria na hali ya ukame ilivyo hali ingekuwa mbaya sana. Leo tuna ziwa kubwa la maji linazungukwa na watu wengi pale na wanategemea maji kutoka kwenye Ziwa Victoria. Lakini hatuelewi. Kwa hiyo, nalo tungekuwa ni vizuri wenzetu wanaokaa katika eneo lile waangalie kwa undani maana ya vitu hivi sielewi ni kwanini lakini mimi ninatoka Iringa.

Kule Iringa tunatumwagilia maji kutoka kwenye mito ambayo ina kina kirefu sana kutoka kwenye nchi kavu. Lakini mimi nimepita Ziwa Victoria ninakuta maji yako karibu sana na nchi kavu lakini hakuna hata bustani moja. Mimi sikuelewa lakini inahitaji kuangalia wenzetu hivi haielewi kwamba maji yale ya mvua ndio haya ya ziwa Victoria yanakuwa ukimwagilia mimea unaweza kupata mazao. Nilikuwa nasoma mtaalamu mmoja wa Asia akielezea hali ya watu wa dunia ya tatu kwamba wanavyotaka wakati wanataka kulima wanapiga magoti kwenye maji wakimwomba Mungu awaletee mvua huku wamepiga magoti kwenye maji. Badala ya kumwomba Mungu awasaidie kutumia maji ya ziwa, mito iliyoko ili waweze kuendeleza kilimo. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hiyo Sali wenzetu wa eneo lile wangemwomba Mungu awasaidie awape akili ili watumie vizuri Ziwa Victoria kwa maana ya kiuchumi kama Azimio linavyosema.

(iii) Lingine ambalo nilitaka kusema ni Ziwa Victoria ndio kielelezo pekee ambacho nchi hizi tatu zimeunganishwa, hakuna kingine *natural* yaani Kenya, Uganda na Tanzania. Hakuna kitu kingine kinachounganisha katika nchi hizi tatu kwa urahisi kama Ziwa Victoria. Sasa kitu kizuri kama hiki lazima kitunzwe.

Nilikuwa napendekeza kwamba mikakati ya kupanda miti kuzunguka Ziwa Victoria na kulifanya liwe kivutio cha utalii, ingekuwa ni jambo la maana sana. Leo Kilimanjaro, Mlima wa Kilimanjaro unatoweka kutokana na vitendo vya binadamu vya kuharibu mazingira. *The biggest enemy of the human environment is man himself.*

Sasa sisi ni maadui wa Ziwa Victoria, kilimo kuzunguka ziwa lile, ukataji wa miti ufugaji wa ng’ombe unazidi kuharibu Ziwa Victoria. Inasemekana hata yale magugu maji kwa upande fulani ni matokeo ya kilimo na mbolea inayozunguka katika eneo lile la Ziwa Victoria ndio yamesababisha kustawishwa kwa magugu maji ambayo yanapunguza umuhimu na yakiachwa vilevile yatafanya matumizi wa ziwa hili yawe magumu sana kwa siku za usoni. Nashukuru nchi za Afrika Mashariki zimeunda mradi wa pamoja wa kuondoa magumu katika ziwa Victoria. Kwa hiyo, naomba utunzaji wa ziwa hili utiliwe maanani katika Azimio hili sipati kutazama kwamba hata vitu vingine lazima vitunzwe. Upandaji wa miti upya, na hata miti iliyopo na hata kilimo utaalamu utolewe aina gani ya kilimo na umbali gani kutoka kwenye maji kusudi ziwa liweze kuendelea kutusaidia kwa muda mrefu zaidi.

Kama walivyo, mbuga za wanyama wa porini, Kilimanjaro, njia nzuri ya kupata fedha kwa mlima wa Kilimanjaro ni utalii. Tukiruhusu wenzetu wanaokaa jirani pale walime mlima wote ule watapata pesa kidogo kuliko watu wanaokuja kuangalia ule

mlima. Vilevile kwa Ziwa Victoria nadhani ni muhimu sana lakini ziwa hili lina faida kubwa zaidi, samaki, maji yenyewe, mandhari, hata hali ya hewa inatuzwa na ziwa hili.

Mwisho Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Ndugu Waziri kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenzangu pale, kwa uamuzi wake wa kutumia maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya Watanzania. Haya mambo ni ya ajabu ajabu. Wewe unaweka mkataba kwamba ukitaka kutumia maji ya Ziwa Victoria upate idhini ya watu kutoka mbali, kule mwisho wa dunia, mwisho wa Afrika, wakati maji yanatoka kwenye nchi yako. Hivi watu wako watakuelewa? *What a poor way of dieing*? Yaani uwe unakufa tu, hivi maji unayaona yanakwenda huko, unaambiwa kuna mkataba uliwekwa na mkoloni au sijui na nani, ukitaka kutumia lazima ukaombe hii idhini ya kwenda mpaka kule wakati una maji!

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa kwa vile wameamua kupeleka maji Shinyanga, Wajerumani walikuwa na mpango wa kuleta maji mpaka hapa Dodoma, hivyo kwani nini tusifanye hivyo? Tuwe na mkakati, hela unayotumia kuleta maji Shinyanga ni kidogo sana ukilinganisha na madhara ya watu wale bila maji. *Central* Tanzania Tabora, Shinyanga, Dodoma, hili eneo lote tungebadilisha hali ya watu kwa kuleta maji pamoja na kujenga mabwawa mengine yanayofanana na Ziwa Victoria.
Hivyo, mimi nimesimama hapa kuunga mkono Azimio hili na vilevile na kuwaomba Watanzania wajifunze kulinda mali hii waliyopewa wasije wakadhani zitakuja tu, Mungu haendelei tena kuumba nchi. Tanzania ukubwa wake ni ule ule na kwa jinsi tunavyozidi kuongezeka inazidi kupungua. Kwa sababu hiyo, tusipotunza hiki tulicho nacho tutashindwa kufanya mambo mengine.

Miti ni ya lazima, leo umeme unazidi kwisha, *we don't have re-courage ku-implement decisions* ambazo ni *unpalatable.* Kila mtu analia ukame, maji yanakauka, mito inakauka kutokana na ukosefu wa miti, lakini tunaangalia, watu wamenyamaza tu! Watu wanalima bustani mpaka kwenye vyanzo vya maji halafu wanadai maji kwa Waziri Lowassa wakati wenyewe wanaua misingi ya uhai wao. Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kuongoza majadiliano ya kuridhia mkataba huu na napenda kuwashukuru sana Wabunge ambao wamechangia na kuwashukuru hata wale ambao wamekaa kimya.

Waliochangia ni Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Eliachim J. Simpassa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mhe.Mwadini Abbas Jecha, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa James M. Wanyancha, Mheshimiwa Jackson Makwetta, na kwa maandishi amechangia Mheshimiwa Semindu Pawa. Nawashukuru wote kwa michango yao. Sikusudii kuijibu kwa sababu ilikuwa inaboresha mkataba, ila nitapitia maeneo machache tu na mimi kujaribu kuyaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati amezungumzia suala la mikataba ya zamani iainishwe. Mheshimiwa Mwenyekiti ulizungumza jambo hili kwenye Kamati na nilitoa maelezo ambayo ningependa kurudia kuyatoa hapa kwamba katika zile nchi kumi za bonde la Mto Nile ambalo tuna mikutano ya pamoja ya Mawaziri wa bonde hilo, tunatazama upya mikataba ile iliyokuwa inatawala matumizi ya maji ya Mto Nile. Na mtakumbuka Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuja Bungeni hapa tukaeleza msimamo wa Serikali ya Tanzania, kwamba hatuitambui mikataba ile kwa sababu haikutungwa kwa niaba yetu na hawakuwa na haki ya kututungia mikataba ile. Kwa hiyo, nchi hizi zimekuwa zikikutana, tumekuwa tunakutana na wataalamu. Wataalamu wetu wemeshakutana mara tatu kule Itebe na wanakutana kikao cha mwisho mwezi Februari, 2005 kumalizia mkataba mpya utakaoongoza hizi nchi kumi juu ya matumizi ya Mto Nile. Kwa hiyo, huu ndio msimamo juu ya mikataba ya zamani.

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, ni vianzo vya maji. Nakubaliana sana na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Makwetta na wote wale waliozungumzia juu ya vianzo vya maji. Ningependa ieleweke wako watu wanaotabiri kwamba vita vikuu vijavyo duniani vitapiganwa kwa sababu ya maji na dalili zote zinanaonekana hivyo. Kwa sababu tatizo la maji kila mahali, maji yanapungua, vianzo vyetu vyote vya maji Tanzania vinapungua haviongezeki. Na kinachonitisha Mheshimiwa ni sisi kutotambua kwamba vyanzo vya maji vinapungua. Viongozi kila wa Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa, Taifa, tupo na tunaona vyanzo vinaharibika wote tumenyamaza.

Vianzo vinachomwa moto tunanyamaza, mifugo inapelekwa kwenye vyanzo tunanyamaza. Kwenye vianzo wanalima, tunanyamaza! Sasa jamani tukikosa maji kama anavyosema Mheshimiwa Makwetta, ni tatizo ambalo tumejisababishia sisi wenyewe. Naomba kutoa wito kurudia tena kutoa wito kwa viongozi wa ngazi mbalimbali na wananchi wenyewe tutunze vianzo vya maji. Vianzo hivi haviongezeki na tusipovitunza sisi watakaoumia ni sisi na vizazi vijavyo. Msemaji wa kambi ya Upinzani amezungumzia juu ya suala la Afrika Mashariki kwamba linahusikaje na zile nchi za Nile. Kama nilivyoeleza kwenye Kamati siku ile nimesema katika mkataba, moja ya kazi tuliyopewa ukitazama ule mkataba tumeambiwa, *we must negotiate as a block.* Tunapozungumza juu ya maslahi katika bonde la Ziwa Victoria katika bonde la Mto Nile, sisi wa Afrika Mashariki tunazungumza kama *block* na inakurahisishia katika mazungumzo badala ya kuzungumza kama Tanzania peke yake, Kenya peke yake, Uganda peke yake. Mnazungumza sauti moja ya Afrika Mashariki na *ku-negotiate as a block*, imetusaidia sana hata kwenye mazungumzo ya mkataba huu wa Nile ambao unaendelea. Kwa hiyo, nafasi ya Afrika ya Mashariki ipo katika mazungumzo na nasema inaendelea vizuri, tumekubaliana vizuri nchi zote tatu, tuna msimamo na mazungumzo yetu yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Namkulala, nakubaliana na hoja zako kwamba tujifunze juu ya kilimo cha umwagiliaji. Nadhani mwaka huu moja ya vitu ambavyo tumesema kwa nguvu sana Bungeni ni suala la kilimo cha umwagiliaji. Waziri wa Kilimo amelielezea na Bajeti imetengwa na kwa kweli ndio ukombozi wa nchi hii. Kilimo cha umwagiliaji ndio ukombozi wa nchi hii. Tulipokwenda Misri Mwandishi Mmoja wa habari alichukua

ramani ya Tanzania akasema nyie watu wa ajabu sana mnakazana kufuata huu mto tu, hebu angalia nchi yenu ilivyojaa mito, akaonyesha mto Ruvuma, Ruvu, Ruaha, Malagalasi na kadhalika. Hii ni nchi ambayo tumejaa mito lakini jamani hatuitumii mito hii vya kutosha. Tungekuwa tunaitumia mito hii vya kutosha leo Tanzania isingekuwa nchi inayouziwa chakula hata kidogo. Hawa Wamisri wana huo mto mmoja lakini leo wanalima chakula na wanapeleka nje.

Kilimo wanachofanya kwenye jangwa kutokana na kilimo cha kisasa cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba jamani tujitahidi tutumie mito ambayo tunayo katika nchi yetu. Katika nchi ambazo Mungu amezibariki kuwa na mito mingi ni Tanzania. Ningeomba azidi kutubariki pia jinsi ya kuyatumia maji haya. Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, nakubaliana sana na hoja zake, sekta binafsi na kwamba samaki hawana mipaka. Lakini suala la miundombinu katika ziwa linawekwa katika miradi iliyo *Nile Com,* tunatazama suala la umeme sehemu ile ilikuwa na Rubada, sasa Rwanda na Burundi kule kuna kupitia mto Kagera, tunategemea kuanzisha shughuli za umeme pale. Lakini vilevile ningependa kulijulisha Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba chini ya utaratibu wa Habitat tumebuni miradi ya maji inayozunguka ziwa Victoria kwa ajili ya ile miji yote inayozunguka Ziwa Victoria. Tumepata kiasi cha pesa Mheshimiwa Anna Tibaijuka Mtanzania aliyeko kule *Standard Chartered* ametusaidia sana, tunaendelea kuisukuma na tunategemea tutapata fedha za kutuwezesha kupata maji kwa ajili ya miji inayozunguka Ziwa Victoria. Kwa hiyo kazi inaendelea Mheshimiwa Karamagi. Mheshimiwa Semindu Pawa, nchi za Maziwa Makuu zina ushiriki upi. Katika mkataba huu, nikiri kwamba Burundi na Rwanda kwa mahesabu ya kuwa katika ziwa wangekuwepo lakini kwa sababu bado maombi yao ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hayajakubaliwa nitashauri tungojee mpaka hapo watakapokuwa wamekubaliwa na busara za viongozi wale ndipo watapoingia katika mkataba huu.

Mheshimiwa James M. Wanyancha, nakubaliana na maelezo yake yote lakini katika bonde hayo maji ya mto Mara unayasema vilevile katika miradi ya *Nile Com* tumepanda kilimo cha umwagiliaji katika Mto Mara wakati wowote watakapopata pesa tutaanza kilimo cha umwagiliaji katika maji ya Mto Mara. Kutotumia maji ya ziwa Victoria nasema tumeanza kutumia maji ya ziwa Victoria na nitumie nafasi hii tena kumshukuru sana Rais Benjamin William Mkapa kwa kukubali kwa ujasiri wake na umahiri wake wa kukubali tutumie maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Bajeti inayopeleka maji miji ya Kahama na Shinyanga ni shilingi bilioni 85 na zote ni pesa za Bajeti ya Tanzania na kwa kweli ni uamuzi wa msingi sana. Ila ningependa kulijulisha Bunge hili kwamba katika kuusanifu mradi, tumeweka maji yaelekee Shinyanga na Kahama lakini yanapofika pale mwelekeo wa Nzega na Igunga, bomba liwekwe "T" ili wakati wowote tukipata pesa tutayasukuma maji yale kwenda Igunga, Nzega na ikiwezekana mpaka Singida. Tuombe Mungu aendelee kutuweka na fedha zipatikane mambo yatajipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jackson M. Makwetta nakubaliana na wewe hatuna makali katika kubuni upya miradi hii. Wanaokwenda ni vijana wa Tanzania wasomi kabisa waliobobea

katika nyanja mbalimbali za sheria na mambo ya maji na kwa kweli wataalamu Watanzania wanaokwenda kwenye mikutano hii lazima niwasifu ni vijana hodari sana na wanatuwakilisha vizuri. Nakubaliana nawe kwamba tunaweza kulifanya Ziwa Victoria likawa kituo cha utalii na hakika Waziri mwenzangu amesikia. Lakini napenda kukutoa hofu kwamba magugu maji kwa kiasi kikubwa sana katika eneo la Tanzania la Ziwa Victoria tumeyadhibiti sana na Mheshimiwa Waziri wa Mazingira hayupo lakini angekuthibitishia kwamba hali inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge wameboresha, ninawashukuru sana kwa jinsi walivyoimarisha hoja yetu naomba sasa nitoe hoja ili Waheshimiwa Wabunge waukubali kuuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Itifaki kuhusu Maendeleo endelevu katika Ufuko wa Ziwa Victoria lilipitishwa na Bunge)*

**MHE. NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Hoja yenyewe ni Bunge liridhie Azimio la Itifaki kuhusu maendeleo endelevu katika ufuko wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Baada ya kufika hapo tumemaliza shughuli za leo na sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 10:54 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 4 Novemba, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*